# Nipashe

Jumanne Desemba 31 , 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580115

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Watu sita wapoteza maisha wakati lori likikwepa shimo

UKURASA 2




UKURASA 13

RIPOTI MAALUM

# Uhaba walimu janga la elimu

**SHULE** nyingi zina upungufu walimu wa sayansi, moja haina mwalimu wa Fizikia tangu 2015...*Endelea ukurasa wa 4*



Wakazi wa mikoa ya Mbeya na Tabora wakishuhudia Mto Lupa ukiwa umejaa maji kutokana na daraja kuvunjika, baada ya lori lenye uzito mkubwa kupita. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya iliamua kuifunga barabara ya Mbeya-Tabora kwa wiki mbili kupisha ukarabati wa daraja. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Matatani kwa tuhuma za kulawiti watoto 24

UKURASA 2

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**DODOMA YAKUMBWA UPUNGUFU WA DAMU**

MKOA wa Dodoma unakabiliwa na upungufu mkubwa wa damu hali inayohatarisha uhai wa wagonjwa wanaohitaji kuongezewa damu kwenye hospitali mbalimbali...

**UKURASA WA 3**

**LIPUMBA ADAI UCHUMI ULIKUWA MGUMU 2019**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amedai mwaka 2019 ulikuwa mgumu kiuchumi na kisiasa nchini...

**UKURASA WA 5**

**CHADEMA YASISITIZA KUUNDA SERIKALI TATU**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeeleza mipango yake katika uchaguzi mkuu wa 2020 iwapo kitashinda kwenye uchaguzi...

## ADAIWA KUKUTWA NA SARE ZA JWTZ

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store


**MICHEZO** NYOTA WA YANGA IKIIVAA SIMBA KUPEWA GODORO UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Matatani tuhuma kulawiti watoto 24

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

MKAZI wa Mtaa wa Semtema 'A" Manispaa ya Iringa, mkoani Iringa, Arnold Mlay, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuwalawiti watoto 24 wa kiume.

Imeelezwa kuwa wengi wa watoto hao ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika eneo hilo.

Taarifa zinaeleza kuwa watoto hao wanadaiwa kulawitiwa katika kipindi cha miaka mitatu na mtuhumiwa huyo.

Akizungumza na wananchi wa mtaa huo, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alieleza kushtushwa na ukubwa wa tatizo hilo na kuamua kuchukua hatua ikiwamo kuunda kamati ya watu 10 kwa ajili ya kufuatilia na kubaini watoto ambao wamefanyiwa ukatili huo.

Kasesela alisema kuwa mtuhumiwa huyo alikuwa na michezo ya kompyuta, na kwamba alikuwa akiwarubuni watoto kwa zawadi ndogo ndogo zikiwamo fedha.

Kasesela alifafanua zaidi kuwa Mlay pia alikuwa akiwatishia watoto kuwatoa uhai ikiwa wangeruhusu mtu mwingine kujua suala hilo.

Alisema kuwa uchunguzi dhidi ya mtuhumiwa huyo ukikamilika, atapelekwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Kasesela, Mlay ni mwalimu ambaye alihitimu katika Chuo Kikuu cha Iringa, na anamiliki kituo chake cha kuchezesha michezo ya kompyuta kwa watoto wadogo katika mtaa wa Semtema 'A'.

Kasesela pia aliwataka wazazi na walezi katika Manispaa ya Iringa kuwa makini na watoto wao wanaocheza michezo katika vituo vya watoto maarufu pamoja na kuwataka kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi ili kuwafichua wanaojihusisha na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Mtaalamu wa ushauri nasaha, David Mgimwa, kutoka Kituo cha Afya Ngome, alisema wameshaanza kutoa huduma ya ushauri nasaha kwa watoto hao.




Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuwatakia kheri ya mwaka mpya Watanzania. Kulia ni Mkurugenzi wa Fedha wa chama hicho, Zainabu Mndolwa na Naibu Mkurugenzi wa Mipango na Uchaguzi, Jafar Mneke. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sita wafariki dunia kwa kuparamiwa na lori

**Renatha Msungu, DODOMA**

WATU sita wamefariki dunia katika ajali ya barabarani iliyohusisha daladala aina ya Coaster na lori lililokuwa likikwepa shimo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi usiku katika eneo la Martin Luther, jijini Dodoma.

Muroto aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Omary Mdilo, Prisca Mbaigwa, Gihali Chilangazi, Simon Mtagwa na Shukuru Ruvuwesh na majeruhi 12.

Alisema dereva wa lori alikuwa akilikwepa shimo na kuivaa Coaster iliyokuwa katika eneo lake na kufumua paa la juu na kusababisha ajali hiyo.

Kamanda Muroto alisema majeruhi waliopo wodini ni 12, kati ya hao wanawake ni wawili na wanaume 10 na wengine wakiwa chumba cha uangalizi maalumu (ICU).

Alisema baada ya ajali hiyo dereva wa lori aina ya Fuso, Joseph Zacharia (26), alitoweka lakini Jeshi la Polisi limemtia nguvuni.

Hata hivyo, Kamanda Muroto alisema dereva wa daladala hana makosa kwa sababu alikuwa katika eneo lake na lori likamfuata na kumgonga na kufumua paa la juu hali iliyosababisha vifo vya watu hao sita.

Naye Muuguzi Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Stanlay Mahundo, alisema wamepokea maiti sita wakiwamo wanaume watano na mwanamke mmoja.

Alisema kati ya hao tayari watano wameshatambuliwa na ndugu zao na kubaki maiti moja ambayo bado haijatambuliwa.

Mahundo alisema, majeruhi hao wanaendelea vizuri huku wengine wakitarajia kuruhusiwa kutokana na hali zao kuendelea kuimarika.

Alisema majeruhi wawili wengine ambao wapo ICU nao hali zao zinaendelea vizuri kutokana na huduma za matibabu ambazo wamepatiwa.

Mmoja wa majeruhi hao, Godfrey Kilimo, mkazi wa Nzuguni, alichosikia ni watu wakisema wasaidie hao bado wazima.

Alisema baada ya muda alipoteza fahamu alipozinduka alijikuta yupo hospitalini akiwa amefungwa bendeji kichwani.

"Nawashukuru sana madaktari wa hospitali hii wamefanya kazi kubwa ya kutupa huduma ili kuhakikisha tunarudi katika hali zetu," alisema Kilimo.

Majeruhi mwingine Shukuru Stephen, mkazi wa Nzuguni, ambaye ni dereva wa bajaji, alisema yeye alikuwa amelala hivyo hakusikia chochote.

Muuguzi wa zamu wodi namba moja katika hospitali hiyo, Khadija Ikaji, alisema majeruhi wote wamefanyiwa upasuaji mdogo na wanaendelea vizuri na kuruhusiwa kwao kutategemea watakavyoeleza maendeleo yao.

Diwani wa Kata ya Nzuguni, jijini Dodoma Aloyce Luhega, alisema ajali hiyo imeleta msiba mkubwa katika eneo hilo na kuwataka wakazi wa eneo hilo kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu.

# Dodoma yakumbwa upungufu wa damu

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MKOA wa Dodoma unakabiliwa na upungufu mkubwa wa damu hali inayohatarisha uhai wa wagonjwa wanaohitaji kuongezewa damu kwenye hospitali mbalimbali mkoani hapa.

Mkuu wa Kitengo cha Damu Salama Mkoa wa Dodoma, Dk. Leah Kitundya, alitoa tahadhari hiyo jana wakati alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, jijini hapa.

Dk. Kitundya alisema kitengo hicho kinakabiliwa na upungufu wa damu salama hali inayotishia uhai wa wananchi wanaofika kupata huduma katika hospitali wakiwamo majeruhi wa ajali.

"Hali ya akiba ya damu mkoani kwetu ni mbaya, hapa ninafikiria kuwaomba majeshi yetu yaliyopo mkoani hapa watuchangie damu maana hakuna watu wanaojitokeza wa kutosheleza kiasi cha damu inayohitajika," alisema.

Alitaja sababu kubwa ya kupungua kwa akiba ya damu salama kwenye kitengo hicho kuwa ni kutokana na wananchi waliokuwa wanajitokeza kuchangia damu kupungua.

Sababu nyingine ni kufungwa kwa shule za sekondari kwa sababu wanafunzi wengi walikuwa wakijitokeza kuchangia damu.

Alibainisha kuwa akiba iliyopo ya damu salama ni chupa 131 kati ya hizo 24 ndizo zilizopimwa kwenye maabara kuu.

Hata hivyo, alisema akiba ya nyingine ya chupa 1,336 bado vipimo vyake havijarudishwa kutoka maabara ya damu salama makao makuu Dar es Salaam.

Alisema kiasi hicho cha akiba ya damu salama kinahudumia hospitali zilizopo Dodoma na hasa hospitali kubwa.

Alizitaja hospitali hizo kuwa ni Benjamin Mkapa, Makole, St. Gema, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dodoma Christian Medical Centre (DCMC) na Hospitali ya Udom kitengo cha kusafisha figo.

Dk. Kitundya alisema akiba iliyopo haitoshelezi

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Fundi wa masanduku ya bati, Abdallah Mohamed, akiyapaka rangi kwa ajili ya kuwauzia wanafunzi katika soko la Vetenari Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kijana matatani kwa tuhuma za kukutwa na sare za jeshi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

KIJANA aliyetajwa kwa jina la Isaka Jakobo (20) mkazi wa Kijiji cha Shigamba, katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani Mbeya, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kukutwa na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema mtuhumiwa alikamatwa Desemba 27, mwaka huu, saa 9:00 alasiri.

Alizitaja sare alizokamatwa nazo kijana huyo kuwa ni nishani mbili, mkanda mmoja wa mkuu wa utii na nidhamu (RSM), mkanda mmoja wa kawaida na kofia mbili ambazo mbili zina krauni zenye rangi ya kijani na moja yenye rangi nyekundu, na begi moja la mgongoni.

Matei alisema kijana huyo alikutwa na sare hizo akiwa amezipakia kwenye pikipiki aina ya Boxer yenye namba za usajili MC852 BLE na kwamba bado uchunguzi unaendelea ili kujua alikozichukua na alikokuwa anazipeleka.

Alisema baada ya uchunguzi wa awali, jeshi hilo lilibaini kuwa pikipiki aliyokuwa anaitumia kijana huyo nayo ni ya wizi.

"Kijana huyo alikamatwa na askari waliokuwa kwenye doria katika eneo hilo baada ya kuwa na wasiwasi naye na walipochunguza walibaini kuwa alikuwa amebeba sare za jeshi. Sasa hatujui alikozitoa na alikuwa anakwenda kufanyia nini, lakini tunaendelea kumhoji," alisema Matei.

Pia alisema jeshi hilo linaendelea na misako katika maeneo mbalimbali ya Mbeya kwa ajili ya kukamata bidhaa zinazoingizwa nchini kinyume cha sheria zikiwamo pombe kali kutoka Zambia na Malawi.

**"Kijana huyo alikamatwa na askari waliokuwa kwenye doria katika eneo hilo baada ya kuwa na wasiwasi naye na walipochunguza walibaini kuwa alikuwa amebeba sare za jeshi. Sasa hatujui alikozitoa na alikuwa anakwenda kufanyia nini, lakini tunaendelea kumhoji," alisema Matei.**

# Lipumba adai uchumi ulikuwa mgumu 2019

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amedai mwaka 2019 ulikuwa mgumu kiuchumi na kisiasa nchini.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na waandishi wa habari, ujumbe mkuu ukiwa salamu za chama kwake kwa wananchi kufunga mwaka.

Alidai mwaka unaoisha leo ulikuwa na kile alichokiita shida kiuchumi kutokana na biashara kupungua na ajira kuwa duni, akitoa rai kwa wahusika kuweka ngumu katika kuhakikisha yanafanyika mapinduzi kwenye sekta ya kilimo ili kukuza uchumi.

Prof. Lipumba ambaye ni mbobezi katika masuala ya kiuchumi, alieleza kuwa takwimu za serikali zinaonyesha idadi ya watu maskini imeongezeka kutoka watu milioni 13 mwaka 2007 hadi kufikia milioni 14 mwaka 2018.

"Nusu ya Watanzania wamo katika dimbwi la umaskini, Tanzania inahitaji kutokomeza umaskini kwa kuleta mapinduzi kwenye kilimo. Kilimo cha korosho wameathirika na sera za serikali zilivyotekelezwa katika ununuzi wa korosho na baadhi yao hawajalipwa msimu wa mwaka 2017 na 2018.



"Wakulima wa tumbaku wamekosa soko baada ya mnunuzi mkubwa kuacha kushiriki kwa madai ya tozo na kodi kubwa," alidai.

Aliendelea kueleza kuwa mwaka 2019 ulikuwa mgumu wa kimaisha kwa Watanzania kwa kuwa kauli za 'vyuma kukaza' zilitawala zaidi, na kwamba taarifa za furaha duniani kwa mwaka 2019 zinaonyesha Tanzania ni nchi ya nne kati ya 156 kwa kukosa furaha.

"Ugumu wa biashara umepunguza kampuni mpya za biashara zinazosajiliwa nchini kutoka 8,890 mwaka 2015 hadi kufikia 5,276 mwaka 2018. Rwanda, kampuni mpya zilizosajiliwa ni 10,635 mwaka 2018 na mwaka 2015 walisajili kampuni 9,775," alidai.

DEMOKRASIA

Prof. Lipumba pia alidai Tanzania imerudi nyuma katika ujenzi wa demokrasia, akitolea mfano matokeo ya uchaguzi wa serikali za mitaa aliyodai zaidi ya asilimia 90 ya wagombea wa chama chake waliojitokeza katika vitongoji, vijiji na mitaa walinyimwa nafasi ya kugombea.

"Tulilazimika kutoshiriki uchaguzi baada ya wagombea wetu kuondolewa pia vyama vingine vya upinzani havikushiriki baada ya kunyimwa fursa.

"Ushiriki wa wananchi katika kuamua mambo yanayogusa maisha yao ni suala muhimu la maendeleo endelevu. Ni muhimu serikali ikatambua ujenzi wa demokrasia ni sehemu muhimu ya maendeleo," alishauri.

Prof. Lipumba pia aliitaka serikali kufanyia kazi kile alichokiita tatizo la watu kupotea katika mazingira yenye utata, akitolea mfano watu mbalimbali waliopotea katika mazingira hayo.

Prof. Lipumba pia alizungumzia uchaguzi mkuu ujao, akieleza kuwa CUF inajipanga kuweka wagombea nchi nzima katika ngazi zote, huku akisisitiza umuhimu wa nchi kuwa na tume huru ya uchaguzi.

"Hii ni nchi yetu, ni wajibu wetu kushiriki katika uchaguzi mkuu 2020 na tuchague viongozi watakaojenga amani, kujenga haki na uchumi utakaoongeza ajira na kuwapa furaha wananchi wote, sote tuwe ngangali katika kudai uchaguzi huru na haki mwaka 2020," alisema.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

RIPOTI MAALUM



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha (katikati), alipozuru katika Shule ya Sekondari Ziba wilayani Igunga kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo Agosti mwaka huu. **PICHA: SANULA ATHANAS**

# Uhaba wa walimu janga elimu nchini

## Miongo miwili usomaji sayansi wa kubahatisha

**Na Sanula Athanas, aliyekuwa IGUNGA**

UNAPOZUNGUMZIA utekelezaji wa wito kwa wanafunzi, hasa wa sekondari, kuzama zaidi katika masomo ya sayansi na Hisabati, kwa Shule ya Sekondari Ziba kuna kiashiria cha njia panda, ikiangukia sababu ya 'nani atawafundisha?'

Dhana hiyo ikielekezwa mahsusi kwa somo la Fizikia, mwonekano unakuwa dhahiri zaidi katika sura mbili tofauti, kati ya kipindi shule hiyo ilipoanzishwa mwaka 2000 na 2015, huku zama inayofuata ni miaka minne kuanzia 2015 hadi sasa.

Nipashe ilimpomdadisi Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Frank Milazi, alianza kutoa picha ya jumla kuhusu kile kinachojiri katika sekondari hiyo ya kata iliyoko kilometa 57 magharibi mwa Mji wa Igunga mkoani Tabora, akifafanua:

"Hapa hatuna mwalimu wa Fikizia aliyeajiriwa na serikali kwa miaka minne sasa. Shule ilianzishwa mwaka 2000. Awali, alikuwapo Mwalimu Kabahoze aliyekuwa ameajiriwa na serikali kwa ajili ya somo hilo, lakini mwaka 2015 alipandishwa kuwa MEK (Mratibu Elimu Kata) na hakuajiriwa mwalimu mwingine kuziba pengo hilo."

Ili kuhakikisha somo hilo halikwami kutokana na uamuzi wa kiserikali miaka minne iliyopita, Mwalimu Milazi anaeleza mbinu mbadala ambayo uongozi wa shule ulichukua, ni kutafuta walimu wawili wa kujitolea kwa malipo kidogo, kuziba pengo lililojitokeza.

Hata hivyo, katika kipindi cha miaka 15 tangu kuanzishwa kwa shule hiyo, mwalimu wa Fizikia aliyekuwapo, alibeba mzigo uliopitiliza kulingana na wastani wa idadi ya wanafunzi anaopaswa kufundisha.

Kisera, inaainishwa kwamba tija ya mwalimu na mzigo unaobebeka kwake ni anapokuwa na wastani wa wanafunzi 45 kwa darasa. Kwa maana hiyo, wastani unaojidhihirisha hapo ni kuwapo uhitaji wa walimu 20 sekondari ya Ziba yenye wanafunzi 914 (wavulana 317 na wasichana 597).

Kilio cha Mwalimu Milazi kinaenda mbali zaidi, akilalamika kwamba uhaba huo pia unaangukia masomo ya Kemia na Baiolojia, ambayo ndiyo wabia wakuu wa Fizikia katika sayansi, kila somo lina mwalimu mmoja.

Shule ya Sekondari Ziba kwa sasa ina jumla ya walimu waajiriwa 16 na wawili wa kujitolea, ambao ndiyo wamejikita katika somo la Fizikia.

"Kwa kifupi ni kwamba, tuna tatizo la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi hapa. Tunaiomba serikali itupatie walau walimu wanne, wawili wa Fizikia na wawili wa Kemia na Baiolojia," anapendekeza na kuongeza kilio kingine kwamba:

"Hatuna nyumba za walimu za kutosha, tuna nyumba tatu tu! Hivyo, walimu 15 hawaishi karibu na maeneo ya shule, wanaishi huko mitaani wamepanga."

### WALICHOFANYA 'DEI WAKA'

Licha ya mtihani wa uhaba wa walimu iliyonao Ziba, pia imedumu na uhaba wa miundombinu kama mabweni, bomba rasmi la maji na bwalo la chakula yanayoonekana kwa mara ya kwanza mwaka huu katika miongo miwili ya uwapo wake.

Katika matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka jana, wanafunzi wa shule hiyo walioandaliwa kwa hatua zote kwenye somo la Fizikia na walimu wa kujitolea, kuna kiwango cha ufaulu ambao 'wameambulia'.

Kati ya watahiniwa 117 katika shule ya Ziba, 48 ndiyo waliofanya mtihani wa somo la Fizikia na kati yao, 27 walipata ufaulu kuanzia alama 'D' na 21 walifeli kwa maana ya kupata alama 'F'.

Matokeo hayo yanaonesha, waliopata alama 'D' jumla yao ni 22; alama 'C' wako wanne; na mmoja ndiye alipata alama 'B', akiwa na kiwango cha ufaulu cha daraja la kwanza alama nane, akiongoza wilaya kwa shule za serikali na yumo katika orodha ya waliofanya vizuri kimkoa.

### DED ANASEMAJE?

Udadisi wa Nipashe, ulihamia kutafuta majibu yanayotoa mwanga kwa kiza kinachoikabili shule hiyo, mezani kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (DED) ya Igunga, Revocatus Kuuli, anayekiri upungufu huo akisema:

"Ni kweli pale Shule ya Sekondari Ziba hakuna hata mwalimu mmoja wa kuajiriwa na serikalini kwa ajili ya somo la Fizikia. Sisi tunapokea walimu kutoka serikalini, tatizo letu hili la uhaba wa walimu tumeshalipeleka Wizara ya Elimu (Sayansi na Teknolojia) na Ofisi ya Rais-Tamisemi, linashughulikiwa huko.

"Tatizo la uhaba wa watumishi Igunga ni kubwa, si kwa walimu tu, bali tuna uhaba mkubwa wa watumishi katika sekta nyingi. Tuna uhaba wa watendaji wa kata na vijiji.

"Kwenye sekta ya afya ndio balaa zaidi, tuna uhaba mkubwa na tumewaandikia barua Wizara ya Afya walishughulikie hili. Kuna vituo vya afya vinne hatutoi huduma za upasuaji kwa sababu hatuna wataalamu. Nafikikiri uhaba wa watumishi si tatizo la Igunga tu, bali la nchi nzima."

### HATUA ZA KIBUNGE

Wajibu mkuu wa mbunge ni kutetea maslahi ya wananchi katika eneo lake. Je, kwa shule ya Ziba amefanya nini? Mbunge wa Manonga, Seif Gulamali, anasema kwa nafasi yake, akiwa daraja kati ya mhimili wa shule na ngazi ya juu, ameshawasilisha maudhui ya kilio hicho kwa mamlaka za juu zichukue hatua.

Vilevile, anasema kwa yaliyo chini ya uwezo wake, amekuwa mbia wa uongozi wa shule na mamlaka nyinginezo katika halmashauri na uongozi wa wilaya, akitaja kushuriki ujenzi wa miundombinu kama mabweni, madarasa na vyanzo vya maji.

"Nimekuwa nikitumia fedha za Mfuko wa Jimbo na wakati mwingine za mfukoni mwangu kuhakikisha shule hii (Ziba) na nyinginezo jimboni zinajengwa," anasema na kuongeza ni matarajio yake kilio cha dai la walimu kitapatiwa majibu kutoka mamlaka husika.

Katika taarifa yake bungeni kwenye kikao cha Bunge la Bajeti Mei 22, 2017, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ilieleza kuwa Tanzania inakabiliwa na uhaba wa walimu 252,693 wa shule za msingi na sekondari.

Aliyekuwa mjumbe wa kamati hiyo, Mbunge wa Nzega Mjini, Hussein Bashe (sasa Naibu Waziri wa Kilimo), aliliambia Bunge kati ya walimu wanaohitajika, 182,899 ni wa shule za msingi na 69,794 wa sekondari.

Katika kinachoonesha uhaba huo wa walimu una mustakabali wa kitaifa, Mbunge wa Mwanga mkoani Kilimanjaro, Profesa Jumanne Maghembe, aliibua kilio cha aina hiyo katika kikao cha Bunge cha Mei 8 mwaka huu, akidai jimbo lake lina uhaba wa walimu 384 wanaohitajika haraka.

### MAJIBU YA SERIKALI

Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Tamisemi), Mwita Waitara, anaungana na sauti ya vilio vinavyopazwa kuhusu uhaba wa walimu, lakini takwimu zikiwa tofauti na idadi iliyowasilishwa na Kamati ya Bunge miezi 31 iliyopita.

Waitara ambaye ni Mbunge wa Ukonga, anatoa takwimu za uhaba walimu kitaifa kwamba ni 80,000. Kati yao, 66,000 wanahitajika kwa ajili ya shule za msingi zaidi ya 16,000; na waliobaki 14,000 ni wa kufundisha sekondari zisizopungua 4,000.

Kuhusiana na utekelezaji wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, alisema wiki iliyopita matarajio ya serikali ni kuajiri watumishi wapya zaidi ya 40,000 katika kada mbalimbali, wakiwamo walimu katika kipindi cha miezi miwili ijayo.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20, serikali imetenga idadi hiyo ya ajira ambazo zitaanza kutolewa Februari 2020, zikiwamo za kada afya na elimu ambazo zitasaidia kukabiliana na uhaba wa watumishi," anasema.

### AHADI YA OLE NASHA

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, aliyezuru Shule ya Sekondari Ziba mwaka huu, anaungana katika orodha ndefu ya wanaokiri pengo kubwa lililopo kitaaluma na anaeleza mikakati ambayo serikali inachukua.

Bila ya kutaja kipindi maalum, Ole Nasha, akizungumza na Nipashe jana, alisema serikali ilishachukua hatua ya kuajiri walimu 18,000 kwa mwaka wa fedha uliopo na inatarajia kuajiri wengine 16,000 mwanzoni mwa bajeti ijayo, akiahidi kusikilizwa kwa kilio cha Ziba.

Pia alifafanua undani wa chanzo cha uhaba uliopo wa walimu kitaifa kwa kiasi kikubwa umechangiwa na hatua ya serikali kuwafuta kazi watumishi waliokosa sifa baada ya kufanyika uhakiki, walimu wakiwa miongoni mwao.

Hata hivyo, alitoa angalizo kwamba kwa mujibu wa taratibu, mamlaka ya wizara yake ni kuibua madai na wenye mamlaka ya kuajiri ni Tamisemi, ingawaje alisisitiza matarajio ya utekelezaji.

Naibu Waziri huyo alidokeza mkakati mmojawapo wa kuongeza walimu wa sayansi, ni kuajiri kundi kubwa la wahitimu wa sayansi zaidi ya 5,000 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), watakaopewa mafunzo maalum ya ualimu.

# Chadema yasisitiza kuunda serikali tatu

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeeleza mipango yake katika uchaguzi mkuu wa 2020 iwapo kitashinda kwenye uchaguzi huo kuwa kitaunda mfumo wa serikali tatu.

Mkakati huo wa chama ulibainishwa na Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Serengeti, Esther Matiko, wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Shinyanga, wakati akitoa salamu za kufunga mwaka 2019 na kuukaribisha 2020.

Alisema muundo wa serikali tatu ndio utatoa dira ya maendeleo kwa wananchi, pamoja kuwa huru kuamua kufanya vitu ambavyo wanavitaka, kuliko kuongozwa na mtu mmoja au kikundi cha watu wachache kwa matakwa yao binafsi.

"Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), endapo tukishika dola kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020, lazima tutaunda mfumo wa serikali tatu, sababu ndio dira ya maendeleo hapa chini, pamoja na kuwa na uhuru bila kuingiliwa na chama ambacho kinatawala," alisema Matiko.

"Chadema katika Kanda ya Serengeti ambayo inaunda mikoa mitatu ya Simiyu, Mara na Shinyanga, tumejipanga vyema kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020 kushinda katika viti vyote vya ubunge, udiwani pamoja na kupata kura nyingi za urais," alisema Matiko.

Kadhalika alisema katika kuelekea kwenye uchaguzi huo mkuu, watahakikisha pia wanadai tume huru ya uchaguzi ili kusiwapo na upendeleo wa kukibeba chama chochote kwenye uchaguzi huo na wananchi wapate viongozi ambao wamewachagua na siyo kuchaguliwa.

Katika hatua nyingine alilaani kitendo cha ukamataji ovyo viongozi wa chama pamoja na kuwabambikizia kesi na kwamba haki za binadamu zinapaswa ziheshimiwe pamoja kuheshimu Katiba ya nchi ikiwa kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni.

Pia alimwomba Rais John Magufuli, kuufuta uchaguzi wa serikali za mitaa ambao ulifanyika Novemba 24, mwaka huu na kuungwa kwenye uchaguzi ujao kwa madai kuwa haukufanyika huru na haki.

Naye Katibu wa Chadema Kanda ya Serengeti, Renatus Nzemo, alitoa wito kwa wananchi kwenye uchaguzi mkuu mwakani, wafanye uamuzi sahihi wa kuchaguza viongozi sahihi ambao watawaletea maendeleo.



Mtoto akiangalia nyumba zilizobomolewa na maji eneo la Mabibo Relini, kutokana na mvua iliyonyesha mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam.
**PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri ataka matamasha msimu wa utalii

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewataka wadau wa utalii kuhakikisha wanafanya matamasha ya kukuza na kuendeleza sekta hiyo wakati wa msimu wa utalii.

Kwa kufanya hivyo watawafanya watalii kushiriki katika matamasha hayo licha ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii.

Akizungumza juzi wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Utalii la Lamadi litakalomalizika kesho katika Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, Kanyasu alitaka tamasha hilo lifanyike katika kipindi kijacho wakati wa mfumuko wa watalii ili watalii wote wanaotoka katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti washiriki.

Alisema lengo la tamasha hilo ni kuwafanya watalii kushiriki moja kwa moja kupitia ngoma za asili, mavazi ya kitamaduni na vyakula vya kiasili hali inayowafanya watalii kukaa kwa muda mrefu nchini.

Kanyasu alisema tamasha hilo lina umuhimu kwa vile linatoa fursa kwa watalii baada ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyo karibu na wilaya hiyo kupata fursa ya kujumuika na jamii kupitia utamaduni wa makabila mbalimbali nchini.

Kanyasu aliwataka waandaaji hao kuliandaa tamasha hilo kwa kuvialika vikundi vya ngoma kutoka pande mbalimbali za nchi badala ya kuwa na vikundi vichache vya kutoka sehemu moja. Katika hatua nyingine, Kanyasu amempongeza Mkuu wa Wilaya ya Busega, Tano Mwera, kwa kuwa na mawazo ya kuanzisha tamasha hilo ambalo litachagiza utalii kwa wananchi wa kawaida baada ya watalii kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Aliwataka wakuu wa wilaya zingine kuandaa matamasha ya utalii kwa ajili ya kukuza utalii katika wilaya zao, hali itakayosababisha watalii kukaa muda mrefu, hivyo kusababisha jamii kunufaika.

Kwa upande wake, Mwera ambaye ni mwenyekiti wa tamasha hilo, alisema tamasha hilo litachagiza utalii wa ndani na kuwafanya wananchi kuwa mabalozi wa vivutio vya utalii.

Pia alisema tamasha hilo litasaidia kuamsha ari ya wananchi wanaoishi karibu na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kushiriki kwenye shughuli za utalii hali itayowasaidia kujiongezea kipato.

## Walimu 16,000 kuajiriwa mwakani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatarajia kuajiri walimu 16,000 katika mwaka ujao wa kalenda ili kukidhi tatizo la uhaba wa walimu hususan wa Sayansi katika shule mbalimbali nchini.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, William Ole Nasha, wakati akijibu swali kuhusiana na upungufu wa walimu wa Sayansi katika Shule ya Viba iliyopo Igunga mkoani Tabora.

Nasha alisema mpango huo wa kuajiri utatekelezwa ndani ya miaka mitatu, lengo ikiwa ni kutatua changamoto ya ukosefu wa walimu hususan wa Sayansi.

Alisema mikakati walioiweka ni kuhakikisha wanaajiri ambao wanahitimu kutoka vyuoni ili kwenda kuziba mapengo yanayohitajika.

"Kuna vyuo maalum ambavyo tumevitenga kwa ajili ya kutoa walimu wa Sayansi hii itatusaidia sana," alisema Ole Nasha.

"Lakini ukumbuke waajiri ni Tamisemi, Wizara ya Elimu tunasema uhaba tulionao Tamisemi kazi yao kuajiri," alieleza.

Alisema wao wanapeleka walimu katika shule kulingana na uhitaji wa sehemu husika.

Alisema moja ya changamoto iliyochangia upungufu wa walimu ni walimu waliokutwa na vyeti feki na kuondolewa.

Alisema kulikabili suala hili itachukua muda, lakini litatatulika ndani ya miaka mitatu hadi minne ambayo wanaendelea kuajiri.

"Tutaendelea kuajiri, kufundisha na kuboresha miundombinu kwa walimu ambao wanaajiriwa," alisema Ole Nasha.

**"Kuna vyuo maalum ambavyo tumevitenga kwa ajili ya kutoa walimu wa Sayansi hii itatusaidia sana," alisema Ole Nasha.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mawakala wanaodai fedha usajili wa simu wadhibitiwe*

SERIKALI iliweka wazi mapema kwamba usajili wa laini za simu kwa njia ya vidole gumba unafanyika bila malipo yoyote.

Kwa maana hiyo kampuni zote za simu za mkononi pamoja na mawakala wake wanapaswa kutekeleza kazi hiyo bila kudai malipo yoyote kutoka kwa wateja wa kampuni hizo.

Pamoja na maelekezo hayo ya serikali, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekuwa ikisisitiza kuwa sharti pekee katika usajili wa simu ni mmiliki wa laini ya simu kuwa na kitambulisho cha taifa ambacho hutolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida).

Hayo ndiyo maelekezo ya serikali tangu kuanza kwa usajili wa laini za simu kuanzia Mei mwaka huu, na hayajabadilika hadi sasa.

Hata hivyo, kutokana na baadhi ya wamiliki wa laini za simu kuchelewa kupata vitambulisho vya taifa au namba za vitambulisho hivyo, hali hiyo ilisababisha wakati fulani msongamano wa kusajili laini za simu hususan katika maeneo ya vijijini.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya mawakala wa kampuni za simu wasio waadilifu wamekuwa wakitumia fursa hiyo kuwatapeli wananchi kwa kuwaambia kuwa bila kutoa fedha, laini zao haziwezi kusajiliwa.

Tangazo la awali la serikali kuwa laini zote ambazo hazitakuwa zimesajiliwa ifikapo leo zingezimwa, limewalazimisha wamiliki kadhaa wa laini hizo kutoa fedha kwa mawakala kuepukana na kuwa waathirika wa kuzimiwa simu.

Pamoja na wananchi kujua kuwa usajili wa laini ni bure, lakini wamekuwa wakitoa fedha kwa matapeli hao badala ya kutoa taarifa kwa mamkala husika kama TCRA na Jeshi la Polisi.

Malalamiko kadhaa yamekuwa yakitolewa dhidi ya mawakala kudai fedha, lakini bila hatua kuchukuliwa dhidi yao kutokana na mamlaka husika kupelekewa taarifa.

Malalamiko hayo yako maeneo mengi lakini kwa kutoa mfano mmoja ni baadhi ya wananchi wa wilaya za Siha na Hai, mkoani Kilimanjaro kulalamikia hatua ya mawakala wa kampuni za simu za mkononi kuwatoza fedha wakati wa usajili wa laini zao za simu ili wasajiliwe kwa haraka.

Kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki hii, tangu Rais John Magufuli atangaze kuongeza siku 20 zaidi za kusajili laini hizo, inadaiwa kuwa baadhi ya mawakala mitaani wenye mashine za kielektroniki zinazotumiwa kusajili, wamegeuza zoezi hilo kuwa fursa ya kujipatia fedha.

Walisema wanashangazwa na vitendo hivyo kwa kuwa katika matangazo ya serikali walielezwa kuwa usajili wa laini ni bure.

Mmoja wa wananchi alisema alikwenda kusajili laini zake mbili kwa mawakala wanaokaa chini ya miavuli ya kampuni za simu, na baada ya kusajiliwa aliambiwa atoe Sh. 2,000 kwamba kila laini moja nilipaswa kulipa Sh. 1,000. Kwamba alipohoji, alijibiwa kama anataka kusajiliwa bure aende kwenye maduka ya kampuni yaliyopo Moshi Mjini.

Tunaviona vitendo vya mawakala hao kufanya watakavyo kwa kudai wananchi fedha za usajili wa laini za simu ni kuidhalilisha serikali ambayo imetangaza kuwa usajili huo ni bure.

Pamoja na pongezi kwa Rais John Magufuli Desemba 27, kutangaza kuongeza siku 20 zaidi za usajili wa laini kuanzia Januari mosi, 2020 hadi Januari 20, tunashauri mamlaka husika kuingilia kati kuwakamata na kuwaadabisha wanaowadai fedha wananchi kwa ajili ya kusajili laini.

Ikiwezekana kuzibana kampuni zao kuwafungia kufanya kazi hizo kwa niaba yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tukijiandaa mapema, uhaba wa vyumba vya madarasa kwaheri



Na Salome Kitomari

**KILA** mwaka idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba kwa ajili ya kujiunga na kidato cha kwanza inafahamika, lakini kila Desemba na Januari huwa kuna changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa.

Kutokana na hali hiyo baadhi ya maeneo wanafunzi wanaanza kidato cha kwanza bila majengo na wengine kukosa madawati kutokana na uhaba.

Nakumbuka changamoto kama hii ilijitokeza Januari mwaka huu, kwa baadhi ya shule za msingi kusoma hadi saa sita na baadaye wanafunzi wa sekondari, huku shule nyingine kama Kibasila jijini Dar es Salaam zikigawanywa na kubakiwa na vyumba vya madarasa machache.

Kila kona ya nchi ilielezwa kuwepo kwa changamoto hiyo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza kukosa shule za kusoma licha ya kupangwa kwenye shule husika, huku wengine wakikosa vyumba vya madarasa.

Mwaka huu tena hali imekuwa ile ile na sasa halmashauri mbalimbali zinakimbizana kujenga vyumba vya madarasa, kutengeneza madawati na mahitaji mengine na kuifanya shule ikamilike kwa kiwango cha chini.

Hivi karibuni Tamisemi walitangaza idadi ya wanafunzi waliokosa nafasi kidato cha kwanza kuwa ni 58,699 kutokana na kukosekana kwa vyumba vya madarasa.

Kwa sasa kuna kampeni na kauli mbalimbali ikiwamo amri kwa wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha kila mwanafunzi aliyefaulu anapata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza.

Muungwana najiuliza kwanini suala hili linakuwa zimamoto kila mwaka, wakati wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza au wanaofika darasa la saba wanajulikana idadi yao kwa maana ya walioko shule binafsi na za umma?

Kwanini kila mwaka iwe ni kukimbizana dakika za mwisho na kuchukua hatua dakika za mwisho?

Kwa mfano, uamuzi wa kubadili muundo wa elimu kutolewa kutwa nzima na badala yake nusu siku ili kuwezesha wanafunzi kupishana kwenye majengo machache yaliyopo!

Licha ya halmashauri kuwa na majukumu mengi ya kusimamia shughuli za umma, lakini inapaswa kuwa na mpango endelevu kulingana na wanafunzi wanaomaliza kidato husika, vinginevyo kila mwanzo wa mwaka itakuwa zimamoto.

Ni vyema halmaushari zikatenga fungu au mfuko wa ujenzi wa shule za sekondari kwa makadirio ya idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba na kuhakikisha kama inatakiwa kuongeza darasa moja kila kata inafanyika hivyo kwa ujenzi nafuu wenye kubana matumizi.

Zipo halmashauri zimefanikiwa kujenga nyumba vya madarasa kwa gharama nafuu na kwa kutumia mafundi wa jamii, kiasi cha kuwawezesha kuondokana na changamoto ya uhaba wa nyumba vya madarasa.

Zimamoto inayoonekana sasa inawapa cha kusema wanasiasa kwenye majukwaa badala ya kwenda kwenye hoja za msingi ambazo hawajatekeleza katika majimbo yao wakati huu wa kuelekea uchaguzi mkuu.

Takwimu za wanafunzi wanaoandikishwa na wanaofanya mtihani wa darasa la saba zipo, maana yake toka wakati huo ni kiasi cha wahusika kujipanga vyema kuhakikisha hakuna mwanafunzi anakosa darasa.

Lakini kwa kukimbizana huku ndiyo maamuzi ya kugawa shule za msingi huku matundu ya vyoo yakiwa ni yale yale, na shule kupoteza ubora wa elimu inayotolewa.

Shule nyingi za 'zimamoto' huwa elimu yake haina ubora unaotakiwa, zaidi ya kuhakikisha kila mtoto amekwenda shule ili ionekane hakuna aliyebaki nyumbani.

Watoto wengi wa kike wamekuwa waathirika wa ugonjwa wa UTI unaosababishwa na matumizi ya vyoo visivyofaa, na kwamba mazingira ya kuchanganya matumizi ya choo kwa wanafunzi wadogo na wakubwa maana yake ni kuwaumiza wote na sana sana wadogo.

Akili ya mwanafunzi wa darasa la awali au la kwanza haiwezi kuwa sawa na ya mwanafunzi wa kidato cha kwanza na ndiyo maana lazima wawe na vyoo vyao.

Lazima Tamisemi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu wawe na utaratibu maalum wa kuhakikisha majengo yanakuwapo kusubiri wanafunzi na si kusubiri wanafunzi wafaulu na ndiyo wasubiri majengo yajengwe.

## BARUA/ MJADALA

# Mwenendo huu si wa kiungwana kabisa

***Mhariri***
***Habari za majukumu!***

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*


*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

*Ni muhimu watu hao wakaelewa kwamba ndani ya usafiri wa umma, kila mtu anakuwa na mipango yake kichwani kama anaenda kazini, na anahitaji utulivu kama anarudi kutoka kazini kwa sababu ya uchovu wa siku nzima na changamoto nyingine alizokutana nazo katika mizunguko yake.*

*Hahitaji kusikia kelele za namna mnavyotongozana au jinsi ulivyomchongea jirani yako kwa mumewe au jinsi ulivyomshushua shoga yako mbele ya watu.*

***Jupilo Jifenenge- Rangitatu***




# Inawezekana kuboresha elimu, kila upande utimize wajibu

**Na Sabato Kasika**

RIPOTI ya nusu mwaka ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ya kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu wa 2019 unaofikia ukingoni leo, inataja mambo manne, ambayo inayasema kuwa ni tatizo kwenye ya elimu nchini.

Mambo hayo ni bajeti finyu, uhaba wa walimu, vyumba vya madarasa na wa vyoo kwenye baadhi ya shule za Tanzania Bara, ambayo yanatajwa kuathiri haki ya kupata elimu.

Hata hivyo, katika ripoti hiyo iliyotolewa Agosti mwaka huu, Mkurugenzi wa kituo hicho Anna Henga anasema, utaratibu wa kutoa elimu bure umesaidia watoto wengi kupata elimu.

Anasema, utaratibu huo wa kutoa elimu bure licha ya kuwa na mafanikio, unakumbana na vikwazo vya ufinyu wa bajeti, uhaba wa walimu, vyumba vya madarasa na wa vyoo.

Tatizo lingine linalojitokeza ndani ya juhudi hizo za serikali za kutoa elimu bure, linaelezwa na LHRC kuwa ni kuongezeka kwa mimba za utotoni, ambazo ni kikwazo kwa maendeleo ya elimu kwa mtoto wa kike.

Mjadala huu unaamini kwamba iwapo kila upande kuanzia kwa serikali, wadau wa elimu ambao ni wazazi, ukitimiza wajibu kwenye suala hili, matatizo hayo yaliyotajwa kwenye ripoti ya LHRC yanaweza kuwa historia.

Suala la kuongeza bajeti kwenye elimu na kuajiri walimu wengi zaidi ni la serikali, lakini haya mengine ya uhaba wa vyoo na vyumba vya madarasa yapo chini ya uwezo wa wadau na hasa wazazi na walezi.

Hivyo serikali iangalie uwezekano wa kumaliza matatizo hayo kwa kushirikiana na wananchi badala ya kuendelea kuwapo kwa uhaba wa walimu ambao wakati mwingine unatokana na ufinyu wa bajeti.

Kwa upande wa uhaba wa vyumba vya madarasa na vyoo, ni muhimu jamii kushirikiana na serikali, katika kutatua tatizo hilo, ambalo lipo katika shule nyingi za umma hapa nchini.

Kimsingi shule za umma ni za wananchi wenyewe, hivyo wanatakiwa kuhakikisha wanaziboresha kadri inavyowezekana badala ya kudhani kuwa jukumu hilo ni la serikali tu kana kwamba wao hawahusiki.

Shule za umma zinahudumia karibu asilimia 94 ya watoto wa Kitanzania, hivyo suala la kuziboresha ni la muhimu, kwa ajili ya kuwasaidia kuwa na sehemu nzuri ya kujifunzia.

Yaani wadau wote wa elimu kuanzia serikali na mamlaka zake husika, wakuu wa shule, walimu, wazazi/ walezi, jamii na wanafunzi kwa ujumla wanahusika katika maendeleo ya elimu nchini.

Mjadala huu unakumbusha kwamba, hapa kila upande una nafasi yake na wajibu, kwa ajili ya kufikia malengo yaliyokusudiwa, ambayo ni utoaji wa elimu bora na tena katika mazingira bora.

Suala hili la maendeleo ya elimu, ni sawa na viungo kwenye mwili wa binadamu, ambavyo kila kimoja kina nafasi yake na haiwezekani kimoja kikajitenga kikidai hakina jukumu lolote kwenye mwili.

Kwenye tatizo la mimba za utotoni, ambalo pia limetajwa kwenye ripoti ya LHRC, ni kwamba linachangiwa na sababu nyingi ambazo sehemu kubwa ziko ndani ya uwezo wa wazazi, walezi na jamii kwa ujumla.

Mimba za utotoni zinatajwa kuwa ni tatizo, ambalo linasababisha watoto wa kike wakose haki ya kupata elimu, na inawezekana hali hiyo ikachangiwa na malezi mabovu ya baadhi ya wazazi.

Wapo baadhi ya wazazi, ambao hawawafundishi watoto wao stadi za maisha na umuhimu wa kujituma katika elimu, na wakati mwingine makundi nayo huchangia kuwapo kwa mimba hizo.

kutokana na sababu hizo na nyingine, ambazo mjadala huu haukuzitaja, ni wazi kwamba nyingi ziko ndani ya uwezo wa jamii yenyewe, lakini kwa bahati mbaya jamii imeshindwa kutimiza wajibu na kusababisha kuwapo kwa tatizo hilo la mimba.

Ripoti mbalimbali zimekuwa zikionyesha kuwa baadhi ya wazazi na walezi hushirikiana na watu wanaowapa mimba watoto wao kwa kupokea chochote, ili mambo yamalizike kimya kimya.

Kwa ujumla inawezekana kuboresha elimu nchini, iwapo kila upande utatimiza wajibu wake, kwani ripoti ya LHRC imeweka wazi hilo, hivyo ni muhimu kutambua kuwa inagusa kila upande.

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



## HABARI KITAIFA

# Ngorongoro kujenga uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), inatarajia kujenga uwanja mpya wa ndege utakaokuwa na njia ya kuruka na kutua yenye urefu wa kilomita 3.2.

Lengo la kujengwa kwa uwanja huo ni kurahisisha huduma za usafiri na utalii kwenye eneo la Ngorongoro na hifadhi za jirani kama Hifadhi ya Taifa Serengeti (Senapa).

Kamishna Uhifadhi wa NCAA, Dk. Freddy Manongi, akizungumza na gazeti hili, alisema uwanja huo utajengwa eneo la Oldivai, na kwamba utarahisisha huduma za usafiri kwa watalii wanaokwenda humo pamoja na eneo la Laetoli.

Alisema uamuzi wa kujenga uwanja huo umekuja baada ya kubaini kuwa baadhi ya watalii wanashindwa kutembelea eneo la Ngorongoro kutokana na umbali mrefu kutoka Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (Kia).

"Uwepo wa uwanja huu utaongeza idadi ya watalii wanaotembelea Ngorongoro Creta, watalii wengi wanalalamika umbali wanaposafiri kwa barabara inawachukua saa tano hadi sita," alibainisha.

Kwa mujibu wa Dk. Manongi, usafiri wa anga ndiyo suluhisho la kero hiyo pamoja na watu wote wenye mahitaji maalum na hawawezi kusafiri kwa muda mrefu kwa barabara.

Alisema usafiri huo utakuwa rahisi kwa biashara ya utalii kwa kuwa wapo watalii ambao hawataki kutumia muda mrefu bali wanataka kufika kreta kuona wanyama na kuondoka siku hiyo hiyo.

Alisema ujenzi wa uwanja huo utatumia vifaa vya kisasa kuwezesha ndege za kila aina kutua na kupaa, na kwamba Baraza la Hifadhi ya Mazingira (Nemc), linatarajia kufanya ukaguzi wa athari za kimazingira kabla ya ujenzi.

Kwa mujibu wa Dk. Manongi, Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), wameshafanya upembuzi wa awali na kupendekeza eneo la kujengwa uwanja huo na kwamba mapendekezo yaliwasilishwa kwenye menejimenti ya NCAA wiki iliyopita.

"Tumechagua kujenga uwanja huu eneo la Oldivai kwa sababu iko katikati ya Ngorongoro na Serengeti," alifafanua.

Naye mtaalamu kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TCAA), Bernard Kavishe, alisema NCAA watajenga uwanja ambao utatumia vifaa vya kisasa kuhakikisha usalama na ulinzi wa watumiaji wote, na kwamba watatoa mwongozo wote kwa mamlaka hiyo.

"Tunawasaidia kwa sababu tunatambua umuhimu wa kuwa na uwanja huu kwa manufaa ya sekta ya utalii," alisema.




Kaimu Mwenyekiti Kanda ya Pwani wa Chadema, Bakari Mwago, akizungumza na wanahabari jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Habari na Uenezi, Gerva Lyenda na Diwani Viti Maalum, Kubra Abdallah. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Dodoma yakumbwa upungufu wa damu

INATOKA UK 2

kutokana na kitengo hicho kuhudumia hospitali kubwa zenye wagonjwa wengi wanaopata ajali.

Awali, alisema walikuwa wakikusanya kiasi cha damu chupa 750 hadi 800 kwa siku, lakini kwa sasa wanakusanya chupa chini ya 20, jambo ambalo ni hatari.

Aliongeza kuwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma inahitaji chupa 25 hadi 30 kwa siku.

Pia alisema kituo cha afya cha Udom kitengo cha kusafisha figo, hawafiki kila siku kuchukua damu, lakini wanapofika wanachukua chupa nyingi kutokana na mahitaji ya wagonjwa.

Aliwaomba viongozi wa serikali kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa wanaofika kupata huduma kwenye hospitali hizo.

Alisema kitengo hicho kinapita kwenye mikusanyiko ya watu kama sokoni, kanisani, msikitini na kwenye vituo vya mabasi ili kuwahamasisha wananchi kuchangia damu.

**Awali, alisema walikuwa wakikusanya kiasi cha damu chupa 750 hadi 800 kwa siku, lakini kwa sasa wanakusanya chupa chini ya 20, jambo ambalo ni hatari.**

# Waandikishaji daftari wapigakura waonywa ulevi

**Na Juster Prudence**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Tunduru mkoani Ruvuma, Gasper Balyomi, amewaonya waandishi wasaidizi wa daftari la kudumu la wapigakura kujiepusha na tabia ya ulevi wakati wote wa uandikishaji.

Aliyasema hayo hivi karibuni wakati akifungua semina ya siku mbili kwa waandishi wasaidizi 200 wa daftari la wapigakura ambao wameteuliwa kuandikisha wananchi kwenye uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika vijiji na kata mbalimbali za Wilaya ya Tunduru.

Kwa mujibu wa Balyomi, uandikishaji unahitaji umakini, uadilifu, kujituma na uaminifu hivyo haitakuwa rahisi mtu mlevi kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Alisema hatosita kumwondoa kituoni mwandishi atakayebainika kunywa pombe saa za kazi na atakayeondoka kituoni bila ruhusa.

Mkurugenzi huyo alisema serikali ina imani na watu waliobahatika kushiriki uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, hivyo uzoefu wao katika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa uandikishaji wa wapigakura na kuwataka kuwasaidia wasiokuwa na uzoefu.

Pia alieleza lengo la kuwapatia mafunzo kuwa ni kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu waliyopewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), ili kuhakikisha kazi hiyo inafanyika vizuri.

Alisema Nec inafanya maboresho katika daftari la kudumu la wapigakura kwa ajili ya kuboresha taarifa mbalimbali za wananchi hususani waliohama kutoka eneo walilojiandikisha mwanzo, kuingiza waliofikisha miaka 18 na kuondoa majina ya marehemu.

Aliwataka waandishi hao kutoa ushirikiano kwa mawakala wa vyama vya siasa ambao watafika katika vituo hivyo na kuwataka mawakala hao kutoingilia kazi za watendaji badala yake wawe waangalizi wa kazi ya uandikishaji.

Naye Mwenyekiti wa Mafunzo, Bartazal Mkwera, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo namna ya kujaza fomu na kutumia mfumo wa alama za vidole BVR, ambayo yatakwenda sambamba na kuanza uandikishaji katika daftari la wapigakura katika tarafa saba za Wilaya ya Tunduru.

Mkwera alisema jumla ya vijana 241 kati ya 255 wameteuliwa kufanya kazi hiyo na kusisitiza kuwa wako tayari kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo la kitaifa.

HABARI KITAIFA

# Watakiwa kutoa elimu fursa utalii

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

MKUU wa Wilaya ya Wete Pemba, Khatib Khamis Mwadini, ameitaka Kamati ya Utalii Mkoa wa Kaskazini Pemba, kuelimisha jamii dhana ya utalii kwa wote, ili waelewe kuwa wanaweza kukuza kipato chao kupitia sekta hiyo kama wanavyonufaika na karafuu.

Alisema sekta ya utalii ni ya pili baada ya zao la karafu katika kukuza kipato cha wananchi, hivyo ni vyema kamati za utalii zikachukua jitihada za makusudi katika kuielimisha jamii, ili wananchi wanufaike nao.

Akifungua mafunzo ya kamati za utalii za Mkoa wa Kaskazini Pemba, yaliyofanyika Wete, alisema iwapo wananchi wataielewa vyema dhana ya utalii kwa wote, watakuza kipato chao na uchumi utaongezeka.

"Tutakapoelimisha jamii tutaisaidia serikali kwani utalii ni usafi wa mazingira na ni usafi wa yote yalituzunguka, kuna vivutio vingi vya utalii, pia kwenye utalii unaweza kujipatia kipato kama unavyojipatia kwenye zao la karafuu, zinahitajika nguvu za pamoja kuelimisha," alieleza.

"Fikra hii imepewa baraka rasmi mwaka 2019, serikali imeona utalii ni sekta muhimu ambayo itaweza kuimarisha uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla, ambapo dhana hii ya utalii kwa wote iliibuliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein," alisema.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Sabah Saleh Ali, alisema lengo la kuundwa kamati hizo ni kwenda kuwafundisha wananchi wa mjini na vijijini na ndipo kukaundwa kamati maalumu ili kusaidia kuelimisha zaidi.

Mkurugenzi wa Idara ya Utalii Zanzibar, Ali Jaku Ali, aliziomba kamati hizo, wadau na wananchi kwa ujumla kushirikiana katika kuhakikisha utalii unaimarishwa nchini.

Mapema, Ofisa Mdhamini Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale Pemba, Khatib Juma Mjaja, alisema ipo haja ya kuviainisha vivutio vya utalii na kuvipangia mikakati ili viimarishwe zaidi.

Akiwasilisha mada katika mafunzo hayo, Salim Hemed Mohamed, alisema kuna fursa mbalimbali katika visiwa vya Zanzibar, ambazo hazijatangazwa, hivyo ni vyema kuimarisha sekta hiyo na kuzitangaza fursa zilizopo ili kukuza uchumi wa nchi.

"Sisi wananchi ni sehemu ya utamaduni, historia, hivyo tutunze historia na utamaduni wetu ili uendelee kwani hivyo ndivyo vinavyoufanya utalii," alisema.

Saleh Malik Abdi, alieleza kuwa umuhimu wa utalii wa ndani ni kukuza uchumi wa nchi, husaidia kutambulisha historia na nyumba za makumbusho, kuongeza maaarifa na ustadi pamoja na utamaduni ambao hujenga haiba ya nchi.

# Kidato cha kwanza chawatega madiwani

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Ragina Chonjo, amewagiza madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza wanaanza masomo yao katika shule walizopangiwa katika kata zote za manispaa hiyo.

Alitahadharisha kuwa ikitokea mwanafunzi yeyote kukosa kuingia kidato cha kwanza, diwani wa kata husika bila kujali ni wa chama gani atachukuliwa hatua kwa kuzembea kutekeleza agizo hilo la serikali.

Chonjo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kilichoambatana na kujadili taarifa ya elimu kwa manispaa hiyo na kufanyika katika ukumbi wa manispaa hiyo.

"Kila diwani wa kata ya Manispaa ya Morogoro hakikisheni wanafunzi hao wanaingia kidato cha kwanza bila kukosa, vinginevyo mtawajibishwa," alisema.

Mbunge wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood, aliitaka Manispaa ya Morogoro kuhakikisha inasimamia walimu na kuwafuatilia kwa karibu ili waweze kufundisha wanafunzi kwa kuwa baadhi ya shule za msingi katika manispaa hiyo amesaidia kuzimaliza changamoto yakiwamo madarasa na madawati.

Diwani wa Sultani, Peter Dhahabu, alisema ipo haja kwa halmashauri hiyo kutenga fedha kwa ajili ya mitihani ya majaribio ya kuwapima watoto hao kabla ya kufanya mitihani ya kitaifa.

"Shule yangu ya Kikundi iliyopo Kata ya Sultani ilikuwa ya mwisho katika matokeo ya mitihani iliyopita, lakini baada ya kukaa na walimu na kuona umuhimu wa mitihani hiyo na nikachangia sasa imefanya vizuri," alisema Dhahabu.

Naye Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Morogoro, Christine Ishengoma, alisema ipo haja kuongeza nguvu pamoja na kuwapa vivutio walimu wanaofundisha shule za pembezoni ili kusaidia kuongeza ufaulu.

"Walimu wa Shule ya Luhungo Manispaa hii wanapita nyumbani kwangu saa nne asubuhi wakitokea shuleni, ina maana hawafundishi ipasavyo," alisema.




Katapila likiliinua lori la mizigo lililokuwa limesheheni mzigo baada ya kuanguka kufuatia kushindwa kupanda mlima kwenye barabara ya mchepuko iliyotengenezwa na mkandarasi anayejenga barabara ya Chunya–Makongolosi Kata ya Matundasi wilayani Chunya Mkoa wa Mbeya. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Uzalishaji chakula Katavi washuka

**Na Neema Hussein, KATAVI**

UZALISHAJI wa mazao ya chakula Mkoa wa Katavi kwa mwaka 2018-2019 umeshuka kutoka tani milioni 1,085,000 zilizozalishwa 2017-2018 hadi tani 865,706.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, wakati akiwasilisha ripoti maalumu ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasung, wakati wa ziara ya kikazi mkoani hapa.

Homera alisema kushuka kwa zao hilo kunatokana na ukosefu wa soko la uhakika na kusuasua kwa zao la mpunga na mahindi, hivyo kupelekea wakulima kukata tamaa mwaka huo.

"Hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2018-2019 umeshuka na hiyo inatokana na kutokuwapo kwa soko la uhakika la mpunga na mahindi hivyo hupelekea wakulima kwa mwaka huo kukata tamaa ya kuzalisha mazao hayo ila 2019-2020 naamini tutakuwa vizuri naona bei kwa sasa imeongezeka," alisema Homera.

Aidha, alisema Mkoa wa Katavi unaendelea kufanya vizuri katika kilimo cha mazao ya biashara ambapo walizalisha tani 7,000 za tumbaku, huku pamba ikiwa ni tani 8,000.

Akijibu changamoto ya kushuka kwa zao la chakula, Hasunga alisema serikali inaendelea kujipanga vizuri kwenye suala la masoko na wizara yake imeanzisha tume ya masoko kwa ajili ya kupata takwimu za masoko yote duniani.

"Niwahakikishie tu serikali imejipanga vizuri katika suala la masoko na tayari wizara yangu imeunda tume kwa ajili ya kitengo cha masoko lengo letu ni kupata takwimu za masoko dunia nzima, hivyo wananchi waendelee kuzalisha mazao kwa wingi," alisema Hasunga.

Baada ya upokeaji wa ripoti hiyo, Hasunga alielekea katika Kata ya Kalema iliyopo katika Wilaya ya Tanganyika kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ya kilimo ukiwamo ukamilishwaji wa skimu ya umwagiliaji, kitalu cha uzalishaji wa mbegu za pamba na uzalishaji wa miche ya korosho.

Aliupongeza Mkoa wa Katavi kwa kushika nafasi ya nne kwa uzalishaji wa mazao kati ya mikoa 26 ya Tanzania, huku akiwataka wananchi waendelee kutumia fursa hii kwa kuwekeza katika kilimo cha matunda na mboga.

# Waondolewa hofu ya soko la zabibu

**Na Ashton Balaigwa, DODOMA**

WAKULIMA wa zabibu nchini wametakiwa kuondoa hofu kuhusu kilimo hicho kukosa soko badala yake waanze kukichangamkia kwa kuwa kwa sasa zao hilo lina uhakika wa soko.

Hali hiyo inatokana na baadhi ya wakulima wakubwa pamoja na wawekezaji kutoka nje kujenga viwanda vya usindikaji na kutengeneza mvinyo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo cha Zabibu Tanzania (Tari Makutupola), Dk. Cornel Massawe, alisema viwanda vya kusindika zabibu na kutengeneza mvinyo vimeshajengwa katika mkoa wa Dodoma na kununua kwa wingi zabibu zinazolimwa katika maeneo yote.

Alisema ujenzi wa viwanda hivyo umetokana na Tari Makutopola kuhamasisha wakulima wakubwa wa zabibu kuungana kujenga viwanda vidogo na vikubwa kwa ajili ya kusindika zao hilo ikiwa ni mkakati wa kuunga mkono mpango wa serikali kuelekea uchumi wa viwanda.

Dk. Massawe ambaye ni mtafiti mkuu wa zao la zabibu nchini, alisema katika kuhakikishia wakulima wa zabibu wanalima zao hilo kwa wingi, wameanza kuzalisha mbegu bora na za kisasa ambazo zina ukindhani na wadudu waharibifu ambao wamekuwa tishio katika miaka ya nyuma kwa zao hilo.

Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano kutoka Tari Makutupora, Vidah Mahava, alisema kwa sasa mkoa wa Dodoma ndio mzalishaji mkubwa wa zabibu, na kwamba wameshaanza kuhamasisha wakulima katika mikoa mingine ya jirani ikiwamo Morogoro, Tabora na Singida kuanza kulima zao hilo.

"Kwa sasa zabibu inalimwa kwa wingi Dodoma hasa katika Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Dodoma (Jiji), lakini kutokana na uwapo wa soko la uhakika, tumeanza kuhamasisha wakulima wengine katika mikoa ya jirani na wameitikia wito wa kulima zao hilo," alisema Mahava.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo wilayani ya Kongwa, Janet Samson, alisema katika wilaya hiyo zao hilo halikuwa linalimwa, lakini baada ya Tari Makutupola kuwapatia elimu kuhusu kilimo cha zao hilo na faida zake, wamehamasika na kuanza kulima kwa kutumia mbegu bora zinazohimili ukame pamoja na ukinzani na wadudu.

**"Kwa sasa zabibu inalimwa kwa wingi Dodoma hasa katika Halmashauri za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Dodoma (Jiji), lakini kutokana na uwapo wa soko la uhakika, tumeanza kuhamasisha...**

# ZEC yafunguka maandalizi uandikishaji wa wapigakura

**Na Suleiman Rashid Omar, PEMBA**

TUME YA Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), imesema maandalizi muhimu kwa ajili ya uandikishaji wapigakura wapya na uhakiki wa daftari la kudumu la wapigakura linalotarajiwa kutumika katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 yamekamilika.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa ZEC, Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mohamoud Hamid, katika mkutano wa wadau wa uchaguzi uliofanyika Chakechake, Pemba.

Alisema ZEC itafanya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura waliomo katika daftari la kudumu kuanzia Januari 18, mwakani na kukamilisha kazi hiyo Machi 4, mwakani na kwamba kazi hiyo itaanzia katika Wilaya ya Micheweni.

Alisema mambo ya msingi ya kuzingatia katika uandikishaji huo ni pamoja na kuwa uandikishaji utazingatia sifa za mpigakura kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi, ambapo pia wapigakura wanaoomba kuandikishwa kwa mara ya kwanza ambao wametimiza umri wa miaka 18 na kuendelea, watatakiwa kufika vituoni kuandikishwa wakiwa na vitambulisho vya Mzanzibar Mkazi.

Alisema miongoni mwa vitu muhimu ambavyo mpigakura mpya huyo atatakiwa aende navyo ni vitambulisho vya Mzanzibar Mkazi vilivyohakikiwa taarifa zao na ambao ni wakazi halali katika maeneo wanayoomba kuandikishwa.

Aidha, wakati wa kazi za kuandikisha wapigakura wapya pia watahakiki wapigakura wakongwe waliomo katika daftari la kudumu la wapigakura, ambao nao watatakiwa kufika vituoni kuhakiki taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura wakiwa na vitambulisho vya Mzanzibar Mkazi vilivyohakikiwa pamoja na vitambulisho vya kupigia kura.

Jaji Hamid aliwataka wadau hao kisiwani Pemba kutoa ushirikiano kwa ZEC ili kuona maandalizi ya uchaguzi mkuu yanafanikiwa na kufanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Faina, alisema ushirikiano kati ya tume hiyo na wadau wa uchaguzi ni muhimu.

Kwa upande wao baadhi ya wadau walisema wamekuwa na wasiwasi mkubwa juu ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkazi ambacho ni sharti muhimu ili katika uandikishaji.

Omar Ali Shehe wa ACT-Wazalendo, alisema angefurahi kusikia kuna ongezeko la Wazanzibar watakaopiga kura katika uchaguzi wa 2020 kutokana na ongezeko la watu, lakini kutokana na ugumu wa kupata vitambulisho hivyo, inawezekana idadi ikapungua.



Meneja wa Bidhaa za Kuwekeza wa Benki ya NBC, Dorothea Mabonye (kushoto) na Meneja Masoko wa benki hiyo, Alina Maria Kimaryo (wa pili kushoto), wakiagana na mmoja wa washindi wa kampeni ya Ibuka Kidedea na NBC Malengo, Ramadhan Saidi (kulia), kabla ya kuondoka katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam jana, akielekea Seychelles pamoja na mwenza wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibaha yaimarisha mifumo ukusanyaji mapato

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani, iko kwenye mkakati wa kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato yake na kubuni vyanzo vipya ili kuwezesha kuchangia mfuko wa maendeleo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Suzana Chaula, wakati akitoa taarifa ya mfuko huo kwa Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, aliyekuwa katika ziara ya siku moja kutembelea vikundi vya wanawake na watu wenye ulemavu.

Suzana alisema wameweka mkakati huo ili kutoa mikopo kwa idadi kubwa zaidi ya vikundi vinavyohitaji vya wajasiriamali kutokana na mwamko mkubwa wa waombaji.

Kaimu Mkurugenzi huyo alimweleza Mgalu kuwa ongezeko la maombi ya mkopo limeongezeka, hivyo kufanya mfuko kushindwa kukidhi mahitaji ya maombi.

"Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha Sh. 373,154,900 kilitengwa kutoka mapato ya ndani ambapo wanawake 149,261,960, na watu wenye ulemavu Sh. 74,630,000, na kwa sasa tuko hatua za mwisho kutoa Sh. 8,000,000 kwa makundi hayo yote," alisema Suzana.

Alisema, mbali ya changamoto ya idadi ya maombi ya mikopo halmashauri, pia baadhi ya wakopaji kutorejesha mikopo kwa wakati na wajasiriamali kukosa maeneo rasmi ya kufanyia shughuli zao pia baadhi ya bidhaa ni kiwango cha chini hivyo kushindwa kuhimili soko.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo, Mgalu ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Pwani, alisema amefanya ziara hiyo ya kibunge kuangalia pia kama sheria mpya ya kutenga fedha kwa ajili ya vikundi inatekelezwa.

Mgalu alisema changamoto zilizoainishwa pamoja na zilizopo kwenye vikundi atazisemea sehemu husika zipatiwe ufumbuzi.



# Wajasiriamali waweka mkakati uzalisha mbegu

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAJASIRIAMALI wa mbegu nchini wameanza mkakati wa kuzalisha mbegu zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na zinazohimili ukame, ili kumsaidia mkulima kupata mazao mengi ya chakula na biashara.

Akizungumza jana katika maonyesho ya teknolojia ya kilimo yaliyofanyika kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tari Seliani, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Seedco, Daniel Ulimboka, alisema kwa sasa wamefanya utafiti na kuja na mbegu bora ambazo zinahimili hali ya ukame na zinaleta mavuno ya kutosha.

Alisema kwa mwaka huu, mvua inanyesha kwa kiwango kikubwa, lakini kuna miaka mvua inakuwa kidogo, hivyo mbegu hizo zitawasaidia wakulima kupambana na ukame utakaojitokeza.

"Tuna mbegu aina ya Tumbili 419 ambayo inafanya vizuri sana hasa katika kipindi ambacho hakuna mvua za kutosha, licha ya kuwapo kwa uhaba wa mvua, bado wakulima wanafurahia kilimo," alitamba.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Melchiory Temu, aliwataka watafiti kubuni teknolojia zinazoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi, ili wakulima wapate mazao mengi.

"Mabadiliko ya tabianchi yanaleta athari na kusababisha kushuka kwa uzalishaji, jambo linalokatisha tamaa wakulima kuendelea kulima," alisema.

Aliwataka wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea ili walime kilimo chenye tija na kuwaletea manufaa kiuchumi.

Mkurugenzi wa Baraza la Nafaka Afrika Mashariki, Gerald Masila, alisema wanafanya juhudi za kuwaunganisha wakulima na masoko, ili wapate faida ya kilimo na kujikwamua kiuchumi.

"Tunafahamu juhudi zitazaa matunda, kwani wakulima wamepata masoko na sasa watakuwa na uhakika wa kujiinua kiuchumi," alisema.

**"Tuna mbegu aina ya Tumbili 419 ambayo inafanya vizuri sana hasa katika kipindi ambacho hakuna mvua za kutosha, licha ya kuwapo kwa uhaba wa mvua, bado wakulima wanafurahia kilimo," alitamba.**

# DC Muro aja na mkakati wa kuboresha utendaji hospitali

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amemwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru wilayani humo, Dk. Maneno Focus, kufanya ziara za kushtukiza katika hospitali zilizoko wilayani humo ili kubaini wauguzi wanaolala na wanaotegea zamu za usiku na kuwachukulia hatua.

Pia, amemtaka mganga mkuu huyo kuwapatia semina wauguzi katika hospitali zilizoko wilayani humo, kutumia lugha ya unyenyekevu kwa wagonjwa na kuwapatia faraja kama saikolojia ya utabibu inavyotaka.

Akizungumza jana na wananchi wilayani humo kwenye mkutano wa hadhara, Muro alidai kuna tatizo la baadhi ya wauguzi wanaoingia usiku, kutotekeleza majukumu yao, akibainisha kuwa katika ziara zake za nyakati za usiku kwenye hospitali, amebaini wengi wao wanalala.

"Kwa mfano, siku moja nilitembelea Hospitali ya Tengeru na zingine, usiku nikajifanya ni mgonjwa, nikakuta madaktari wamelala, mlinzi akaniambia nikakae eneo fulani nitatibiwa asubuhi, ndipo nikampigia simu daktari mmoja ambaye alikuja na yeye akajionea mwenyewe," alidai.

Muro alisema anaamini ziara za mara kwa mara za kushtukiza, zitawafanya wauguzi kuwa makini na kazi yao na watawahudumia wagonjwa kwa muda wote wa saa 24 kama inavyotakiwa na walivyoelekezwa.

Kiongozi huyo wa wilaya pia alimwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru, kupeleka wauguzi katika zahanati za vijiji vya Songoro na Maruvano, baada ya ukarabati na ujenzi wa majengo yake kukamilika.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Meru, Dk. Focus, alisema ofisi yake imejipanga kuwahudumia vyema wananchi wa Meru na wafanyakazi wazembe watadhibitiwa katika uongozi wake.

Alisema chini ya uongozi wake, wamejitahidi kuboresha huduma katika Hospitali ya Wilaya ya Meru kwa kuongeza vifaa tiba, huku vituo vya afya na zahanati zikiendelea kujengwa kwa kasi ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

"Katika hospitali, zahanati na vituo vya afya tumeboresha huduma zetu kwa hali ya juu na vifaa hususani vya mama na mtoto vinapatikana kwa zaidi ya asilimia 98, tunataka mama akifika kujifungua, kusitokee kabisa kifo cha mtoto au mama," alitamba.



Ofisa Muuguzi katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma, Hadija Ikaji, akimhudumia mmoja wa majeruhi wa ajali ya daladala, Shukuru Stephin, aliyelazwa katika wodi hiyo, kutokana na ajali iliyohusisha daladala linalofanya safari zake kati ya mjini na Nzuguni na fuso iliyotokea juzi, usiku jijini Dodoma na kusababisha vifo vya watu 6 na majeruhi 12. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ahimiza kuenzi mila, desturi

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

OFISA Utamaduni wa Mkoa wa Arusha, Irene Ngao, amewataka Watanzania kuendelea kuthamini na kuzienzi mila, desturi na utamaduni uliopo katika jamii ili kuendelea kuzirithisha kwa vizazi na vizazi.

Ngao alito wito huo, juzi, alipozungumza na wananchi wenye asili ya Karagwe na Kyelwa, Mkoa wa Kagera waishio Arusha, waliounda umoja wao wa kusaidiana.

Alisema serikali inatambua uwapo wa mila na desturi mbalimbali zilizopo katika jamii, hivyo inategemea zirithishwe zaidi kwa vizazi vilivyopo na vinavyokuja ili utaratibu huo usisahaulike katika jamii.

"Nasisitiza kila kabila liendelee kuenzi utamaduni na mila zao na tuhakikishe zinatuunganisha badala ya kutugombanisha, kwani serikali nayo kwa upande wake inaendelea kufundisha somo la utamaduni shuleni, ili watoto wetu wazitambue mila na desturi zilizopo," alisema.

Mwenyekiti wa umoja huo, Wilibald Ngambeki, alisema wamekuwa na utamaduni wa kukutana kila mwaka, ambapo hiyo ni mara ya 23 kukutana tangu waanzishe umoja huo mkoani hapa.

Alisema lengo la kufanya tamasha hilo ni kuhakikisha watoto wanaozaliwa mjini, wanazijua mila na desturi zao na kuzienzi ili zisipotee.

Ngambeki alisema kila mwaka wanakutana na kuonyesha utamaduni unazofanywa na jamii yao na kuwapa fursa watoto wao kujionea masuala mbalimbali na kujifunza.

"Utamaduni ni kitu muhimu sana, kwani unasaidia kupunguza makali ya utandawazi, hivyo jamii kuendelea kujikita katika utamaduni wake na kuacha kuiga mambo ya utandawazi. Nashauri kila kabila liendelee kuenzi utamaduni wake ili usipotee," alishauri.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya tamasha hilo, Barungo Augustino, alisema wamekuwa wakikutana kwa lengo la kutunza mila, desturi na utamaduni wao.

Aliyataka makabila mengine kuendelea kuenzi utamaduni kwa kukutana mara kwa mara, akiamini kwamba bila kufanya hivyo, utamaduni utaendelea kupotea na itabaki historia tu.





## TGNP yanoa watendaji wa vijijini utawala bora

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MTANDAO wa Kijinsia Tanzania (TGNP Mtandao), umekamilisha kazi ya kuwanoa viongozi wapya wa vijiji na wajumbe wa serikali za vijiji vya Maua na Uchau Kusini, Moshi Vijijini kuhusu dhana ya utawala bora.

Kwa mujibu wa Ofisa Mwandamizi wa TGNP, Deogratius Koyanga, viongozi hao walijengewa uwezo kwa siku kadhaa ili waendeshe vijiji vyao vizuri na kitaalamu kwa kuzingatia sheria na taratibu.

"Tulipokuja kijijini kwa ajili ya mapumziko ya sikukuu za mwisho wa mwaka, wadau wa maendeleo kutoka mashirika ya kiraia tulijitolea kuwanoa viongozi wapya wa vijiji ili waweze kuendesha vijiji vyetu vizuri na kitaalamu wakijua sheria na taratibu.

"Kuna suala zima la uibuaji wa miradi ya maendeleo na namna ya kuisimamia iwe endelevu na pia nimepata nafasi ya kusisitiza juu ya ulinzi wa mtoto wa kike asipate mimba, kwa sababu inamweka katika nafasi ya kukatisha masomo yake," alisema.

Kuhusu mafunzo hayo, Koyanga alisema wamefarijika kama wadau kuwajengea uwezo viongozi hao juu ya utawala bora na haki za binadamu.

Alisema miongoni mwa mambo waliyojifunza ni pamoja na maana ya utawala bora, faida za utawala bora, athari za kukosa utawala bora, misingi ya utawala bora, nguzo za utawala bora, haki za binadamu, misingi ya haki za binadamu, vyanzo vya haki za binadamu, uhusiano kati ya haki za binadamu na utawala bora na misingi ya utoaji wa haki.

"Naamini kwamba mafunzo hayo yatawasaidia katika kujenga jamii ambayo misingi ya utawala bora na haki za binadamu inakuzwa, inalindwa, inazingatiwa, inatekelezwa na kuhifadhiwa," alisema.

Alisema mbali na hayo, viongozi hao wa vijijini wamepewa mafunzo juu ya ushiriki wa wanawake katika uongozi ikiwamo siasa.

# Wajumbe 271 kuamua bosi mpya UVCCM Siha

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

MCHAKATO wa kumsaka atakayerithi kiti cha Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Wilson Mushi, ulitarajiwa kuhitimishwa rasmi jana, baada ya majina ya wagombea watatu kupelekwa kwa wajumbe wa mkutano mkuu maalum kupigiwa kura.

Jana, Katibu wa UVCCM wilayani humo, Bulugu Magege, aliiambia Nipashe kuwa uchaguzi huo mdogo wa marudio unatarajiwa kufanyika jana katika mji mdogo wa Sanya Juu ambako wajumbe wa mkutano mkuu 271 walitarajiwa kuamua nani anafaa kuwaongoza kwa kipindi kilichobakia.

"Ni kweli tuna uchaguzi wa mwenyekiti wa wilaya, tunajaza nafasi ya Mushi ambaye aliajiriwa serikalini kuwa Ofisa Mtendaji wa Kata. Tayari wagombea wamepatikana na leo (jana) wanapigiwa kura kumtafuta mwenyekiti mpya," alisema.

Aliwataja waliokuwa wanawania kiti hicho kuwa ni John Barakael Mushi, Gema Michael Mtui na Yohana Lengere.

Kabla ya kuelekea katika uchaguzi huo, Magege alionya kuwa uchaguzi huo ni kama mchezo wa kirafiki, kwa kuwa wote ni wana CCM na hakuna sababu ya kuwapo na hila, fitina, wala kuvunjana miguu kwa wagombea na wafuasi wao wanaowaunga mkono.

Kwa mujibu wa Magege, wajumbe wa mkutano mkuu maalum jana walikutana kwa ajili ya ajenda moja ya uchaguzi wa kujaza nafasi ya Mwenyekiti UVCCM wa Wilaya ya Siha.

Kumekuwapo usiri mkubwa tangu siku ya mwanzo ya kutoa fomu hadi siku ya uchaguzi huo kufanyika kama hakukuwa na mchakato huo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akizungumzia uchaguzi huo alisema: "Suala la uchaguzi ndani ya chama na hasa UVCCM, wajumbe wa mkutano mkuu maalum wanapaswa kutambua dhamana waliyopewa ni kubwa, hivyo ni jukumu lao kuhakikisha wanawachagua viongozi bora watakaowatumikia.

"Wasichague tu kiongozi kwa kuangalia dini, kabila wala rushwa na badala yake, wawachague viongozi wenye moyo wa dhati wa kukitumikia chama na kukiletea maendeleo."



Mkuu wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro (mwenye fulana nyeusi), akiwa na Balozi wa Utalii wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Nancy Sumari (mwenye nguo ya kaki), wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha utalii wa ndani katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mtandao wasanii wajitosa kusaidia wanaoishi na VVU

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

WATOTO 100 wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) katika Wilaya ya Siha, sasa wanao uhakika wa kuzifikia huduma bora za afya katika maeneo yao, baada ya Mtandao wa Wasanii wa Muziki wa Injili nchini (Tagoane), kuonyesha upendo wao kwa kuwaunganisha na huduma hiyo.

Akiwa katika Wilaya ya Siha, Rais wa Tanzania Gospel Artists Network, Dk. Godwin Maimu, alisema waliona hawawezi kuendelea kuwaacha watoto wanaosumbuliwa na maambukizo ya virusi hivyo kutaabika kutokana na maradhi mbalimbali ambayo gharama zake za tiba ni kubwa.

Dk. Maimu alitoa taarifa yake jana kuhusu sadaka yao kwa vijana hao, wakati wa kongamano la upendo lililofanyika katika Usharika wa Nasai wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Kongamano hilo liliyakutanisha makundi maalumu ya yatima, watu wenye ulemavu, wajane, wazee na wale wanaoishi na VVU.

"Hatuwezi kuwaacha watoto wanaosumbuliwa na maambukizo ya VVU kuendelea kutaabika kutokana na maradhi mbalimbali ambayo gharama zake za tiba ni kubwa.

"Wengi huathirika zaidi kutokana na kushindwa kumudu gharama za tiba, hivyo Tagoane tumeona, tuwakatie bima za afya watoto hawa 100 ili watibiwe mahali popote," alisema.

Dk. Maimu alisema watoto yatima waliofaulu kuingia kidato cha kwanza mwaka 2020, pia watanunuliwa na Tagoane sare za shule, madaftari, kalamu na vifaa vingine vyote vinavyohitajika kwa ajili ya taaluma.

Katika hatua nyingine, Dk. Maimu alisema Tagoane inatarajia kujenga shule maalum kwa ajili ya watoto yatima na wale wanaoishi na VVU katika Wilaya ya Siha, ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua watoto wote nchi nzima.

"Lengo la kujengwa kwa shule hiyo maalum ni ili watoto hao waweze kutimiza ndoto zao, huku wakijengwa kisaikolojia kutokana na ukweli kuwa wapo watoto wenye ulemavu na wenye uwezo mzuri wa kielimu, pamoja na ndoto zao za kujiendeleza, lakini wanashindwa kutokana na matatizo waliyonayo," alisema.

Akizungumza katika kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, aliipongeza Tagoane kwa kuwasaidia watoto 100 wanaoishi na VVU kwa kuwakatia bima ya afya, kwa kuwa watakuwa na uhakikisha wa matibabu muda wote.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Siha, Marko Masue, aliitaka jamii kutokuwaficha watoto wenye ulemavu ndani, badala yake wawatoe ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa ikiwamo ya elimu na matibabu.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kuna watoto yatima zaidi ya 1,000 na watu wenye ulemavu 355 katika Wilaya ya Siha, lakini bado kuna tatizo la jamii inaonekana kuwatenga. Ni matumaini yangu kupitia kongamano hili litawaibua ili waweze kupata huduma hizo muhimu," alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 31, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 19

## Kilwa inavyowekeza kwa watu kuishi kirafiki na mazingira



Ukurasa 18

## Mji wa Syria una paka wengi kuliko watu



Ukurasa 14

## Sababu zinazochangia meno ya watoto kutoboka, kuoza



### MIMBA SHULENI

# Shinyanga yalia na wazazi wanaomaliza kimyakimya

Ukurasa 16

ELIMU KUTOKA POLISI

# Fahamu namna ya kuzuia maafa

MAAFA ni matokeo ya majanga au janga ambalo husababisha vifo, upotevu wa mali au mazingira ambapo jamii iliyoathirika haiwezi kukabili kwa uwezo na raslimali zake bila ya msaada kutoka nje ya jamii hiyo.

Janga au majanga ni balaa au baa linaloweza kusababisha maafa.

Ili maafa yatokee ni lazima liwepo janga na vitu vinavyoweza kuathiriwa na janga hilo mfano watu, miundombinu au mazingira.

**SABABU ZA KUATHIRIWA NA JANGA AU MAJANGA**

Kuwa karibu na eneo la janga, mabadiliko ya hali ya hewa na Uharibifu wa mazingira ni baadhi ya sababu.

Aidha, umaskini, kutokujua au kufahamu, matatizo ya kijamii na kisiasa.

**AINA ZA MAAFA**

Kwanza ni maafa yanayosababishwa na nguvu za kiasili bila au pakiwa na visababishi vidogo kutoka kwa binadamu mara nyingi hutokana na jiolojia, haidrolojia au mabadiliko ya hali ya hewa.

Mfano ya aina hii ya maafa ni ukame, tetemeko la ardhi, kimbunga, mafuriko, milipuko, radi na magonjwa ya milipuko.

Kuna maafa yanayosababishwa na vitendo vya kibinadamu kwa bahati mbaya, makusudi au uzembe.

Mifano ya aina hii ya maafa ni pamoja na ajali ya vyombo vya usafiri au viwandani, moto, wakimbizi, migongano ya kijamii/vita.

Vilevile kuna aina ya makundi ya maafa ambayo hutokea kwa kasi yaani ghafla na yale yanayotokea polepole.

**MAAFA YANAYOTOKEA GHAFLA**

Ni moja ya makundi ya aina ya maafa yanayotokea kwa ghafla bila ya kutegemewa mfano tetemeko la ardhi, ajali, moto pamoja na milipuko ya kemikali.

Katika aina hii ya maafa huwa mara nyingi hakuna muda wa kutosha wa kutoa onyo kwa wananchi.

**MAAFA YANAYOTOKEA POLEPOLE**

Hii ni aina nyingine ya makundi ya maafa ambayo huwa na tabia ya kujengeka polepole ndani ya jamii.

Baadhi ya mifano ya aina hii ya maafa ni pamoja na ukame, migongano ya kijamii na vita.

Katika aina hii ya maafa, huwa kuna muda wa kutosha wa kutoa onyo au tahadhari na jamii inaweza kujiandaa kukabiliana nayo.

**NAMNA YA KUZUIA MAAFA**

Ni hatua zinazochukuliwa (Kabla ya maafa) kwa kusudi la kuzuia maafa yasitokee kabisa au kupunguza madhara yake.

Maafa yanaweza kuzuilika au kupunguza madhara yake ndani ya jamii kwa kuzingatia tahadhari zinazotolewa mara kwa mara na mamlaka husika, kuhama kutoka kwenye maeneo yasiyofaa kwa maisha ya kibinadamu.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa kukabiliana na maafa wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Nasser Mwakamboja, jamii haiwezi kuzuia maafa yote, lakini baadhi ya maafa yanaweza kuzuiliwa.

Aidha, kwa yale ambayo hayawezi kuzuiwa, madhara yake yanaweza kupunguzwa kwa kutekeleza baadhi ya mipango mahsusi inayotakiwa kufanyika kabla, wakati na baada ya maafa kutokea.

"Uelewa mdogo wa namna ya kukabiliana na maafa ni miongoni mwa changamoto za kuzuia na kupunguza madhara ya maafa pindi yanapojitokeza." Anasema ACP Mwakamboja.

Kuzuia ni hatua muhimu na imedhihirisha kuwa ni gharama nafuu kuliko ile ya kukabili maafa.

***Imetolewa na;***
***Kitengo cha Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***
***S.L.P 9141***
***Dar es Salaam***
***Baruapepe habariphq@yahoo.com, habari.phq@tpf.go.tz***




Moja ya maafa yanayosababishwa na vimbunga. **PICHA: MTANDAO**

JIELIMISHE

## Sababu zinazochangia meno ya watoto kutoboka, kuoza



AFYA ya kinywa ni muhimu hata kwa mtoto mchanga ambaye hana meno kinywani mwake.

Ingawa meno ya mtoto mchanga huanza kuonekana miezi sita baada ya kuzaliwa, mzazi anashauriwa kuanza kusafisha kinywa chake siku chache baada ya kuzaliwa kwa kufuta fizi zake kwa kitambaa kisafi.

Mpaka meno ya mtoto mchanga yaanze kuonekana yanaweza kupata maambukizi endapo kinywa kitakuwa hakitunzwi vyema.

Wakati yakiota, yanaweza yakaanza kutoboka hivyo ni vizuri kuanza usafi wa kinywa na meno.

Kuanza kutunza meno ya mtoto tangu anapokuwa mchanga huweza kumkinga na kutoboka kwa meno na magonjwa mengine ya kinywa kwa miaka mingi ijayo. Pindi mtoto anapozaliwa, taya zake zimeshabeba meno yote 20 ya utotoni.

Anza kusafisha kinywa cha mtoto wako siku chache baada ya kuzaliwa kwa kufuta fizi zake kwa kitambaa kisafi. Meno ya mbele ya utotoni huweza kujitokeza miezi sita baada ya kuzaliwa ingawa baadhi ya watoto kuchelewa kuota meno mpaka miezi 12 au 14.

Mpaka ujiridhishe kuwa mwanao anaweza kupiga mswaki mwenyewe, endelea kumsaidia kupiga mswaki mara mbili kwa siku kwa kutumia mswaki wa watoto pamoja na dawa ya meno yenye madini ya floridi.

Kwa mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitatu, wazazi ama walezi wanatakiwa waanze kumpigisha mswaki mara tu meno yanapoanza kutokeza kinywani.

Mswaki huo unatakiwa uwe mdogo na dawa ya meno yenye madini ya floridi ukubwa wa punje ya mchele.

Upigaji wa mswaki unapaswa kufanywa kwa umakini asubuhi baada ya kifungua kinywa na usiku kabla ya kulala. Mzazi anatakiwa ahakikishe mtoto hamezi dawa ya meno inayotumika wakati wa kusafisha kinywa na meno, mtoto aiteme yote na kusukutua kwa maji safi.

Kwa watoto wa umri wa kati ya miaka mitatu mpaka sita, wakati wa kupiga mswaki, mzazi anatakiwa ahakikishe dawa ya meno inayotumika ina madini ya floridi na ukubwa wa punje ya harage.

Kwa kawaida, meno ya utotoni yanapoanza kujitokeza miezi sita mpaka mwaka mmoja baada ya kuzaliwa, baadhi ya watoto huvimba na kuhisi maumivu kwenye fizi.

Inashauriwa, hali hii inapotokea, pitisha taratibu kidole ama kitambaa kisafi ili kutuliza hali hiyo. Watoto wengi wafikapo umri wa miaka mitatu, huwa na meno yote 20 ya utotoni.



ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Jamii ikabili tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa



Baadhi ya wanajamii wakiwa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa, ili wanafunzi waliofaulu wasikose nafasi. **PICHA: MTANDAO**

TANGU Januari mwaka 2016, Watanzania walianza kufurahia matunda ya elimu bure inayoendelea kutolewa katika shule za msingi hadi kidato cha nne.

Hiyo ni baada ya serikali kuamua kuondoa ada, ili kuwapunguzia wazazi mzigo.

Hatua hiyo ya kutoa elimu bure inakwenda sambamba na uandikishaji wa watoto wengi wanaoanza elimu ya msingi kila mwaka, na huenda miaka ijayo kukawa na wanafunzi wengi zaidi wanaoingia sekondari.

Wanafunzi walionza darasa la kwanza wakati elimu inaanza kutolewa bure mwaka 2016, ndio ambao mwaka 2022 watakuwa wanahitimu elimu ya msingi, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa wengi wao kwenda sekondari.

Kwa maana hiyo ni vyema maandalizi kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa yakaanza sasa badala ya kusubiri wafaulu ndipo harakati ya ujenzi zianze.

Kimsingi, tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa limeendelea kuwapo kila mwaka hali ambayo inasababisha baadhi ya wanafunzi waliofaulu darasa saba kukwama kuanza masomo kwa wakati.

Ikumbukwe kuwa wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi mwaka 2018 na kufaulu kwenda sekondari mwaka huu, baadhi yao walikumbana na tatizo hilo la shule kuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa.

Hali hiyo ilisababisha baadhi ya shule za sekondari kulazimika kuwapanga wanafunzi kwa zamu, lengo likiwa ni kuhakikisha wanapata elimu wakati jitihada za kujenga vyumba vipya vya madarasa zikiendelea. Bado baadhi ya wanafunzi wanaojiandaa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2020, wamekumbana na tatizo la uhaba wa madarasa, hali ambayo inalazimu zifanyike jitihada za makusudi, kuhakikisha wanaanza masomo kwa wakati.

Hii inatokana na kile kilichowahi kusemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, kwamba kuna uhaba wa madarasa kwenye baadhi ya shule za sekondari nchini.

Akizungumzia matokeo ya darasa la saba ya 2019 mwanzoni mwa mwezi huu, Jafo alielezea kwa kina tatizo hilo kwamba wapo baadhi ya wanafunzi waliofaulu, lakini hawakupata nafasi kutokana na uhaba wa madarasa.

Anasema, jumla ya wanafunzi 58,699 sawa na asilimia 7.73 wakiwamo wavulana 28,567, sawa na asilimia 48.53 na wasichana 30,132, sawa na asilimia 51.33 ya waliofaulu mwaka 2019, hawakupata nafasi ya kuchaguliwa kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa.

> Wakuu wa Mikoa hakikisheni vyumba vya madarasa vinakamilika ili wanafunzi wote waliofaulu waanze masomo kwa pamoja.

Jafo anaitaja mikoa yenye uhaba wa vyumba vya madarasa na idadi ya wanafunzi kwenye mabano kuwa ni Arusha (4,739), Dar es Salaam (5,808), Iringa (3,480), Kigoma (12,092) na Lindi (1,695).

Kwa mujibu wa Jafo, mikoa mingine yenye uhaba wa vyumba vya madarasa ni Manyara (728), Mara (9,493), Mbeya (2,716), Pwani (2,918), Rukwa (686), Simiyu (6,616), Songwe (4,684) na Tanga (3,044).

### WALIOFAULU

Anasema, wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 kuwa ni 701,038, ambao ni sawa na asilimia 92.27 ya wanafunzi 759,000 waliofaulu.

Kwamba mwaka 2019 jumla ya wanafunzi 759,737 walifaulu, sawa na asilimia 81.3 ya waliofanya mtihani, wakiwamo wavulana 363,999, sawa na asilimia 47.9 na wasichana 395,738, sawa na asilimia 52.08.

Akifafanua zaidi, Waziri Jafo anasema, kati ya waliofaulu, wamo wanafunzi wenye ulemavu 1,461 sawa na asilimia 0.19 wakiwamo wavulana 777 na wasichana 684.

"Kati ya wanafunzi waliochaguliwa, 3,145 sawa na asilimia 0.41 ya waliofaulu, wamechaguliwa kujiunga na shule za bweni, 970 watajiunga na shule za vipaji maalum wenye ufaulu mzuri zaidi, 1095 watajiunga na shule za ufundi na 1,080 watajiunga na shule za bweni kawaida," anasema Jafo.

Jafo anasema, wanafunzi 697,893 sawa na asilimia 99.59, wakiwamo wavulana 361,866 na wasichana 395,692 wamechaguliwa kujiunga na shule za sekondari za kutwa katika kata mbalimbali nchini.

### MAAGIZO

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amewaagiza wakuu wa mikoa nchini kuhakikisha wanasimamia ipasavyo ujenzi wa vyumba vya madarasa vikamilike kwa wakati, ili wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 waanze masomo kwa pamoja.

Anasema lengo la serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaanza kusoma kwa pamoja, kwa sababu wakipishana muda wa kuanza masomo, baadhi yao wanashindwa kufanya vizuri, jambo ambalo si sahihi.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo Desemba 29, 2019, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2015/2020, kwenye mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi.

"Wakuu wa Mikoa hakikisheni vyumba vya madarasa vinakamilika ili wanafunzi wote waliofaulu waanze masomo kwa pamoja. Kitendo cha wanafunzi kupishana kuanza masomo kinawafanya waliochelewa kutofanya vizuri katika mitihani yao," Waziri Mkuu anasema.

Aidha, anawataka viongozi hao wahakikishe wanasimamia vizuri elimu kwa watoto wa kike na kuwachukulia hatua watu wote watakaobainika kuwakatisha masomo iwe kwa kuwaoa, kuwaozesha au kuwapa ujauzito.

Waziri Mkuu anasema, serikali imeweka sheria kali ya kumlinda mtoto wa kike ili kumuwezesha kuhitimu masomo yake aweze kujikwamua kiuchumi na aondokane na utegemezi, hivyo ni marufuku kuwakatisha masomo.

Kwamba, serikali inataka kuona idadi kubwa ya watoto wa kike wanatimiza malengo yao kielimu, hivyo ni lazima wakaondolewa vishawishi kwa kuboresha mazingira yao ya kujifunzia ikiwamo kuongeza idadi ya mabweni.

### JAMII VIPI?

Wazazi na jamii kwa ujumla wanahusika katika maendeleo ya shule kupitia bodi za shule, ili kuhakikisha wanapunguza matatizo yakiwamo ya uhaba wa madarasa, badala ya kuiachia serikali kana kwamba hawahusiki.

Kwa wale wanaotambua hilo, hawasubiri kusukumwa au kuvizia serikali ifanye kazi hiyo, badala yake wanaitana na kuweka mikakati ya kufanikisha maendeleo ya shule hizo, kwa kutambua kuwa ni za umma.

Mfano mmojawapo ni huu wa wakazi wa Musoma Vijijini mkoani Mara, ambao sasa wanaendelea na mikakati ya kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ili wanafunzi wote waliofaulu waanze masomo.

Januari 3, 2020 wakazi wa Kata ya Bulinga watakuwa na harambee ya kuchangia ujenzi wa madarasa matatu ya sekondari yao kisha Januari 6 kutakuwa na harambee nyingine, katika Shula ya Sekondari ya Kata ya Rusoli.

Shule ya Sekondari Rusoli ina uhaba wa chumba kimoja cha darasa, na harambee hiyo itaendeshwa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo, akishirikiana na wadau wengine wa elimu.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Musoma, Majid Kalugendo, anasema kuna uhaba wa vyumba 13, na sasa juhudi zinafanyika, kuhakikisha vyumba vinajengwa ili wanafunzi wote waliofaulu wanaanza masomo.

ELIMU

**NA MARCO MADUHU, SHINYANGA**

MIMBA SHULENI

# Shinyanga yalia na wazazi wanaomaliza kimyakimya

• Kitaifa, dawa yao iko jikoni




Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari Shinyanga Mjini, wakiwa wamebeba mabango kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

MILA na desturi zilizopitwa na wakati zimeendelea kuwa tatizo mkoani hapa, wakazi wakiathiriwa sana na tatizo la mila potofu ya kutopenda kusomesha shule watoto mabinti.

Ni mwenendo unaoendana kuozesha ndoa za utotoni na kuwakatisha masomo mabinti, wazazi wao wakilenga kunufaika kwa mifugo.

Kutokana na kuendekeza mila hizo, kunachangia idadi kubwa ya wanafunzi wa kike kukatishwa masomo kwa kupewa ujauzito wa makusudi, ili wafukuzwe masomoni kuishia katika kufanyika ndoa ya utotoni.

Takwimu za kitaifa za mwaka 2012, zinaonyesha hadi wakati huo Shinyanga inaongoza kitaifa kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni, ikifuatiwa na mikoa ya Tabora na Mara.

Aidha, katika mimba za wanafunzi zilizotolewa hizi karibuni kwenye kikao cha kutangaza matokeo ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato kwanza mwakani, hadi mwaka jana 2018 wapo wanafunzi 69 wa mkoani Shinyanga kuwa walipewa ujauzito na kuacha masomo, 60 waliokuwa sekondari na tisa, elimu ya msingi.

Hivi, tangu Januari hadi mwezi uliopita, takwimu zinaainisha, kuna wanafunzi zaidi ya 138 waliokwishapewa ujauzito na wameacha masomo. Hapo, kuna 117 wa sekondari na 21 shule za msingi.

Takwimu zilitolewa na halmashauri nne, kati ya sita zilizopo mkoani Shinyanga, zinaodokeza idadi ya mimba na halmashauri husika katika mabano: Kahama Mji (40), Kishapu (38), Ushetu (42), Shinyanga Vijijini 18.

### WAZAZI LAWAMANI

Kushamiri kwa mimba hizo za wanafunzi, wazazi ndio wanaonyooshewa vidole kuwa chanzo kikubwa cha mimba za mabinti shuleni, katika mtazamo wa kuendekeza mila na wakati, ni wazazi kuozesha watoto wao kabla ya kumaliza shule kwa sababu ya tamaa ya mahari.

Ni matukio yanayotajwa kukumbatia tabia ya kumaliza kesi hizo kimya kimya, hali inayosababisha watuhumiwa wasiingie katika mikono ya sheria na hata kuwaadhibu.

Tayari kuna lawama ya kukuzwa tabia inayoelezwa wazazi wanamaliza kesi hizo kimya kimya, watuhumiwa ambao ni chanzo cha mimba hizo za wanafunzi, kuligeuza kwamba ni kitu cha kawaida, hata wapo wanaothubutu kuyabainisha tena mimba za aina hiyo kwa wanafunzi wengine.

> Ili tatizo la mimba hizi za wanafunzi zipate kukoma mkoani Shinyanga, ni lazima wasimamizi wa sheria watekeleze majukumu yao ipasavyo.

### KUTOKA POLISI

Victoria Maro ni Ofisa wa Polisi kutoka Kitengo cha Dawati la Jinsia mkoani Shinyanga, ana ufafanuzi wa takwimu za matukio ya ukatili waliofanyiwa mabinti.

Hapo anataka kujumuisha matukio yanayohusu ulawiti, ubakaji, mimba na ndoa za utotoni kwa mabinti, akirejea mwaka jana pekee kulikuwapo na matukio 473, lakini kesi zilizofungwa kutokana na kukosa mwendelezo jumla yake ni 33.

Ameendelea kutaja kesi zilizokwisha tajwa mahakamani 107 na zingine 168, ambazo bado zipo kwenye hatua ya upelelezi.

Vivyo hivyo, inafafanuliwa kwamba kuna idadi ya watuhumiwa 143 na kuna wazazi 22 waliomalizana kesi zao kimyakimya.

Msimamizi huyo wa mashauri na ya mashtaka ya kujijnsia ndani ya Polisi, kwamba takwimu za ukatili dhidi ya watoto mwaka huu (2019) kwamba kuna matukio 70, kesi zilizofungwa kutokana na kukosa mwendelezo 70, zilizotajwa mahakamani 133, zilizoisha 76, ambazo zipo kwenye upelelezi 191, na kubainisha changamoto iliyopo ni kukosekana ushahidi.

"Tatizo kubwa ambalo tuna kabiliana nalo sisi Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na maofisa ustawi wa jamii, dhidi ya kuendesha kesi hizi za ukatili dhidi ya watoto zikiwamo mimba za wanafunzi ni kukosekana kwa ushahidi. Keshi nyingi huishia njiani, baada ya upande wa mashtaka kumalizana na mshitakiwa," anasema Maro.

"Takwimu za matukio haya ya ukatili dhidi ya watoto ambazo nimezitoa juu ya kesi zilizokosa mwendelezo na watuhumiwa kuachiwa huru, zimetokana na kukosekana kwa ushahidi, baada ya wazazi kumalizana na watuhumiwa, wakaacha kutoa ushirikiano na kutohudhuria mahakamani, hivyo kesi inafutwa," anaongeza.

### MKAKATI KITAIFA

Tedson Ngwale ni Katibu wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa serikali kupunguza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga, (MTAKUWWA), anasema kutokana na wazazi kumaliza kesi hizo kimya kimya, imesababisha Shinyanga kuongoza kwa mimba za wanafunzi kitaifa.

Anasema tatizo hilo la kumaliza kesi kimya kimya linaiumiza sana taifa, hasa ikizingatiwa serikali inapigana kutafuta mbinu za kutokomeza mimba hizo za wanafunzi.

Ngalwe anasema, walitarajia kukomesha kasi hiyo kwa watuhumiwa kufungwa kwa mtazamo itawaogopesha wanaume kuwafuata mabinti kimapenzi, lakini wazazi nao wamekuwa kikwazo kwa mkakati huo chanya.



Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga, Nyabaganga Taraba.

"Takwimu za mimba za wanafunzi mkoani Shinyanga kwa mwaka wa fedha, kati ya Julai 2018 hadi Juni 2019 kuna jumla ya wanafunzi 168 walipewa ujauzito.

"Mgawanyo ulikuwa, wanafunzi wa sekondari 167 na mimba saba kutoka elimu ya msingi, ndani ya mwaka huo huo wa fedha, ndoa za utotoni zipo 32 na kitaifa mkoa unaongoza kwa mimba na ndoa za utotoni asilimia 59.

"Hivi sasa serikali tunaandaa mpango mkakati wa kuwabana wazazi ambao wamekuwa wakimaliza kesi kimya kimya na watuhumiwa," anafafanua Ngwale.

Anadokeza kuwa sehemu ya mkakati mpya wa uliopo ni; "Kujenga nyumba salama ya kihifadhi wanafunzi waliopewa ujauzito ili wasirudi kuishi nyumbani kwao na kuanza kurubuniwa."

Kwa mujibu wa Ngwale, mtazamo wa kiserikali ni kwamba endapo watuhumiwa wataadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo zinazogusa hadi kifungo cha miaka 30, mimba na ndoa za utotoni zitakoma Shinyanga na kubaki historia.

### DC KISHAPU

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Nyabaganga Taraba, anawataka wasimamizi wa sheria watekeleze majukumu yao kwa vitendo, ikiwamo kuwachukulia hatua wanaochezea mwenendo wa jesi husika, akisema binafsi ni tataizo linalomuumiza sana kichwa wilayani kwake.

Mkuu wa Wilaya anasema, kwa kiasi kikubwa, wanafunzi wanaopata mimba, wengi wako katika rekodi ya kufanya vizuri darasani, lakini linapokuja suala la kuwakamata watuhumiwa kesi zao huishia njiani, watuhumiwa wakiachiwa huru, sababu kuu ni ushahidi kukosekana.

"Ili tatizo la mimba hizi za wanafunzi zipate kukoma mkoani Shinyanga, ni lazima wasimamizi wa sheria watekeleze majukumu yao ipasavyo.

'Kwa sababu, kesi hizi zimekuwa zikichezewa sana na kugeuka kuwa 'ATM' za watu wanaozungumza na watuhumiwa na kisha wanapewa 'kitu kidogo' hatimaye inapotelea hewani," analalamika Taraba.

### MZEE WA MILA

Mzee wa kimila mkazi wa Shinyanga kutoka Kijiji cha Welezo Kata ya Nsalala Shinyanga Vijijini, Kapaya Sosoma, anasema tamaduni za kabila la Wasukuma huwa hawapendi kesi pamoja na kutosomesha mtoto wa kike, na ndio maana mwanafunzi akipata ujauzito wao tayari wameshahesabu ng'ombe na kuona kama baraka katika familia.

Anasema jambo jingine Msukuma huwa anaogopa sana askali Polisi pamoja na hakimu, na ndio maana likifika suala la mashitaka hua hawapendi kutoa ushahidi, na kuamua kumalizana na mtuhumiwa kwa kupewa fedha au mifugo, na hatimaye kuacha kuhudhuria mahakamani na kumrubuni mtoto kumkana mtuhumiwa na kesi inafutwa.

"Mimi mwenyewe ni shuhuda mzuri tu, wakati fulani nilipokuwa mwenyekiti wa kijiji nilipata kesi moja ya mwanafunzi kupewa ujauzito, nilipomwita mzazi wake kuwa tukafungue kesi ili mtuhumiwa apate kuchukuliwa hatua kali za kisheria, mzazi huyo alikataa na kusema yeye hapendi kesi," anasema Sosoma.

"Wakati nikiendelea kumshawishi mzazi huyo aligoma kabisa na kufikia hatua ya kumwita mtuhumiwa wakazungumza naye, kisha akamwambia akimbie hapo kijijini aende kusikojulikana, mwisho wa siku hakuna kilichoendelea, mwanafunzi huyo akajifungua mtoto na hatimaye kuzima ndoto zake," anaongeza.

### MZAZI JE?

Mmoja wa wazazi Salehe Manota, anakiri jamii ya watu wa kabila wa Wasukuma huwa hawapendi kesi, na kubainisha kuwa endapo ukamshtaki mtuhumiwa aliyempatia mimba mtoto wako na akafungwa jela, kutatokea uhasama mkubwa sana kati ya ukoo wa mtuhumiwa na hata wanakijiji kutenga kwa kuonekana una mkosi.

"Ni kweli kesi nyingi za watuhumiwa wanaowapatia ujauzito mwanafunzi hua zinaishia njiani kwasababu ya kuogopa uhasama wa kifamilia, na ndio maana wazazi humalizana na watuhumiwa kimya kimya, pamoja na baadhi ya watumishi wa serikali ambao huifuatilia kesi hiyo, ili ipate kuisha tuendelee na maisha mengine," anasema Manota.

### KATIBU TAWALA

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga Albert Masovela, anabainisha kuchukizwa na kuendelea kuwapo na mimba hizo za wanafunzi, licha ya kuwepo jitihada za serikali, pamoja na mashirika binafsi kuungana kwa pamoja kuzitokomeza lakini hali bado ipo pale pale.

Anasema, kinachopaswa sasa ni maofisa ustawi wa jamii kuanzia ngazi zote, pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali, yaendelee kutoa elimu kwa wananchi waachane na mila na desturi zilizopitwa na wakati za kutopenda kusomesha watoto wa kike, na kuacha kuwa ozesha ndoa za utotoni pamoja na kuwa elezea madhara yake.

Aidha, anasema hata kwa matokeo ya wanafunzi 12,354 waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwakani (2020), ana hofu huenda wasi ripoti wote shuleni sababu baadhi yao watakutwa hata na ujauzito au wameshaolewa ndoa za utotoni, kipindi walipokuwa nyumbani wakisubiri matokeo walipohitimu darasa la saba.

"Mkoa wetu wa Shinyanga bado unakabiliwa na tatizo kubwa sana la wanafunzi kuwepa ujauzito na hofu yangu hata hawa wanafunzi wa kike 12,354 ambao wamefaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, huenda wasi ripoti wote shule sababu ya kuwa na ujauzito au wameshaolewa," anasema Msovela.

"Elimu hii ya mila, desturi zilizopitwa na wakati na madhara ya watoto wadogo kupewa ujauzito inapaswa kuendelea kutolewa zaidi ndani ya jamii, pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria watuhumiwa wa matukio hayo na wale ambao huzichezea kesi hizo, ikiwa sheria ipo wazi kabisa ili liwefundisho kwa watu wengine," ameongeza.

### WADAU KAMPENI

John Myola, ni Mkurugenzi wa Shirika la Agape mkoani Shinyanga, linalotetea haki za wanawake, wasichana na watoto, anasema katika kutekeleza miradi yao kuhusu elimu ya afya ya uzazi na jinsia, wamekuwa wakikumbana na changamoto ya mila na desturi ambazo wazazi ni wagumu kuziacha.

> Ili tatizo la mimba hizi za wanafunzi zipate kukoma mkoani Shinyanga.

Anasema, licha ya kutoa elimu ya afya ya uzazi na jinsia, inayolenga kutokomeza mimba na ndoa za utotoni, kuna baadhi ya wazazi wanafuta maelekezo ya kutoendekeza kuozesha wanafunzi, lakini baadhi ni wagumu.

Mkurugenzi wa Shirika la Fikra Mpya mkoani Shinyanga, Leah Josiah, wanaotetea haki za watoto, anasema katika kupambana na kutokomeza mimba za wanafunzi, wamekuwa wakizunguka shuleni kuzungumza na wanafunzi wa kike na kuwapatia elimu ya kujitambua, ili waache ngono katika umri mdogo.

Anasema kwa huu unaosikia ukiongoni, wameshatembelea shule 13 kutoa elimu hiyo ya kujitambua kwa wanafuzi wa kike, jambo analoamini litasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mimba za shuleni, muhimu ni kuelewa vyema madhara ya kushiriki ngono katika umri mdogo.

---

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

## Tunaojitosa uchaguzi shime tukawajibike




Wananchi wakipiga kura katika uchaguzi mkuu uliopita. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

LEO tunafika tamati ya mwaka. Tunapoanza siku ya kwanza ya mwaka huu 2020, ni vyema tukajiandaa kisaikolojia kwamba, mwaka huo unaoanza uwe wa uwajibikaji.

Nasema hilo kwa kutazama kilichokuwa kwenye ajenda yetu ya taifa kama Tanzania. Mosi, mwaka huu 2020 tunatarajia kufanya uchaguzi mkuu utakaohusisha nafasi ya marais wa Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Pia wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, madiwani Bara na wenzao wa ngazi yao Zanzibar.

Kimsingi, hilo linatajawa kuwa tukio muhimu na la kipekee, kwa sababu ya msingi kwamba inaendana na uwajibikaji kwenye siasa, unaojenga uwajibikaji kwenye jamii na maisha yetu katika mustakabali.

Nianze kuwapongeza wanaowajibikia nafasi zao hongera na wanaopotoka, wajitathmini kama wanahitajika tena.

Kipindi cha siasa za uchaguzi duniani kote, wagombea wa kawaida hutumia mbinu tofauti za kutafuta kuungwa mkono ili kushinda uchaguzi wenyewe.

Tupate darasa kidogo la kiamtaifa. Ni hivi karibuni dunia imeshuhudia namna Bunge la Marekani mwaka huu lilivyochukulia hatua kwa Rais Donald Trump, kwa madai ya kutumia madaraka yake vibaya.

Pamoja na hilo, Rais Trump, inasemekana anadaiwa kushirikisha Russia, katika uhusiano uliohujumu uchaguzi mkuu uliomwingiza madarakani.

Kwa mujibu wa taratibu za Marekani ushirikiano huo unachukua sura ya uhaini. Maswali mengi yanaulizwa kwamba, Je, Russia ilikuwa na maslahi gani hata kumsaidia Rais Trump?

Kwa maana hiyo, tunapoelekea uchaguzi mkuu, ni vyema sote tukawa waangalizi na kamwe tusiliache jukumu hili kwa waangalizi wa nje ya nchi tu. Ubora wa shamba unaanzia kwa mkulima, kisha bwana shamba anafuata.

Rushwa kwenye uchaguzi huathiri haki na huanzia kwenye upigaji kura, tena mzizi wake unashuka mapema kwenye mchakato wa kutafuta wagombea.

Vyama husika ni sharti viweke taratibu na miongozo itayokuwa wazi na wezeshi kwa wagombea wote, zikiwamo kada za wanawake, vijana na walemavu.

Miongozo hiyo inapaswa ilenge kupata viongozi bora na sio bora viongozi.

Kwa utaratibu uliopo ni kwamba vyama vinapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha rushwa na matumizi ya fedha hayaathiri utaratibu mzima kwa mgombea yeyote.

Sio sahihi kwa mtu akiwajibika na akatumia fedha kuhonga wapigakura kwa mbinu zinazolenga kununua uongozi. Inapotokea rushwa inatumika kupata uongozi, wanufaika huchukulia nafasi hizo walizipata kama mali binafsi na wanahisi ni fedha ndizo zimewawezesha kuzipata nafasi hizo.

Pia inaenda mbali kwamba wanakalia nafasi hizo kama matunda ya hongo na muda wao wa kutumia wadhifa kurejesha fedha walizotumia.

Viongozi wanaopatikana kwa utaratibu huo hawafai. Sasa huu mwaka 2020 ni fursa kwa Watanzania kupata viongozi kwa taratibu za wazi zinazokubalika.

Uchaguzi wetu unapaswa kuwa wa mfano ukanda wote wa Afrika Mashariki na bara zima, njia bora ni kuchagua viongozi waadilifu, tutakawaanda na kuchagua kupiga hatua ya kimaendeleo itakayoongozwa na viongozi wenye hadhi na taswira ya uwajibikaji.

Ni viongozi wawajibikaji pekee, ndio watakuwa na uthubutu wa kuhoji mapato na matumizi, kitendo kitakachowaweka kwenye nafasi nzuri kuhakikisha maendeleo ya jamii hayaathiriki kwa viashiria vya rushwa na ufisadi.

**Kwa maoni na ushauri, wasiliana kwa baruapepe: samawatiarts@yahoo.com**

## JE, WAJUA?



Mkazi wa mji wa Kfr Nabil nchini Syria akiwa amezungukwa na paka. **PICHA: MTANDAO**

# Mji wa Syria una paka wengi kuliko watu

BAADA ya miezi kadhaa ya mashambulio ya mabomu kutoka kwa vikosi vya Syria na Urusi, mji wa Kafr Nabl nchini Syria sasa umesalia kuwa makazi ya paka wengi kuliko watu.

Watu wachache waliosalia katika mji huo wa Syria uliolipuliwa wanajiliwaza na mamia au pengine maelfu ya paka, kama ilivyobaini BBC. Baadhi ya wakazi hujificha chini ya kifusi cha nyumba zilizobomolewa ili kujikinga dhidi ya mabomu yanayodondoshwa kutoka angani.

Mmoja wao ni Salah Jaar mwenye umri wa miaka 32, lakini kama unavyoona hayuko peke yake.

Katika kifusi kilicho karibu naye, kuna mamia ya paka waliojikuta katika hali kama yake.

"Unafarijika paka akiwa karibu nawe."

Nyumbani kwa Salah katika Mji wa Kafr Nabl, wakati mmoja ulikuwa makazi ya watu 40,000, lakini sasa ni watu chini ya 100 waliosalia.

Ni vigumu kubaini ni paka wangapi walio katika mji huo, ni mamia kwa hakika lakini huenda wako kwa maelfu.

"Watu wengi wamehama mji wa Kafr Nabl hali iliyofanya idadi ya watu kuwa ndogo sana. Kwa kuwa paka wanahitaji watu wa kuwatunza kuwapa maji na chakula, wamehamia katika nyumba za watu walioamua kubaki katika mji huo ...kila nyumba ina karibu paka 15, au hata zaidi," anasema Salah.

Bado Salah anafanya kazi ya uandishi habari katika kituo cha radio cha Fresh FM, japo studio za kituo hicho zilibomolewa katika mashambulizi ya angani ya hivi karibuni.

Walikuwa na bahati shughuli za kituo hicho zilihamishiwa mji ulio karibu kutokana na sababu za kiusalama, muda mfupi kabla ya mashambulio hayo.

Kituo hicho ambacho huwatangazia watu kuhusu kitisho cha mashambulio kupitia habari, na vipindi vingine kilipata umaarufu kutokana na paka.

> Paka wengi walizaliwa katika jengo hilo. Mmoja wao aliyekuwa na rangi nyeupe na madoa ya hudhurungi alimpenda sana Raed. Angeliandamana naye kila mahali na hata kulala kando yake.

Makumi kati ya paka hao walifanya ofisi za kituo hicho kuwa makazi yao. Mwasisi wa kituo hicho na mwanaharakati Raed Fares, aliyeuawa na wanamgambo wa Kiislam wenye silaha mwezi Novemba 2018, alitenga fedha za kuwanunulia maziwa na chakula.

"Paka wengi walizaliwa katika jengo hilo. Mmoja wao aliyekuwa na rangi nyeupe na madoa ya hudhurungi alimpenda sana Raed. Angeliandamana naye kila mahali na hata kulala kando yake," anasema Salah.

Anapoondoka katika mabaki ya iliyokuwa nyumba yake, anakaribishwa na sauti za paka kutoka kila upande. "Hili humtokea kila mtu," anasema na kuongeza.

"Wakati mwingine tunapotembea njiani tunaweza kutana na paka 20 au 30 wanaoandamana na sisi kila tunapoenda. Baadhi yao walitufuata hadi nyumbani."

Giza linapoingia milio ya mbwa wasio na wenyewe husikika kutoka kila upande wa mji huo. Wao pia wana njaa na hawana pakwenda. Hali ya kupigania mabaki ya chakula na mahali pa kulala inawafanya kushindana na paka wa Kafr Nabl.

Katika makabiliano kati ya paka na mbwa mshindi ni nani?

"Bila shaka mshindi ni paka! Wako wengi sana kuliko mbwa hao," anasisitiza.

Wengi wao walikuwa wanapendwa sana na familia zilizotoroka mji huo baada ya vikosi vya utawala wa Syria kuanzisha operesheni ya kukomboa mji wa Idlib mwezi Aprili.

Sasa baada ya kukosa wa kuwatunza na chakula cha mara kwa mara wamelazimika kutafuta makazi mapya chini ya kifusi cha mijengo iliyoporomoka.

Na japo watu kama Salah hawana matumaini ya kuishi, bila kujua chakula kinatoka wapi, wanajiliwaza na paka hawa ambao wamegeuka kuwa marafiki wa dhati.

"Kila ninapokula, nao hula, iwe ni maboga, spageti au hata mkate uliokauka. Katika hali hii nahisi sote ni viumbe wadhaifu na tunahitaji kusaidiana," anasema. **BBC**

## UTAFITI

# Ukarimu unaweza kukusaidia kuishi muda mrefu

UKARIMU gani unaweza kuufanya? Je, ni sawa mtu kuonyesha hisia zake?

Inawezekana kuna ukweli, wanasayansi na wasomi katika kituo cha utafiti wanasema kuwa mtu anaweza kufanya mambo mengi zaidi ya ukarimu na kuongeza muda wa kuishi. Wafanyakazi wa Taasisi ya Ukarimu ya Bedari iliyopo Chuo Kikuu cha California, huko Los Angeles nchini Marekani (UCLA), wako tayari kwa ajili ya utani.

"Tukiangalia upande wa kisayansi. Ni kama tuko kwenye mzunguko, hapa tunazungumzia upande wa kisaikolojia na kibaiolojia," anasema Daniel Fessler, mkurugenzi wa taasisi hiyo.

Suala la mtu kuwa mkarimu limechukua vichwa vya habari hivi karibuni. Rais wa zamani wa Marekani Barack Obama anasema kuwa: "Kuwa jasiri ni ukarimu, hakuna ubaya kwa mtu kuwa dhaifu au kuwa na huruma," anasema na kuongeza: "Mtu kuwajali watu wengine si udhaifu, ni jambo jema... tunapaswa kujali wengine kwa kuwa na uadilifu na kuwajali wengine kwa heshima."

Ellen DeGeneres aliwahi kuzungumzia ukarimu wakati akizungumzia urafiki wake na George W Bush:

"Ninaposema kuwa mkarimu, unapaswa kuwa mkarimu kwa wengine, simaanishi kama watu wanafikiria sawa na vile wanavyotenda...ninachomaanisha ni kwamba uwe mkarimu kwa kila mtu bila kujali," anasema.

### UKARIMU UNA MAANA GANI NA KWA NINI NI MUHIMU?

Hilo ndilo jambo ambalo wataalamu wanataka kufanyia utafiti. Je, wako makini? Na je, ni suala ambalo linazingatia uhai na vifo vya watu?

Kazi ya Fessler ilikuwa ni kuangalia namna ambavyo watu wanaweza kushawishika kufanya vitendo vya ukarimu, kwa kushuhudia fadhila na kueneza ukarimu.

"Nadhani ni sawa kusema kuwa tunaishi katika umri ambao si rafiki...duniani kote, kile tunachokiona ni ongezeko la migogoro baina ya watu ambao wana maoni tofauti katika masuala ya kisiasa au tofauti za kiimani," anasema.

Anabainisha kwamba ukarimu ni fikra, hisia na imani ambayo ina uhusiano na hatua ambazo zinaweza kuwanufaisha wengine, na kwamba kuwanufaisha wengine haimaanishi kuwa ndio mwisho.

Anasema kutokuwa mkarimu kwa upande mwingine ni jambo ambalo lisilovumilika kutokana na watu kupunguza thamani kwa wengine. Fessler anasema kuwa msongo wa mawazo ni miongoni mwa changamoto. Kuishi na watu kwa wanakutendea vizuri ni bora, kuliko kuishi kwa hofu na mbaya zaidi kunafupisha maisha yako.

Kuishi na watu kwa ukarimu, na kuonyesha namna mtu anaweza kuwa mkarimu kwa wengine kunasaidia mtu kupata tatizo la shinikizo la damu.

Mara nyingi huwa rahisi kuwa mkarimu kwa wengine kuliko kwako mwenyewe, anasema mtafiti.

"Kuna namna nyingi sana kuonyesha ukarimu kwetu binafsi na kwa watu wengine. Katika maeneo ya kazi, shuleni na nyumbani, ni maeneo ambayo mtu unaweza kuonyesha huruma na upendo kwa wengine."

Lakini ukarimu hauwezi kuchukua mbadala wa namna ambavyo watu wanaweza kujali wengine.



Rais mstaafu wa Marekani, Barack Obama ni mmoja wa waumini wa ukarimu. **PICHA: MTANDAO**

SAYANSI

NA FELICIAN KILAHAMA

# Kilwa inavyowekeza kwa watu kuishi kirafiki na mazingira

KWA kipindi cha Desemba 18 mpaka 30, 2019, nilipata fursa ya kutembelea Wilaya ya Kilwa.

Kama ilivyo ada baada ya kufika Masoko, ilibidi kujitambulisha kwa Mkuu wa Wilaya Christopher Ngubiagai, na kwa bahati nzuri nilimkuta ofisini mwake akichapa kazi.

Niliongozana na Ofisa Misitu wa Wilaya, Njabha Lyatura na Makala Jaspar ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Mpingo Conservation and Development Initiative (MCDI). Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kufika Kilwa Masoko salama.

Baada ya ukaribisho na kueleza nia ya kuwapo hapo, Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa Kilwa ni Wilaya mkoani Lindi yenye ardhi kilometa za mraba 13,347.5. Kiutawala wilaya hiyo ina tarafa sita, kata 20 na vijiji 97 vilivyoandikishwa. Kiuhalisia Kilwa bado haijawa na wingi wa watu maana ni takribani watu 14 katika kilometa za mraba, ingawa kuna watu wengi kwenye Kata ya Songosongo (watu 454 katika kwa kilometa za mraba).

Kilwa inayo misitu iliyohifadhiwa kisheria yenye jumla ya hekta 228,400 pia hekta 15,410 za mikoko.

Vilevile, kuna hekta zipatazo 287,384.9 zilizohifadhiwa kwenye ardhi ya vijiji 12 wilayani humo.

Sehemu kubwa ya uvunaji wa rasilimali misitu ni kwa ajili ya kuni, mkaa, nguzo, mbao na magogo.

Wavunaji wengi wakipendelea aina za mninga, mhongo, mpangapanga, msekeseke, pamosa, msufi na mtondo/mtondoro. Kulingana na ufafanuzi wa Mkuu wa Wilaya, wilaya hiyo inanufaika kutokana na misitu ya asili iliyo kwenye ardhi ya vijiji.

Anasema kuwa tangu mwaka 2004, Halmashauri ya Wilaya hiyo inawekeza kwa wanajamii kwa ajili ya kulinda na kuendeleza mazingira.

Ngubiagai anaishukuru Serikali Kuu kwa kuweka sera nzuri na Sheria ya Misitu (Cap323 RE: 2002) vyote kwa pamoja vilivyosababisha wananchi kuitunza misitu ya asili iliyo kwenye ardhi ya vijiji na hatimaye kunufaika kimapato na kimazingira.

Vyombo hivyo (Sera na Sheria) vinatoa fursa kwa serikali za vijiji kutangaza na kuhifadhi misitu ya vijiji kwa faida ya wanakijiji husika.

Hivyo kupitia programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu na hasa misitu inayosimamiwa na jamii; wahusika wanaweza kunufaika na rasilimali misitu kwa misingi endelevu.

**MKURUGENZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilwa anabainisha kwamba kupitia misaada inayotolewa na MCDI kwa ushirikiano na Halmashauri ya Kilwa, lakini na halmashauri zingine kusini mwa Tanzania, uhifadhi na matumizi endelevu wa rasilimali za misitu umekuwa wa kutia moyo.



Hifadhi ya misitu kama hii muhimu kwa mazingira. **PICHA: MTANDAO.**

Anabainisha tangu mwaka 2004, halmashauri imewekeza kwa wanavijiji kupitia Programu ya Taifa ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu hususani misitu ya jamii. Anasema, utekelezaji wa suala hili ulianza taratibu kupitia Kijiji cha Kikole; ambako Serikali ya Kijiji ilitenga hekta 454 za msitu na hatimaye kuutangaza kuwa msitu uliohifadhiwa kwenye ardhi ya kijiji.

Hata hivyo, kutokana na ushirikiano mzuri na wadau katika maendeleo; MCDI iliweza kutoa misaada ya kitaaluma na fedha hivyo kuiongezea nguvu halmashauri kuwekeza kwa jamii vijijini ili kutunza na kuishi kirafiki na mazingira.

Aidha, juhudi za MCDI ziliwezesha vijiji 12 katika Wilaya ya Kilwa kuingizwa kwenye programu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (misitu ya jamii), wananchi wakaelimishwa kuhusu umuhimu na faida za misitu.

Halmashauri kwa kushirikiana na MCDI pamoja wadau wengine kama WWF; jamii vijijini ikajengewa uwezo wa kulinda, kusimamia na kutumia rasilimali misitu kiuendelevu.

Juhudi zilizofanyika wilayani Kilwa tangu 2004 hadi sasa mafanikio yake yanaridhisha. Inatia moyo kwamba rasilimali misitu zilizokuwa zinaharibiwa kutokana na kilimo cha kuhamahama, kuanzisha makazi kiholela na kuteketeza misitu kwa mioto kichaa; sasa inatunzwa na wanavijiji kunufaika ipasavyo.

Jamii katika vijiji vyenye rasilimali misitu wilayani Kilwa; ina uelewa mkubwa kuhusu manufaa ya misitu siyo tu kwa kuboresha hali ya hewa na mazingira kwa ujumla, bali pia kuwawezesha kunufaika kutokana na mapato yatokanayo na rasilimali misitu.

Kwa uwezo jamii iliyojengewa kwa kipindi cha miaka 15 iliyopita; sasa wanapanda miti ya asili na kuvuna iliyopo kwa njia endelevu.

Miti aina ya mipingo na miombo inapandwa kwa wingi kwa nia ya kuimarisha uoto wa asili na mazingira.

Kujituma na kudhamiria kwelikweli, halmashauri kwa kushirikiana na MCDI pamoja na WWF; jamii kwenye vijiji 12 imeweza kuingiza kipato cha shilingi bilioni 1.6 kutokana na usimamizi shirikishi wa misitu.

Kwa njia hiyo wafanyabiashara wa mazao ya misitu toka ndani na nje ya Tanzania, wameweza kununua bidhaa kutoka kwenye misitu iliyosimamia ipasavyo na kwa viwango vya kimataifa mpaka kupewa cheti kila mwaka kupitia mpango wa kimataifa wa uthibitishaji misitu (Forest Certification).

Hadi mwaka huu wa 2019 unamalizika, fedha zilizopatikana zimetumika kuboresha maisha ya jamii kupitia utekelezaji wa miradi ya kijamii kwa faida ya wote. Mathalani, kusaidia wajawazito 236 kwa kuwapatia Sh. 50,000 ili kununua vifaa muhimu vinavyohitajika wakati wa kujifungua, lakini kuwezesha watu 15 kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya.

Aidha, ujenzi wa nyumba ya nesi kijijini na kuwezesha watu 10 wasiojiweza kupatiwa bima za afya.

Vilevile, ofisi za vijiji vitatu zimejengwa; nyumba moja ya kulala wageni (village guest house) imejengwa na inatumika. Pia fedha hizo zimewezesha ujenzi wa soko la kijiji ili wanakijiji wafanye biashara kwa urahisi. Kadhalika ujenzi wa ghala la nafaka umekamilika na pia kuchangia ununuzi wa mashine ya kusaga.

> “Kujituma na kudhamiria kwelikweli, halmashauri kwa kushirikiana na MCDI pamoja na WWF; jamii kwenye vijiji 12 imeweza kuingiza kipato cha shilingi bilioni 1.6 kutokana na usimamizi shirikishi wa misitu.

Vijiji vimeweza kukarabati visima tisa vya maji pamoja na pampu za umeme. Isitoshe wameweza kujenga nyumba ya mwalimu, shule ya msingi na kununua madawati 100 na vifaa vya shule pamoja na wanafunzi 20 kulipiwa ada na shule kuwekewa umeme.

Wanafunzi 323 kwa madarasa tofauti wamenunuliwa sare za shule.

Pamoja na jamii vijijini kujengewa uwezo wa kuisimamia misitu ya asili kwa manufaa mapana ya taifa letu; halmashauri na wadau wake wameendelea kujengea uwezo wa kujipatia kipato kupitia miradi mbadala kama ufugaji wa nyuki.

Kwa mfano, Kijiji cha Kisangi wana jamii saba wamepatiwa mafunzo juu ya ufugaji nyuki na tayari mizinga 23 imetundikwa kwenye eneo lililochaguliwa mahususi kwa kazi hiyo ya kuzalisha asali na bidhaa nyingine zitokanazo na rasilimali nyuki.

Tuwekeze kwa jamii kuweza kuishi kirafiki na mazingira asilia; kushindwa kufanya hivyo mazingira asilia yatatugeuka na kuwa mwiba kwetu, hivyo maisha yatakuwa magumu kuliko matarajio.

***Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki mstaafu, anapatikana kwa anwani ya P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania, fkilahama@gmail.com; +255756007400; +255714250050;***



WADAU SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

## WAKATI Tanzania ikielekea kuwa ya viwanda, bado kuna tatizo la uhaba wa walimu wa masomo ya Sayansi, kwenye baadhi ya sekondari za umma. Wadau wanasemaje?



**SIDADI ALFAN (MMILIKI WA KITUO SIDADI DAY CARE, DAR ES SALAAM)**

WAKATI tukielekea Tanzania ya viwanda kumekuwa na changamoto ya walimu kwa sababu tulihamasishwa kila kata kuwe na sekondari tukafaulu, lakini hakukuwa na maandalizi ya walimu wa kutosha katika masomo muhimu kama tahasusi ya sayansi.

Ina maana hii inatokana na taifa kutokuwa na sera hasa watunga Sera ya Taifa, badala yake kunakuwa na utekelezaji wa kisiasa.

Nina imani kubwa huu mpango wa viwanda ndio ulikuwa ni mpango ulioitwa wa milenia 2015-2035 lakini ukakimbizwa bila kufuata hatua, kwa maana kila jibu la hesabu huwa na njia.

Hatuwezi kufikia Tanzania ya viwanda bila kuanza kuzalisha walimu kwanza katika tahasusi ya sayansi. Hatuwezi kupata wahandisi katika ujenzi wa madaraja, wakemia, wanafamasia wa kutosha, wala wahandisi katika uundaji wa magari, ndege na meli.

Hii ndiyo sehemu ya kuinua uchumi kwa haraka. Kwa kuwa tunaingia kwenye nchi ya viwanda yafuatayo yafanyike: Kubadilisha mifumo ya shule za sekondari ya kawaida na kuziingizia mfumo wa ufundi, kuthibitisha au kuvijengea uwezo vile vyuo vilivyojitolea kufundisha taaluma na si kuvifungia, kwani hata wanaotoka vyuo vikuu wanahitaji kushirikiana na wenye diploma, chini ya diploma kuwe na mtu mwenye cheti, kwani mara nyingi wanaomaliza vyuo ukiwaingiza kwa mtu mwenye diploma wanaachwa mbali kwani wa diploma ana vitendo, lakini huyu mwingine ni wa nadharia.

Hiyo yote ni kukosa mwanzo wenye vitendo tangu awali. Tutafakari ni wapi tulipokwama tuchukue hatua.



**RAHELI MGALLA (MHITIMU WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)**

KITAALAM mimi ni mwalimu ninayesubiri ajira. Kulingana na mada husika, napenda kuchangia kama ifuatavyo: Viwanda ni dhana pana, ambayo kwa hiyo inatakiwa iwe na mipango endelevu na mikakati imara, hivyo kulingana na Tanzania kuwekeza katika viwanda, ni vyema kujua kuwa viwanda vinataka elimu mchanganyiko.

Maana katika viwanda Kuna nadharia, vitendo, na mipango au mikakati. Kwa hiyo ni vyema tukawekeza katika walimu wote pia. Yaani wa sayansi, biashara na sanaa, kwa sababu walimu wa sayansi watasaidia katika vitendo, walimu wa sanaa watasaidia katika nadharia na walimu wa uchumi na biashara watasaidia katika kupanga biashara, bidhaa na masoko kwa ujumla.

Hivyo kama serikali itawekeza katika nyanja zote, ndipo Tanzania tutakuwa na mipango endelevu ya viwanda. Lakini tukijikita katika walimu wa sayansi tu, itafika kipindi watatakiwa wa uchumi, biashara na sanaa ili viwanda viendelee zaidi na hapo hatutakuwa nao na mwisho tutaonekana hatukuwa na mipango au mikakati ya muda mrefu, lakini pia ili tatizo la uhaba wa walimu wa masomo sayansi liishe katika sekondari za umma, inatakiwa kuwe na mikakati ya uzalishaji wa walimu hao.

Kwa mfano serikali inaweza kuamua kuzalisha asilimia fulani ya walimu wa sayansi na kuwafanya watoto wapende masomo hayo. Kama kuna haja ya kuwa na asilimia 40, ni lazima pia kuwe na mikakati ya watoto kupenda masomo hayo utawekaje. Ni muhimu kuboresha mazingira ya kusomea.



**ASHA JUMANNE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA hali ilivyo sasa, ni wazi kwamba Tanzania ya viwanda hatuwezi tukaifikia, kwa sababu shule nyingi za umma hazina walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi kwa ajili ya kuandaa wataalamu wa baadaye. Tutapataje wahandisi watakaoendesha mitambo ya viwanda ikiwa wanasayansi wanaogundua vitu hawapo?

Kwa mfano mtoto mmoja kutoka Morogoro, alitengeneza bunduki, lakini akahojiwa kwamba amepata wapi ujuzi. Lakini ndiyo wanasayansi wenyewe hao.

Kama angeendelezwa sisi wenyewe tungeweza kuiendeleza nchi. Serikali itafute wavumbuzi ili ifike mbali badala ya anapojitokeza anahojiwa na kutiwa hofu. Tunatakiwa kuwa na wanasayansi wetu, siyo kutegemea wa kutoka nje wakati watoto wetu wapo hapahapa.

Serikali iwe na mikakati ambayo itahakikisha shule zake zote zinakuwa na walimu wa kutosha, tena si wa kutosha tu, bali wafundishe ili baadaye nchi hii iwe na wanasayansi wengi wenye utaalamu wa aina mbalimbali. Nchi hii itafikaje kuwa Tanzania ya viwanda wakati masomo ya sayansi ni kama yamesahaulika kwa kukosa walimu wa kutosha?

Tukitaka tufike tunapotaka, masomo ya sayansi yapewe uzito unaotakiwa ili tupate watengenezaji wa ndege hapahapa na watengenezaji treni hapahapa na utaalam wa kila aina. Vinginevyo Tanzania ya viwanda hatutaifikia bila ya wataalamu wetu wenyewe.



**GIDEON OKETCH (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NI kweli kwamba walimu wa masomo ya sayansi ni wachache sana katika sekondari za umma na uhaba huu unachangiwa na wazazi kutowahamisisha watoto wao kuelekeza nguvu kwenye masomo hayo.

Badala yake wanafunzi wanakaririshwa tu kwamba masomo hayo ni magumu na kujikuta wakikata tamaa. Walimu pia huchangia toka shule za msingi kutotaka kupangiwa masomo hayo na hivyo kuchangia kuwapo kwa uhaba wa walimu wa masomo hayo katika shule za sekondari za serikali.

Vilevile serikali kwa upande wake haitoi motisha kwa walimu wa masomo ya sayansi. Kimsingi sayansi ina ugumu wake, hivyo serikali itoe hamasa na msisitizo pamoja na motisha kwa walimu na wanafunzi wanaofanya vizuri, katika masomo ya sayansi, na kuwe na warsha za masomo ya sayansi na mashindano yafanyike nchi nzima yakisimamiwa na serikali na wadau wa elimu, ikiwa ni njia mojawapo ya kuhamasisha kuwapo kwa walimu wa kutosha wa masomo hao, kwani tatizo hili la uhaba wa walimu linaanzia kwa walimu wenyewe kuogopa masomo hayo na kusababisha kuwapo kwa uhaba wao, hivyo njia hiyo ninayoisema inaweza kusaidia kuhamasisha wengi wao kuyapenda na kuyasomea ili baadaye waje kuyafundisha katika sekondari mbalimbali. Wazazi kwa upande nao wawahamasishe watoto wao kupenda masomo ya sayansi na kuwapa mifano ya mafanikio mengi ya masomo hayo.



**EMMANUEL AKONAY (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

UPUNGUFU wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari za serikali ni tatizo, hasa zile za pembezoni, na kwa hali kama hii tunaweza kukosa wataalamu wa baadaye wa fani mbalimbali.

Niliwahi kusikia kwenye vyombo vya habari kwamba mkoa fulani shule zilikuwa zikilazimishwa kuchangia Sh. milioni moja kwa ajili ya kuwaendeleza walimu waliopo, hali ambayo ililalamikiwa na walimu. Hii inaonyesha kweli kuna uhaba wa walimu wa masomo hayo nchini na sijui sababu ni nini.

Kama wapo waliohitimu vyuo na hawajaajiriwa, basi serikali iwaajiri mapema ili kusaidia kumaliza tatizo la upungufu wa walimu wa masomo hayo. Aidha, kuwe na mikakati maalumu ya kuwaandaa vijana kuwa walimu wa kufundisha masomo yatakayowasaidia wanafunzi kujitegemea na siyo kutegemea ajira.

Kujenga kizazi, ambacho kitaweza kujitegemea na kupambana na maisha, hivyo ni muhimu kujikita zaidi, katika kuzalisha walimu vijana, ambao pia watafundishwa mbinu za kuwawezesha wanafunzi pindi watakapohitimu wajue jinsi ya kujitegemea. Lakini kikubwa zaidi ni kupata wataalamu wa fani mbalimbali ili waweze kusaidia nchi kufikia kuwa ya viwanda.



# Ahimiza amani Mwaka Mpya

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKAZI wa Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kusherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya kwa amani na utulivu ili wavuke salama mwaka na kuuanza mwaka 2020 kwa kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alipokuwa anazungumza na wanahabari kwa lengo la kuwatakia heri ya Mwaka Mpya wananchi wa mkoa huo, ambapo alisema mkoa kwa sasa ni salama na hakuna matukio ya ajabu ajabu.

Chalamila alisema wananchi wanatakiwa waendeleze amani iliyopo kwa kuheshimiana na kuthaminiana wao kwa wao na kila mmoja atekeleze wajibu wake.

Alisema Jeshi la Polisi litaimarisha ulinzi katika maeneo yote muhimu kwa ajili ya kuwadhibiti wale wote watakaotaka kufanya uhalifu maeneo hayo na kuwanyima amani wenzao.

"Tunatamani kila mmoja aumalize mwaka kwa amani, lakini niwaambie tu kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vipo kwa ajili ya kudhibiti tabia za watu, hivyo kwa atakayetaka kuvuruga amani ni lazima vimshughulikie," alisema Chalamila.

Aliwataka wazazi na walezi kujiandaa kwa ajili ya kuwapeleka watoto wao shuleni mwezi Januari wakiwamo wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza na wale waliofikia umri wa kuanza darasa la kwanza.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliwataka wazazi kuwalinda watoto wao wakati wa sikukuu ili kuepuka madhara yanayoweza yakawakuta.

Alisema watoto wasiachwe peke yao wakizurura mitaani wakati wa mkesha wa Mwaka Mpya, na kwamba endapo kutakuwa na ulazima wa kwenda kutembea basi wanatakiwa waambatane na watu wazima.

"Watoto hawatakiwa kuingia kwenye kumbi za starehe na sisi Jeshi la Polisi tutakuwa tunafanya doria maeneo mbalimbali na endapo sehemu yoyote ya starehe watakutwa watoto ni lazima mmiliki wa eneo hilo atawajibika," alisema Matei.

Alisisitiza watumiaji wa vyombo vya moto kuepuka kuendesha wakiwa wamelewa kwa maelezo kuwa wanaweza wakasababisha ajali ambazo zinaweza zikagharimu maisha yao pamoja na ya watu wengine wanaotumia barabara hizo.

# Mbaroni tuhuma kukwepa kodi ya shehena vitenge

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WATU watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuingiza nchini shehena za vitenge kutoka nchi jirani za Malawi na Zambia kwa kupitia njia za panya ili kukwepa kulipa kodi na ushuru wa forodha.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa hao walikamatwa kwenye matukio mawili tofauti ambapo tukio moja linawahusisha watuhumiwa wawili na lingine linamhusu mmoja.

Alisema tukio la kwanza lilitokea Desemba 22 mwaka huu majira ya usiku, ambapo watu wawili ambao wanajulikana kwa majina ya Elia Mwakagile (30) na Furaha Mwakalengela (35), wakazi wa Mwakibete jijini Mbeya, walinaswa wakisafirisha mabelo 24 ya vitenge.

Matei alisema watuhumiwa walikamatwa eneo la Ituta lililopo Kata ya Iyunga jijini Mbeya, Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam) wakiwa wanasafirisha mzigo huo kwa kutumia gari binafsi aina ya Toyota Hiace yenye namba za usajili T.471 BJJ.

"Watuhumiwa hawa walikamatwa na askari wa doria ambao walikuwa katika kituo, waliposimamishwa na kukaguliwa ndio mzigo huu ukakutwa ukiwa umefichwa nyuma ya gari na hawakuwa na nyaraka zozote zinazoonyesha kuwa walilipa chochote," alisema Matei.

Alisema baada ya maaskari hao kuwahoji watuhumiwa hawakuwa na majibu ya kueleweka, ndipo wakapelekwa kituo cha Polisi. Alisema mzigo huo ulifunguliwa na kubaini kuwa kila belo lina doti 50 za vitenge ambapo yote kwa ujumla yana doti 1,200, na kwamba jeshi hilo linaendelea na taratibu za kuwakabidhi watuhumiwa pamoja na mzigo wao kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya taratibu zingine.

Kwa mujibu wa Kamanda Matei, tukio la pili lilitoke Desemba 22 mwaka huu ambapo jeshi lilimnasa mwanamke mmoja ajulikanaye kwa jina la Mariam Japhet (35), mkazi wa Kata ya Ilembo wilayani Mbeya akiwa na doti 42 za vitenge ambavyo aliviingiza kutoka Malawi bila kulipia ushuru.

Alisema mwanamke huyo alikamatwa majira ya saa 12:30 alfajiri katika Kata ya Kyela Kati, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela na baada ya kumhoji ilibainika kuwa hana nyaraka zozote zinazoonyesha kuwa alikuwa amelipia ushuru.

Alisema mtuhumiwa pia pamoja na mzigo wake atakabidhiwa TRA kwa ajili ya hatua zingine za kisheria.



Mjumbe wa Baraza Kuu la Wazazi Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya (kulia), akikabidhi msaada wa mashine ya kudurufu maandishi (Printer) kwa viongozi wa jumuiya hiyo, Wilaya ya Kyela kama sehemu ya mkakati wake wa kuimarisha jumuiya katika wilaya zote. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wataalamu wazembe Tamisemi waonywa

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

NAIBU Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia masuala ya Afya, Dk. Doroth Gwajima, amekemea vitendo vya baadhi ya wataalamu wa idara hiyo kutotimiza wajibu wao ipasavyo katika kukagua miradi.

Amesema baadhi ya miradi inafikia mpaka hatua ya kuanza kutumika, huku ikiwa imekosewa, hivyo kutakiwa kubomolewa ili kuanza upya ama kufanyiwa marekebisho hali ambayo inasababisha ongezeko la gharama za miradi hiyo.

Dk. Doroth aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye ziara ya kukagua miradi ya afya katika Halmashauri ya Busokelo ambako alikagua hospitali yenye hadhi ya wilaya inayojengwa na serikali kwa Sh. bilioni 1.5.

Aliwataka wakaguzi hao kuzungumza lugha moja na makandarasi ili kuepuka mivutano isiyokuwa ya lazima ambayo inaweza ikasababisha mradi kutakiwa kuanzwa upya ama kufanyiwa marekebisho baada ya hatua za mwisho kufikiwa.

Alisema kwa sasa serikali itakuwa inafanya mapitio ya fedha za miradi inazotoa ili kujiridhisha na matumizi yake kama ni yaliyokusudiwa ama kuna baadhi wanafanyia vitu vingine.

"Kuna baadhi ya maeneo nchini unakuta mkandarasi anafikia hatua ya mwisho kwenye ujenzi ndio inabainika kuwa kuna makosa, kwa sasa ninyi wenye mamlaka ya ukaguzi ndio mtakuwa mnafidia hizo gharama za marekebisho ambayo mnatakiwa kuyadhibiti tangia mwanzo," alisema Dk. Doroth.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Busokelo, Dk. Ramadhani Hussein, alisema ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hiyo unaenda vizuri na kila mtaalamu anayetakiwa kufanya ukaguzi anatimiza wajibu wake ipasavyo ili kuhakikisha hautokei upungufu.

Alisema alishatoa maelekezo kwa kila mmoja kupitia eneo linalomhusu ili kubaini upungufu uliyopo na kufanyiwa marekebisho ili maelekezo ya Idara ya Afya yazingatiwe ipasavyo.

"Tangu tumeanza ujenzi mpaka sasa, wataalamu wa idara zote ambazo zitakuwapo hapa wameendelea kukagua maeneo yao na nimetoa maelekezo kila mmoja kuhakikisha eneo lake liko sawa kwa mujibu wa matakwa ya idara," alisema Dk. Hussein.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Eston Ngilangwa, alisema baadhi ya idara zimeshakamilika kwenye mradi huo na baadhi ziko katika hatua za mwisho na kwamba kufikia Januari mwakani zitakuwa zimekamilika.

Ngilagwa alisema endapo watapata vifaa tiba mapema wanakusudia kumalizia idara ya wagonjwa wa nje mwanzoni mwa mwezi Januari na kuanza kufanya kazi.

Alisema katika ujenzi huo wanahakikisha kila idara inajengwa kwa kuzingatia ubora unaohitajika na kwa thamani halisi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo.





# TFS kuelimisha vijiji mipaka ya hifadhi

Na Renatha Msungu, DODOMA

WAKALA wa Misitu nchini (TFS) kwa kushirikiana na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, wanatarajia kuanza kutoa elimu katika vijiji 150, vilivyo karibu na hifadhi ya misitu ili kujua mipaka yao na ya hifadhi.

Mkurugenzi wa TFS, Profesa Desantos Silayo, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mikakati waliojiwekea kuhakikisha wanadhibiti ukataji ovyo wa misitu ikiwamo uchomaji moto.

Profesa Silayo alisema, lengo la kutoa elimu hiyo ni pamoja na kutaka kupunguza migogoro kwa wananchi wasio na uwelewa kuhusu mipaka ya hifadhi ya misitu na maeneo yanayostahili kuendeshwa kilimo kwa jamii inayozunguka.

Alisema mwaka jana wametoa elimu kwa vijiji 90, wamepata matokeo chanya kutokana na vijiji kuwa na uwelewa wa hawalimi au kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya hifadhi.

"Mkakati wa kutumia elimu unasaidia kwa kiasi kikubwa hivyo tunaendelea nao mwaka ujao ili kuhakikisha kila kijiji kilicho karibu na hifadhi ya misitu wanakuwa na elimu ya utunzaji wa hifadhi ya misitu na ardhi," alisema Profesa Silayo.

Alisema lengo ni kuona hifadhi zilizopo maeneo ya jirani na vijiji yanakuwa salama kwa ajili ya kuleta maendeleo mbalimbali katika eneo husika na taifa kwa ujumla.

Akizungumzia kuhusu kuimarisha ulinzi, Profesa Silayo alisema wana boti kubwa tano zenye uwezo wa kwenda kina kirefu cha maji kwa ajili ya kukabiliana na wahalifu wa hifadhi za misitu wanapobainika na kutaka kutoroka.

Alisema boti hizo zinafanya kazi katika maji ya bahari kuu, Mtwara, Lindi, Rufiji na Nkinga mkoani Tanga, boti hizo hufanya kazi za kuangalia wahalifu wa hifadhi za misitu.

Hata hivyo, alisema wana boti mbili ambazo hufanya kazi katika Ziwa Victoria, ni kuhakikisha hifadhi za misitu zinakuwa salama katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"TFS, imejipanga mwakani kuendeleza mkakati wa kulinda hifadhi za misitu zisiharibiwe," alisema Profesa Silayo.

Alifafanua kuwa wameimarisha usafiri katika wilaya mbalimbali kwa watumishi wao lengo ikiwa ni kuhakikisha misitu na hifadhi zake zinakuwa salama.

Alisema pia wameweka mipango mizuri ya usimamizi na kila mahali imeboreshwa na itaendeshwa chini ya mfumo uliopangwa.

Hata hivyo, alisema wana imani mwaka ujao eneo la hifadhi ya misitu litakuwa salama na kuitaka jamii kutoa ushirikiano pale wanapoona misitu inaharibiwa na watu wasiowema.



Wananchi wa Kijiji cha Chipogolo, Wilaya ya Mpwapwa, wakiondoa miti iliyoziba kwenye madaraja yanayodaiwa kuwa ni madogo na kushindwa kupita maji kwa uhuru, yaliyopo kati ya barabara ya Dodoma na Iringa eneo la vitongoji vya Maendeleo na Mkombozi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Ataka kingo za madaraja kuongezwa

Na Peter Mkwavila, MPWAPWA

MWENYEKITI wa Kijiji cha Chipogolo wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, Sophia Chindole, ameiomba serikali kuchukua hatua za haraka za kuongeza kingo za madaraja yaliyopo kati ya kitongoji cha Maendeleo na Mkombozi kwenye eneo la Barabara ya Dodoma na Iringa ili kunusuru maisha ya wakazi wa eneo hilo.

Alisema kuwa ikiwa serikali haitachukua hatua hiyo ya kuongeza kingo kwenye madaraja hayo kuna uwezekano mkubwa wa kutokea kwa maafa ya mafuriko katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha kwa kuwa maji yanapita juu ya daraja na kusambaa hadi kwenye makazi ya wananchi.

Alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye eneo hilo la madaraja hayo kijijini hapo.

"Barabara hii inatoka Dodoma hadi Iringa katika eneo hili la Chipogolo wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma, tupo hatarini kukumbwa na mafuriko kutokana na haya madaraja kuwa madogo, hivyo tunaiomba serikali yetu sikivu kuyaangalia kwa jicho la pili," alisema.

Alisema madaraja hayo ni madogo yanashindwa kuhimili upitishaji wa maji kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha, hivyo wanaomba kingo hizo kuongezwa ili kuepukana na adha hiyo ya mafuriko.

Naye mkazi wa kitongoji cha Maendeleo, Elia Mahalanah (70), amemwomba Rais John Magufuli, kuiagiza Wizara ya Ujenzi kupanua kingo za madaraja ili kuepusha madhara.

Alisema madaraja hayo yatasababisha maafa wakati wowote katika kipindi cha mvua zinazoendelea kunyesha kutokana na maji hayo kusomba miti na kuziba midomo ya madaraja hayo.

Kwa upande wake David Maduma, alisema madaraja hayo yana kingo ndogo zinazosababisha maji kushindwa kupita kutokana na kujazwa na miti ambayo inasombwa na maji.

Maduma alisema ni kawaida kwa madaraja hayo kujaa maji kipindi cha masika, lakini imekuwa kimya kwa mamlaka husika pamoja na kuwa viongozi wengi wanaitumia njia barabara hiyo.

# Moto wateketeza vibanda vya machinga

Na Peter Mkwavila, DODOMA

ZAIDI ya vibanda 25 vya wafanyabiashara wadogo (wamachinga) wanaofanya biashara katika soko la Sabasaba, jijini Dodoma vimeungua na moto unaodaiwa kuwa ni hitilafu ya umeme katika moja ya kibanda.

Wafanyabiashara hao walisema moto huo ulianza kuwaka saa moja kasoro asubuhi na kuteketeza vibanda vya mamalishe, saluni, simu pamoja na vya nguo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao anayeuza simu, vifaa mbalimbali vya simu, pamoja na kufanya miamala ya pesa, Adam Makumburu, akizungumza na waandishi wa habari kwenye tukio hilo, alisema kuwa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lilichelewa kufika katika eneo la tukio na hivyo kusababisha vibanda hivyo 25, kuteketea.

Alisema kwa upande wake bidhaa zilizokuwa ndani ya kibanda chake ni za zaidi ya Sh. milioni 25 ambazo zimeteketea.

Naye Mwenyeti wa soko hilo, Edward Ndahani, alisema kuwa vibanda vilivyoteketea ni 25, kati ya vibanda zaidi ya 120 vilivyopo kwenye eneo hilo.

"Bado hatujajua thamani ya vitu vilivyokuwamo ndani ya vibanda hivyo kwa sababu tunaendelea kufanya tathmini, lakini kwa kifupi ni kuwa vilivyoungua ni vya saluni, mama lishe, vya kuuzia simu na vifaa vingine vya simu, nguo za mitumba na za dukani," alisema Ndahani.


Kwa upande wake Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, Gilbert Mvungi, alisema walipata taarifa za tukio hilo saa 12:48 asubuhi, lakini walishindwa kufika kwa wakati kwa kuwa gari lilikuwa uwanja wa ndege kwa ajili ya ndege iliyokuwa inapaa.

"Taarifa tulizipata mapema, lakini kulikuwa na uchelewaji kwa kuwa tulikuwa uwanja wa ndege na tuliondoka saa 1:33 baada ya ndege kupaa ili kuelekea eneo la tukio, na hii imesababishwa na kuwa na gari moja," alisema.

Mvungi alisema baada ya kufika eneo la tukio walifanikiwa kuzima moto kwenye vibanda 26 vilivyokuwa vinaungua na kuokoa vibanda vingine visiungue, hata hivyo changamoto kubwa waliyoipata ni utaratibu mbaya uliotumika kujenga kwa kuwa hakuna nafasi ya kutosha kuruhusu gari kuingia.

Kuhusu wao kushirikishwa katika ujenzi wa vibanda hivyo, alisema watu wa halmashauri ndio walitakiwa kusimamia ujenzi wa huo, na Zimamoto kazi yao ni kushirikishwa katika michoro ya majengo ili kutoa ushauri wa kitaalamu.

Alisema kitokana na changamoto hiyo wanatarajia kukutana na viongozi wa soko hilo ili kujadiliana namna ya kufanya ili kuepuka madhara yatayojitokeza baadaye.



HABARI ZANZIBAR

# Ramia ataka mitazamo mipya kiuchumi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, amewataka wajumbe wa Jukwaa la Bajeti na Uchumi kuibua mitazamo mipya ya kiuchumi ili kuimarisha bajeti ya serikali ya mwaka 2020-2021 kuwa bora na yenye tija kwa wananchi wake.

Aliyasema hayo wakati akifungua jukwaa hilo kwa watendaji wa mamlaka ya serikali za mitaa na wafanyakazi mbalimbali katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakili, Kikwajuni Mjini Unguja.

Alisema, ni vyema kuwa na mipango imara itakayoimarisha ukuaji wa uchumi na mapato ya nchi kwa dhamira ya kuongeza kasi ya miradi ya maendeleo.

Kadhalika alisema, Zanzibar bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uchumi wake, kuendelea kukua na kuhimiza uwajibikaji kwa watendaji katika sekta za umma na binafsi.

Hata hivyo, Balozi Ramia alisema Zanzibar imekuwa na vianzio vingi vya kukuza uchumi hivyo ni vyema kujipanga ili kusaidia wananchi.

Aliwataka washiriki hao kutoa mawazo yao vizuri katika jukwaa hilo ili malengo ya jukwaa yaweze kufikiwa.

Akiwasilisha mada kuhusu utekelezaji na mwelekeo wa bajeti ya serikali 2019-2021, Omar Mlenge, kutoka Wizara ya Fedha, alisema kwa mwaka 2020 serikali haitegemei kuongeza kodi.

Alizitaka taasisi za ukusanyaji kodi TRA na ZRB kusimamia kwa kina masuala ya kodi ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.




Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Jamala Taib, akikunjuwa kitambaa kuashiria uzinduzi wa shahada ya kwanza ya Uuguzi na Ukunga katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) Shule ya Afya na Sayansi za Tiba, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa chuoni hapo, kampasi ya Vuga Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Taasisi zatakiwa kutekeleza majukumu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

TASISISI za kupinga na kupambana na vitendo vya udhalilishaji nchini kwa kushirikiana na vyombo vya kusimamia sheria Mkoa wa Kusini Unguja, zimetakiwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu ili waathirika wa matukio hayo waweze kupata haki yao.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, wakati akifungua mkutano wa kutathmini mpango mkakati wa utekelezaji wa hifadhi ya mtoto kwa kipindi cha miezi sita kupitia mradi wa Unicef uliowashirikisha maofisa kutoka katika taasisi mbalimbali za mkoa.

Alisema umoja, ushirikiano na uadilifu wa taasisi hizo ndio njia pekee itakayowezesha kupiga hatua ya kupunguza na kuondoa vitendo hivyo kwa kuwa vinasababisha kuathiri mila, silka na desturi za taifa.

Aliwataka watendaji hao kuhakikisha kila mmoja anawajibika kwa nafasi yake ili kuondoa malalamiko kwa wananchi.

Alisema serikali itachukua juhudi za kuzitafutilia kesi hizo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizobainika katika tathmini ya kikao hicho ambazo zinasababisha kukwamisha mwenendo mzima wa kesi za vitendo hivyo.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuachana na muhali kwa kutokuvifumbia macho vitendo hivyo na badala yake waendelee kusimama imara katika kutoa ushahidi wa kesi hizo zinapofika mahakamani ili kuisaidia mahakama kutoa hukumu kwa mujibu wa sheria.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa masuala ya udhalilishaji Mkuu wa Dawati la Kijinsia mkoani humo, Ali Mohamed Othman, alisema jumla ya makosa 81 ya vitendo vya udhalilishaji yameripotiwa kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai hadi Desemba katika vituo mbalimbali vya polisi yakiwamo makosa ya kubaka (45), kutorosha (18), kulawiti (9), kukashifiwa (6) na kujaribu kutaka kubaka (3).

Naye ofisa kutoka ofisi ya Mahakama ya Mkoa Mwera, Khamis Haji Simai na Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkoa wa Kusini, Mohammed Kassim Hassan, kwa pamoja walisema kuwapo kwa usiri katika jamii.

Aliitaka jamii kuwa tayari kutoa ushahidi na kuachana kufuta kesi kwa hiari na kucheleweshwa kwa majalada wakati wa kupelekwa na kurudishwa makamani kwa baadhi ya askari polisi ni miongoni mwa changamoto zinazochangia kurudisha nyuma juhudi za kuzipatia uamuzi wa haraka kesi hizo.

# UWT waaswa ushirikiano kuimarisha chama

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Chumbuni, Miraji Khamis Kwanza, amewataka kinamama wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Wilaya ya Amani Unguja, kuwa na ushirikiano katika kukiimarisha chama ili kiweze kupata ushindi ifikapo 2020.

Aliyasema hayo alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la UWT Wilaya ya Amani na kuwataka kuzidisha ushirikiano kwa lengo la kukiimarisha Chama Cha Mapinduzi.

Alisema hivi sasa wakati wa daftari la kudumu umeshafika, hivyo kinamama wasimame kuhamasisha kwenda kujiorodhesha na pia kuwahimiza vijana waliofikia umri wa miaka 18 kwenda kujiandikisha ili waweze kupiga kura.

Alisema daftari linahitaji kuimarishwa kuhamasishwa na kutiwa hamasa na kinamama wa UWT ndio viongozi wasimamizi wa mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uhamasishaji wanachama kwenda kujiandikisha kwa wingi bila ya kufanya ajizi.

"Daftari limeshafika tuitumie fursa kwa ujiandikisha kwa kila mwenye sifa na vijana wetu tuwahimize kwa kila aliyefikia umri," alisema.

Alisema ili nchi iweze kupata maendeleo zaidi na amani na utulivu iweze kudumu ni lazima kuhakikisha chama kinapata ushindi wa kishindo na historia ya nchi ni kuidumisha amani iliyopo ambayo ni hazina kubwa kwa chama na wananchi wake.

Aliwataka kinamama kukaa na kujitathmini kwa kujua wapi walipotoka na wanakokwenda na kuona jinsi nchi ilivyoweza kupiga hatua na kupata mafanikio makubwa kwa kusimamia Chama Cha Mapinduzi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Amani, Fatma Hamrani, aliwataka kinamama kuliongoza gurudumu la maendeleo hadi kulifikisha ukingoni kwa usalama na kupiga kura kwa amani na kudumisha ushirikiano uliokuwapo.

Naye Katibu wa UWT Wilaya ya Amani, Asha Mzee Omar, akisoma taarifa ya utendaji wa kazi za UWT kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, alisema uhai wa chama ndani ya wilaya hiyo imezidi kuimarika zaidi kwa kuongeza wanachama wapya 1,454, zamani walikuwa 3,573 na kufikia 5,027.

Alisema kwa upande wa siasa Wilaya ya Amani ni nzuri wanachama na wananchi wanaendelea kufanya kazi na mambo mengine ya kujitafutia maisha bila bughudha.

Alieleza kuwa wanachama na wananchi wa Wilaya ya Amani wanampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM, Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuleta maendeleo makubwa ya kiuchumi, miundombinu, huduma za kijamii, amani na utulivu katika uongozi wake wa miaka tisa ndani ya Zanzibar.

# Amcos zaagizwa kujipanga upya

**Na Stevie Chindiye, TUNDURU**

SERIKALI imewataka wajumbe wa bodi za vyama vya ushirika vya mazao vya Nakatete Amcos na Nalule Amcos kujipanga kwa ajili ya kuanza kutekeleza shughuli za wakulima wa vyama vyao, ili kuendana na shughuli za kusimamia upimaji wa korosho za wakulima na kushughulikia malipo yao.

Maelekezo hayo yametolewa na Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Tunduru, Goerge Bisani, kufuatia vyama hivyo kukosa waandishi wapya ambao walitakiwa kufanya shughuli za vyama hivyo baada ya waandishi wa awali kutumbuliwa na Mkuu wa Wilaya katika kikao kilichoketi Desemba 23, mwaka huu.

Alisema hali hiyo imetokana na kuwapo kwa mgomo baridi kwa vijana ambao walionekana kuwa na sifa katika vijiji hivyo kugoma kufanya shughuli hiyo majina yao yalipopendekezwa kupitia vikao vya Amcos hizo.

Akifafanua taarifa hiyo, Besani alisema kuwa ili kutekeleza maagizo yaliyotolewa katika kikao hicho tayari ofisi yake imefanya usimamizi wa Amcos nyingine tano ambazo zimepata watendaji wapya 10 ambao ni waandishi wakuu na wasaidizi wao, na wakeshakamilisha taratibu zote na kuanza kazi mara moja.

Kuhusu viongozi wa Chama Kikuu Tamcu waliotumbuliwa katika kikao hicho, Bisani alisema kuwa mchakato wa kuchuja majina watumishi wa kujaza nafasi hizo unaendelea kwa umakini mkubwa ili kuepusha matukio yaliyojitokeza nyuma.

Vyama ambavyo watumishi wake walitumbuliwa ni Mlimi Amcos, Chiliwena Amcos, Mshikamano Amcos, Namsosa Amcos, Nguvumali Amcos pamoja na Mwenyekiti wa Mlingoti Magharibi.

# Waitara aonya viongozi upinzani

**Na Happy Severine, SIMIYU**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mwita Waitara, amewaonya viongozi na wanachama wa vyama vya upinzani, watakaokwamisha utendaji wa viongozi wa serikali za mitaa kutokana na kususia uchaguzi uliofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Waitara alisema hayo wilayani Maswa mkoani Simiyu, wakati akizungumza na viongozi mbalimbali, ikiwa ni sehemu ya ziara ya siku moja wilayani humo.

Alisema uchaguzi wa Serikali za Mitaa umekwisha, hivyo ni vizuri viongozi wote waliochaguliwa ambao wanatokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakajiamini kwa kufanya kazi kwa sababu waliapishwa kisheria.

"Uchaguzi umeshamalizika, ninyi ndiyo viongozi mliochaguliwa ama kupita bila kupingwa, nyote humu mnatokana na CCM, mjiamini mlishakula kiapo cha kutumikia nafasi zenu fanyeni kazi zenu kwa uhuru kwa kufuata sheria kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi," alisema.

Alisema wachape kazi licha ya kuwapo matamko mbalimbali kutoka kwa vyama vya upinzani kutowapa ushirikiano kwa kile walichodai hakuwakupata ridhaa ya kuchaguliwa na wananchi na kuwataka wayapuuze.

"Kuna chama kimoja cha upinzani hivi karibuni kimefanya uchaguzi wake na kutoa matamko mbalimbali ya kutowatambua viongozi wote waliochaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa, niwahakikishieni msitishwe, ninyi pigeni kazi kwani mnalindwa na sheria zilizoko katika nchi hii," alisema.

"Na kupitia mkutano huu, niwaagize wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuwashughulikia kisheria watu wote wakataokwamisha utendaji wa viongozi wa serikali za mitaa," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, Efreim Lema, alisema tangu viongozi hao wachaguliwe wamekuwa mstari wa mbele kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo kama ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akipata maelezo kutoka kwa mjasiriamali, Maiko Nalimi, baada ya kufungua rasmi Tamasha la Utalii wa Lamadi lililozinduliwa jana na Naibu Waziri huyo, katika Wilaya ya Busega mkoani Simiyu.

# Kongamano utawala bora laibua mazito

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar, Yakout Hassan Yakout, amesema, kila mwananchi kwa nafasi yake ana wajibu wa kudumisha na kuimarisha utawala bora, ili kufikia maendeleo yaliyokusudiwa na serikali.

Akizungumza wakati akifungua Kongamano la Utawala Bora Wete Pemba, alisema iwapo utawala bora utaimarishwa, amani itaendelea kudumu katika jamii.

Alisema wananchi wana mchango mkubwa katika kuimarisha utawala bora, hivyo zinahitajika nguvu za pamoja ili kufikia maendeleo endelevu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Seif Shaaba Mwinyi, aliwataka wananchi wa Zanzibar kuwa wazalendo ili kujiletea maendeleo.

"Serikali imeshaandaa rasimu ya dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2030, hivyo tunatakiwa tutunze na kuheshimu miradi na shughuli za maendeleo," alieleza Mwinyi. Naye Katibu wa Tume ya Maadili Zanzibar, Asma Jidawi, aliwataka wananchi kuimarisha maadili, ili kupata utumishi uliotukuka, hivyo kila mwananchi kwa nafasi yake ana wajibu wa kulitekeleza hilo.

"Maandalizi huanza nyumbani, hivyo tutakapoimarisha maadili pia tutadumisha utawala bora katika nchi," alisema.

Akiwasilisha mada ya majukumu ya kijamii, Mjumbe wa Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Ali Ahmed Uki, alitaja majukumu ya kijamii katika utawala bora kuwa ni kushiriki katika mambo ya nchi moja kwa moja au kupitia uwakilishi, sheria kutekelezwa bila upendeleo na kufikia muafaka kwa maslahi bora ya jamii.

"Majukumu mengine ni ufanisi mzuri upatikane kwa mujibu wa maslahi ya jamii, taasisi za serikali, sekta binafsi na taasisi za kiraia ziwajibike kwa wadau pamoja na kutoa taarifa kwa jamii kwa uwazi," alisema.

Alisema kuna haja ya kuheshimiwa kwa misingi ya utawala bora husuan uwazi na uwajibikaji kwa maslahi ya jamii, kushirikiana baina ya serikali, wadau na jamii pamoja na kuweka mbele maslahi ya jamii.

Akiwasilisha mada ya utawala wa sheria, Dk. Sikujua Omar Hamdan Mhadhiri wa SUZA, alisema ili kudumisha utawala bora, ni vyema kuondoa muhali katika utekelezaji wa sheria, kuzipitia na kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria, kuielimisha jamii juu ya uwapo wa sheria mbalimbali na kuimarisha mfumo wa utoaji haki.

Naye Mkuu wa Idara ya Mikataba na Urejeshaji Mali kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), Nassir Ahmed Haji, alisema viongozi wana wajibu wa kusaidia na kuhamasisha mapambano dhidi ya rushwa katika maeneo yao, kukemea na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na kusimamia misingi ya utawala bora ukiwamo, uwazi, uwajibikaji na utawala wa sheria.

Akichangia, Suleiman Ali Said kutoka Wakfu na Mali ya Amana, alisema ili kuzuia rushwa ni vyema huduma zikatolewa kwa wakati na kwa anayestahili, jambo hilo litamsaidia wananchi kupata haki zao kwa urahisi.

"Tunasema kwanini itokee rushwa, ni kwa sababu baadhi ya huduma za kijamii hazitolewi kwa urahisi ama zinazoroteshwa, hivyo mwananchi huona atoe rushwa, ili apate huduma kwa haraka, hali hii iwapo itaendelea ni viguvu kuondosha rushwa," alisema.

Wakili wa kujitegemea, Abdul-karim Mussa Said, alieleza serikali imeweka sheria na mfumo mzuri, ingawa shida ipo watekeleza, jambo ambalo linawapa wakati mgumu wananchi na kushindwa kusema kwa kuogopa kukoseshwa kile anachokihitaji. Naye Suleiman Nassor kutoka Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu iliyopo Mkanjuni Chakechake, alisema utawala bora haujawapa haki watu wenye ulemavu, kwani wanashuhudia baadhi ya majengo ya kisasa, sio rafiki kwa watu hao, na wanashindwa kuzifikia huduma wanazostahili.

HABARI KIMATAIFA

## Ndege za Marekani zashambulia magaidi

**WASHINGTON,** Marekani

NDEGE za Jeshi la Marekani zimetekeleza mashambulizi ya anga dhidi ya ngome za kundi moja la wanamgambo wenye mafungamano na serikali ya Tehran, na kuua wapiganaji kadhaa.

Operesheni hii inakuja siku mbili baada ya shambulio la roketi ambalo lilimuua kwa mara ya kwanza raia mmoja wa Marekani nchini Iraq.

Jeshi la Marekani, limesema siku ya Jumapili liliendesha mashambulizi ya anga dhidi ya ngome tano za kundi la Hezbollah lenye mafungamano na Iran.

Mashambulizi hayo yaliyotekelezwa kufuatia mashambulizi ya mara kwa mara ya kundi la Kataëb Hezbollah dhidi ya kambi za jeshi za Iraq zinazokaliwa na vikosi vya operesheni ya kupambana dhidi kundi hilo.

Uthibitisho huo umetolewa na msemaji wa Pentagon Jonathan Hoffman. **RFI**

# Mji Syria wakaliwa na idadi kubwa ya paka kuliko watu

**DAMASCUS,** Syria

BAADA ya miezi kadhaa ya mashambulio ya mabomu kutoka kwa vikosi vya Syria na Urusi, mji wa Kafr Nabl nchini Syria, sasa umesalia kuwa makazi ya paka kuliko idadi ya watu.

Watu wachache waliosalia katika mji huo, ulioliplipuliwa na mabomu huwa wanajiliwaza na mamia ya paka.

Kulingana na uchunguzi wa BBC, baadhi ya raia hujificha chini ya kifusi cha nyumba zilizobomolewa ili kujikinga dhidi ya mabomu yanayodondoshwa kutoka angani.

Mmoja wao ni Salah Jaar mwenye umri wa miaka 32, anakaa katika jengo lilosambaratishwa na mabomu, lakini kila siku anazungukwa na mamia ya paka ambao wameachwa na wamiliki wao.

"Unafarijika paka akiwa karibu nawe," alisema na kuendelea "Zinafanya tusahau milipuko ya mabomu, kuporomoka kwa majengo, mateso, na uwoga."

Mji wa Kafr Nabl, wakati mmoja ulikuwa na watu 40,000, lakini sasa ni watu chini ya 100 waliosalia.

Ni vigumu kubaini ni paka wangapi waliopo hapo, lakini ni mamia na uhenda wamefikia maelfu.

"Watu wengi wamehama mji wa Kafr Nabl hali iliyofanya idadi ya watu kuwa ndogo sana. Kwa kuwa paka wanahitaji watu wakuwatunza kuwapa maji na chakula, wamehamia katika nyumba za watu walioamua kubaki katika mji huo. Kila nyumba ina karibu paka 15, au hata zaidi," Salah alisema.

**Wakati mwingine tunapotembea njiani tunaweza kupatana na paka 20 au 30 wanaoandamana na sisi kila tunapoenda. Na baadhi yao walitufuata hadi nyumbani.**

Salah bado anafanya kazi ya uandishi habari katika kituo cha radio cha Fresh FM, japo studio za kituo hicho zilibomolewa katika mashambulizi ya angani ya hivi karibuni.

Walikuwa na bahati shughuli za kituo hicho zilihamishiwa mji ulio karibu kutokana na sababu za kiusalama, muda mfupi kabla ya mashambulio hayo.

Kituo hicho ambacho huwatangazia watu kuhusu kitisho cha mashambulio kupitia habari na vipindi vingine kilipata umaarufu kutokana na paka.

Makumi kati ya paka hao walifanya ofisi za kituo hicho kuwa makazi yao. Mwasisi wa kituo hicho na mwanaharakati, Raed Fares, aliyeuawa na wanamgambo wa Kiislam wenye silaha mwezi Novemba 2018, alitenga fedha za kuwanunulia maziwa na chakula.

"Paka wengi walizaliwa katika jengo hilo. Mmoja wao aliyekuwa na rangi nyeupe na madoa ya hudhurungi alimpenda sana Raed.

Anapoondoka katika mabaki ya iliyokuwa nyumba yake, anakaribishwa na sauti za paka kutoka kila upande, Hili humfanyikia kila mtu, anasema.

"Wakati mwingine tunapotembea njiani tunaweza kupatana na paka 20 au 30 wanaoandamana na sisi kila tunapoenda. Na baadhi yao walitufuata hadi nyumbani." aliongeza kusema.

Giza linapoingia milio ya mbwa wasio na wenyewe husikika kutoka kila upande wa mji huo. Wapo wenye njaa na hawana pakwenda. Hali ya kupigania mabaki ya chakula na mahali pa kulala inawafanya kushindana na paka wa Kafr Nabl.

Wengi wao walikuwa wanapendwa na familia zilizotoroka mji huo, baada ya vikosi vya utawala wa Syria, kuanzisha operesheni ya kuukomboa mji wa Idlib Aprili iliyopita.

Sasa baada ya kukosa wa kuwatunza na kuwapa chakula cha mara kwa mara, wamelazimika kutafuta makazi mapya chini ya kifusi cha majengo yaliyoporomoka.

Na japo watu kama Salah hawana matumaini ya kuishi, bila kujua chakula kinatoka wapi, wanajiliwaza na paka hao ambao wamegeuka kuwa marafiki wa dhati.

"Kila ninapokula, nao hula, iwe ni maboga, spageti au hata mkate uliokauka. Katika hali hii nahisi sote ni viumbe wadhaifu na tunahitaji kusaidiana," alisena. **BBC**



Manuari ya kivita ya Jeshi la Urusi ikifanya mazoezi yalioshirikisha nchi za China na Iran katika Bahari ya Oman hivi karibuni. **PICHA: AFP**

# Libya yakana kusaidiwa na Uturuki

**ANKARA,** Uturuki

SERIKALI ya Libya iliyopo mjini Tripoli, inayoungwa mkono na Umoja wa Mataifa, imekanusha kuwa inasaidiwa na kikosi cha waasi wa Syria wanaoungwa mkono na Uturuki

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki ametahadharisha kwamba mgogoro wa nchini Libya, unaweza kutumbukia katika vurumai inayoweza kugeuka Syria nyingine. Waziri huyo Mevlut Cavusoglu, alisema hayo wakati akifanya juhudi kwa lengo la kupitisha sheria ya kuiwezesha nchi yake kupeleka wanajeshi nchini Libya.

Serikali ya Libya imekuwa inakabiliana na majeshi ya Jenerali muasi, Khalifa Haftar, yanayoungwa mkono na Urusi, Misri, Umoja wa Falme za Kiarabu na Jordan.

Waziri Cavusoglu, amesema ikiwa Libya itageuka kuwa Syria nyingine na nchi zote za kanda zitaathirika.

Waziri huyo alisema hayo alipokuwa anahutubia mkutano wa chama tawala nchini Uturuki AKP.

Alisema inapasa kufanya kila linalowezekana kuepusha vurumai na kugawanyika kwa Libya.

Alieleza kuwa hicho ndicho hasa kinachofanywa na nchi yake Uturuki. Ametamka kuwa Uturuki inashirikiana na serikali halali ya nchini Libya.

Majeshi ya Haftar, mpaka sasa bado hayajaweza kuingia mjini Tripoli, lakini taarifa zinasema vikosi vyake vimepata mafanikio ya kiasi fulani kusini mwa mji huo kutokana na msaada wa wapiganaji kutoka Urusi na Sudan.

Kwa mujibu wa taarifa za kidiplomasia, ndege zisizokuwa na rubani za Umoja wa Falme za Kiarabu zimesaidia kwenye mapigano hayo.

Ndege hizo zimemwezesha Jenerali Haftar kudhibiti vita vya angani kwa sababu ndege hizo zinadondosha mabomu mara nane zaidi kulinganisha na ndege zinazotumiwa na serikali halali ya Libya.

Wakati huo huo, serikali ya Libya imekanusha madai kwamba waasi wa Syria wanaoungwa mkono na Uturuki wanapigana bega kwa bega na wanajeshi wa serikali hiyo.

Tamko la kukanusha madai hayo limetolewa baada ya kinachodaiwa kuwa mkanda wa video uliowaonyesha waasi hao wakizungumza lahaja ya kiarabu cha Syria.

Jumamosi shirika linalofuatilia masuala ya haki za binadamu nchini Syria, lilidai kwamba waasi wa Syria wapatao 300 wanaoshirikiana na Uturuki waliwasili nchini Libya.

Shirika hilo lilisema wapiganaji hao wamekusanyika kwenye kambi ya serikali ya Libya kwenye sehemu hatari ya kusini mwa mji mkuu wa Libya, Tripoli. **DW**

# DMO awavaa watumishi wanaouzia damu wagonjwa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MGANGA Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Siha, Dk. Andrew Method, amewaonya watumishi wa idara ya afya wilayani humo, kutojaribu kuuza damu kwa wagonjwa, badala yake ametaka kila mtumishi kuheshimu maadili ya taaluma yake.

Dk. Method alitoa tahadhari hiyo jana wilayani hapa wakati akifunga kambi ya vijana wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) iliyokuwa katika Shule ya Sekondari Nuru, ambao pia walichangia utoaji wa damu.

"Hii damu inayotolewa hapa na ninyi vijana, sisi tunaitoa bure kwa wenye mahitaji kuongezewa damu wakati wanapopata matatizo au ajali.

"Sasa hata watumishi wangu huwa nikipata nafasi kama hii nawaonyaga kwamba wasije wakajaribu kuleta ujanja ujanja wa kupata pesa, kwa sababu sitosita kumchukulia hatua mfanyakazi yeyote wa hospitali au kituo cha afya atakayebainika kukiuka maadili ya kazi yake ikiwamo kuuza damu," alisema.

Katika kudhibiti tatizo hilo, Dk. Method aliwasisitiza wananchi kutoa taarifa kama kutakuwa na mtu atakayelazimishwa kutoa fedha ili kupewa damu.

Aidha, alisema wilaya hiyo kila mwaka ina lengo na kukusanya chupa 680 za damu kwa mwaka 2018 na 2019, mwitikio ulikuwa mzuri tofauti na miaka ya 2016 na 2017 ambayo ilikuwa na changamoto.

Kwa mujibu wa Dk. Method, kwa mwaka 2016 na 2017 walikusanya kati ya chupa 200 na 300 za damu tu kwa mwaka mzima.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alisema serikali imekuwa ikiimarisha miundombinu ya afya na kuipatia vitendea kazi sekta hiyo ili kutoa huduma bora za afya ya msingi kwa wananchi.

Naye Katibu wa UVCCM wa Wilaya ya Siha, Bulugu Magege, alisema kambi hiyo ilikuwa na vijana 105 kutoka wilayani humo kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ikiwamo uzalendo, kulipenda taifa na kulitetea na kutangaza mazuri yanayofanywa na serikali ya awamu ya tano.

# Viongozi watakiwa kuliombea taifa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

VIONGOZI wa dini nchini wameombwa kuombea amani taifa na watu wake ili kubarikiwa kwa kila jambo wanalolifanya na hatimaye kuongeza ufanisi na juhudi katika kukuza uchumi.

Pia viongozi hao wametakiwa kuliombea taifa na viongozi wake ili wapendane, kushirikiana na kuwa wamoja katika masuala mbalimbali ya ujenzi wa taifa.

Wito huo ulitolewa na Diwani wa Ngarenaro jijini Arusha, Isaya Doita, alipokuwa akizindua upandaji miti katika Zawiya Kuu ya Msikiti wa Zawiyatull Qadiriyyat ulioko katika kata hiyo. Alisema pamoja na kuwaombea viongozi hao, pia wanapaswa kuwakosoa na kuwahusia ili wawe na maadili mema katika utendaji wao wa kazi.

Doita alisema anawaheshimu viongozi wa dini zote na kusema atakuwa tayari kwa kila kazi yoyote atakayoitwa kuifanyana viongozi wa dini.

Naye mwenyekiti wa Zawiya hiyo, Mkoa wa Arusha, Abdi Omar, alisema wakiwa taasisi ya dini wanaungana na serikali kutunza na kuboresha mazingira ili kuifanya Arusha iwe ya kijani. Aliongeza kuwa katika mkoa wa Arusha kuna zaidi ya zawiya 30 na kwa kila moja wameadhimia kupanda miti 3,000 ili kuhakikisha wanatunza kingo za mito na kupunguza mmomonyoko wa ardhi.

Abdi alitanabaisha kuwa katika kufanikisha lengo hilo, taasisi hiyo ilipata ufadhili wa fedha kutoka Shirika la Hifadhi la Taifa (Tanapa) ambalo liliwachangia Sh. milioni 10.

Kwa upande wake, mlezi wa zawiya hiyo, Salim Mbaraka, maarufu kama Mtimkavu, aliwataka watu wote kuishi na watu wote wakiwa na tabia njema ambayo ndiyo silaha kwa kila jambo.



Askofu Mkuu wa Makanisa ya Abundant Blessing Centre (ABC), Flaston Ndabila (wa pili kushoto), akikabidhi vifaa vya shule kwa mwanafunzi wa kidato cha pili wa Shule ya Sekondari Zawadi, Irene Raina (wa tano kutoka kushoto), vilivyotolewa na kanisa hilo kwa wanafunzi wasiojiweza na yatima jijini Dar es Salaam juzi. Wa kwanza kushoto ni mfadhili wa msaada huo, Fanuel Leonard na wa tatu ni mke wa Askofu, Janeth Ndabila. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Aomba msaada kupata baiskeli

**Na Beatrice Moses**

WAZAZI wa Munira Rashid (12), mwenye ulemavu, wakazi wa Saranga, wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam wamekwama kugharamia kipimo cha CT- Scan na kumnunulia baiskeli maalumu na kulazimika kuomba msaada kutoka kwa wasamaria wema kuwasaidia.

Akizungumza na Nipashe, mama mzazi wa mtoto huyo, Sakina Sadick, alisema familia imekuwa katika wakati mgumu kumhudumia kutokana na kutokuwa na kipato kinachojitosheleza.

"Naomba wasamaria wema wajitokeze kumsaidia mwanangu apate huduma ya tiba ya kipimo hicho ili atibiwe macho, tumesota huu ni mwaka wa pili sasa tangu alipoandikiwa kupimwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, tumekwama gharama za malipo," alisema.

Sakina alisema kuwa awali walijitahidi kutafuta fedha hizo ambazo zilikuwa ni Sh. 160,000 wakapata nusu yake, (Sh. 80,000) ambazo baada ya muda walijikuta wanazitumia kwa mahitaji mengine baada ya kukwama kupata za kuongezea.

"Mwanangu Munira nilimzaa mwaka 2008 akiwa mzima, lakini baada ya miezi minne ndipo nikabaini jambo la tofauti mwilini mwake, kichwa kilianza kuwa kikubwa kwa kasi, tukampeleka CCBRT na alitibiwa na kufanyiwa upasuaji mara mbili, lakini bado hakurejea katika hali ya kawaida," alisema Sakina.

Alibainisha kuwa Munira ambaye awali alikuwa anaona aliugua homa kali akiwa na umri wa miaka tisa na kulazwa Hospitali ya Mwananyamala, baada ya hapo alianza kupoteza uwezo wa kuona hadi sasa, ndipo akatakiwa kupiwa CT-Scan kwa uchunguzi utakaowezesha kupata matibabu.

Alisema wamewahi kujiandikisha kwenye mfuko wa mpango wa kunusuru kaya maskini Tanzania (Tasaf), lakini hawakupata msaada.

Munira ambaye ana uwezo mzuri wa kujieleza alisema kuwa anatamani kusoma, lakini hawezi kutembea wala kuona kwa hiyo amekuwa akijifunza kuhesabu kwa kutumia visoda.

Rashid Abdallah baba mzazi wa mtoto huyo, alisema awali alikuwa akifanya kazi kwenye kituo cha mafuta, lakini walipunguzwa, hivyo amekuwa akitafuta kipato cha familia kwa kufanya vibarua ikiwamo vya kusaidia fundi kwenye ujenzi.

"Nimekwama mtoto wangu kwa sasa ni mkubwa kazi kumbeba, naamini tukisaidiwa baiskeli itasaidia kumhudumia, naomba wanajamii wenzangu wenye moyo wa kusaidia wajitokeze kutusaidia kwa kuwasiliana nasi kwa namba ***0654 728106***," alisema Abdallah.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, alisema kaya hiyo inahitaji msaada, akibainisha kuwa alijiandikisha Tasaf, lakini katika hali ya kushangaza aliondolewa ikielezwa kuwa wanasaidia watoto wanaosoma.



Sakina Sadick akimhudumia mwanawe Munira Rashid ambaye ni mlemavu anayehitaji msaada. **PICHA: BEATRICE MOSES**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**HAPPINESS ANTONY MAYALA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0989-0013** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIBARA Sekondari mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KBR//RB/464/2018.**

115569002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SIADI MOHAMEDI SIMBA**
P.O.BOX 447 DODOMA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili **T 678 CRT.** Chassis namba **04335310.** Engine namba **4016103.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/TR/3346/2019**

115569502

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MC A/63)**

**Mahakama ya mwanzo ya MBALIZI**

**Wilaya ya MBEYA**

**MIRATHI NAMBARI: 06...YA..2013**

**MPINGAJI................BENDANA APOLLO MAHAY**
**MAREHEMU........ANJELINA FERDINAND MASHAURI**

**KWA: APOLINARI CHRISTIAN MAHAY**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**JUU YA KUPINGA KUSIMAMIA MIRATHI**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya...ALHAMISI...tarehe...02/01/2019...saa...2:30...ASUBUHI. Kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mshauri wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Lakiri yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe...18/12/2019.

HAKIMU MAAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
MBALIZI - MBEYA

115569602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo: Mjini Tanga**

**Usimaminzi wa Mirathi. Namba 174/2019**

**Ombi la Isaya Solomoni Samweli**
**Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Hilgath Solomoni Mdime**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na husiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17l01l2020. kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa miathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 18l12l2019

Sahihi ya Hakimu
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

115569402

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
27/12/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano tarehe 28/12/2019** Kampuni ya **Mussa holdings** itapitisha gari lenye vipimo vya tofauti kutoka Moshi kuelekea Same, Kutoka Same Kurudi Moshi. Gari lenye namba za usajili **T277ALQ.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-
   **Urefu - 9.7**
   **Upana - 3.0**
   **Kimo - 3.0**

3. Njia itakayotumika ni Same kupitia Mwanga –Moshi gari litasafiri muda wa kuanzia saa 12:00Asubuhi

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115569302

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# RONALDO ASHINDA TUZO YA SITA DUBAI



**DUBAI,** Falme za Kiarabu

CRISTIANO Ronaldo amemaliza mwaka 2019 kwa kushinda tuzo ya mwanasoka bora wa kiume wa Dubai Globe Soccer.

Ronaldo, ambaye alikuwa wa tatu kwenye tuzo za Ballon d'Or mwaka huu akiwa nyuma ya Virgil van Dijk na mshindi Lionel Messi, sasa ameshinda tuzo hiyo kwa mara ya sita kwa kipindi cha miaka tisa tangu kuanzishwa kwake.

Pia ameitwaa tuzo hiyo kwa mara ya nne mfululizo kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye aliisaidia Juventus kutwaa taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu wa 2018-19 likiwa ni la kwanza tangu kuanza kucheza soka nchini humo na pia alikuwa nguzo ya Ureno kubeba ubingwa wa Ligi ya Mataifa ya Uefa.

"Napenda kuishukuru familia yangu, mpenzi wangu, kijana wangu, Cristiano, watoto wangu watatu ambao wananisubiria hotelini, marafiki zangu, wachezaji wenzangu wa Juventus na timu ya taifa, na watu wote waliopo hapa, nashukuru kwa sapoti yenu," alisema Ronaldo, akiwaambia waandishi wa habari.

"Ningependa kuwashukuru nyie Jumuiya ya Kiarabu, ambao mmekuwa watu muhimu zaidi kwangu. Napenda kuishukuru Dubai pia na napenda mahali hapa, nakuja kila mwaka.

# Moyes amrithi Pellegrini West Ham

**LONDON,** England

DAVID Moyes ameteuliwa kuwa kocha wa West Ham kwa mara ya pili baada ya Manuel Pellegrini kufukuzwa.

Wagonga nyundo hao wa London wapo nafasi ya 17 kwenye Ligi Kuu, hali iliyosababisha Pellegrini kufukuzwa Jumamosi wakati wakifungwa 2-1 na Leicester City nyumbani.

Kocha huyo wa zamani wa Manchester City, Pellegrini alishindwa kupata matokeo mazuri licha ya kuwa na wachezaji wenye kipaji pale West Ham na sasa wanapigania kutoshuka daraja.

Na sasa wameamua kumrudisha Moyes, ambaye aliwaongoza vijana hao kutoka jijini London kuwa na msimu mzuri zaidi wa 2017-18.

Amesaini mkataba wa miezi 18 kuinoa West Ham kama ambavyo imetangaza kwenye tovuti yake.

Kocha huyo wa zamani wa Manchester United aliiwezesha West Ham kumaliza ligi ikiwa nafasi ya 13 kwa mara ya mwisho kuinoa timu hiyo, lakini mkataba wake wa muda mfupi haukuongezwa na Pellegrini aliteuliwa Mei mwaka 2018.

Moyes, ambaye pia amewahi kuzinoa kwa nyakati tofauti, Everton na Sunderland kwenye Ligi Kuu, alikuwa hana timu tangu alipoondoka kwenye dimba hilo la London.

Baada ya kutangazwa kurudi West Ham, Moyes alisema: "Ni jambo la kuvutia kurudi tena hapa. Najisikia kama niko nyumbani.

"Nilipamisi hapa kwa sababu kwa uhakika kabisa nilipokuwa hapa nilifurahia wakati wangu na sasa nafurahia kuwa tena sehemu ya klabu hii, hivyo nasubiri kuanza kazi."





# *Klopp: Tunaingia nusu ngumu zaidi*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amewaambia wachezaji wa Liverpool kutarajia nusu ya msimu mwingine wa kupambana baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Wolves katika Uwanja wa Anfield na kuwaweka kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England kwa tofauti ya pointi 13.

Bao la Sadio Mane lilitosha kuweka tofauti ya timu hizo mbili wakati Liverpool walipookolewa na Teknolojia ya Maamuzi kwa njia ya Video (VAR), iliyokataa bao la kusawazisha la Pedro Neto.

Wekundu hao wamecheza nusu ya mechi zake msimu huu na wanaonekana wanaelekea kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu msimu huu baada ya kipindi cha miaka 30, lakini Klopp amesema nusu ya msimu unakuja unaweza kuwa mgumu zaidi.

"Tunaingia nusu ya msimu sasa," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari. "Tuna mechi 19 za kucheza na pengine 18 au 19 zitakuwa kama mchezo wa leo (juzi), kwa sababu tofauti.

"Sasa tutakutana na timu ambazo zinapambana kwenye ligi kwa kila kitu walichonacho, halafu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Europa.

"Nani anajali kuhusu pointi za Desemba? Tumetengeneza msingi ambao utafanya kazi kuanzia leo na kuendelea."

# Haaland ashukuru kutua Dortmund

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland ameishukuru klabu ya Salzburg kwa kusaidia maendeleo yake na kuelezea "ni sehemu ya mazingira ya kuvutia zaidi" kujifunza, wakati akijiandaa kuendeleza kipindi chake cha uchezaji katika Klabu ya Borussia Dortmund.

Baada ya uvumi wa muda mrefu kuhusu majaliwa yake, huku akihusishwa na kutakiwa na klabu kama Juventus, Manchester United na RB Leipzig, mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Norway amekubali kujiunga na Dortmund kwa mkataba ambao utamueka hapo hadi msimu wa 2023-24.

Uhamisho huo unamaanisha kwamba, Haaland ametumia mwaka mmoja tu akiwa na Salzburg, ambapo aliweza kuchomoza na kung'ara Ulaya, ikiwamo kufunga mabao matano ikiwa ni mara yake ya kwanza kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Licha ya kuondoka, kinda huyo ameweka wazi kwamba mara zote ataangalia nyuma katika klabu hiyo ya Austria ambayo ilimsajili kutoka Molde.

"Usajili wangu kwenda Salzburg ulikuwa bora katika maisha yangu hadi sasa," alisema katika taarifa yake iliyochapishwa kwenye tovuti ya Salzburg.

"Mengi zaidi yametokea mwaka jana, ni ngumu kuamini. Nilikuwa na nafasi ya kujifunza mengi kwenye mazingira ya kuvutia na kwa muda mfupi. Kwa uhakika kabisa najisikia fahari kwa kila mtu aliyehusika klabuni hapa.

"Najisikia fahari kuwa sehemu ya timu hii na nawatakia kila mmoja pale Salzburg kuwa na msimu wenye mafanikio zaidi.

"Kwa upande wangu safari bado inaendelea hapa Borussia Dortmund, lakini mara zote nitaangalia nyuma pale Salzburg nikiwa na furaha."

Haaland atajiunga na wachezaji wenzake pale Dortmund Januari 3, wakati wa mapumziko mafupi ya Ligi Kuu ya Ujerumani.






# GUARDIOLA AMPIKU MOURINHO 100 EPL

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amempiku Jose Mourinho kuwa kocha aliyeshinda kwa uharaka zaidi mechi 100 za Ligi Kuu ya England.

Mabao kutoka kwa Sergio Aguero na Kevin De Bruyne yaliiwezesha City kupata ushindi wa 2-0 dhidi ya Sheffield United Jumapili, ingawa Teknolojia ya Maamuzi kwa njia ya Video (VAR), yalionekana kuleta utata.

VAR ililikataa bao la ufunguzi la Lys Mousset, huku mwamuzi Chris Kavanagh akionekana kuuzuia mpira wa John Fleck ambao ndio ulisababisha bao la Aguero dakika ya 52.

Ushindi huo ulimfanya Guardiola kufikisha mechi 100 alizoshinda kwenye Ligi Kuu kati ya 134 alizoiongoza City.

Wakati alipoulizwa kuhusu hilo kwenye mkutano wake na waandishi wa habari, Guardiola haraka aliwasifia wale wote wanaomzunguka.

"Ni zawadi kubwa kwa klabu, wachezaji na stafu wote kwa kupata ushindi wa 100," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni mafanikio ya kujivunia hasa kwa muunganiko huu na ni zawadi kubwa kwa wachezaji wote na uongozi wote waliohusika kwa kipindi hiki."

Kocha wa sasa Tottenham Spurs, Mourinho awali alikuwa akiishikilia rekodi hiyo, baada ya kushinda mechi 100 katika mechi 142, huku kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akiwa ameiongoza timu hiyo katika mechi 159 mapema mwezi huu.

# *Lampard: Jorginho ana bahati kuepuka nyekundu*

**LONDON,** England

FRANK Lampard amekubali Jorginho alikuwa na bahati kuepuka kadi ya pili ya njano kabla ya Chelsea kutoka nyuma na kupata ushindi wa 'usiku' dhidi ya Arsenal.


Mzaliwa huyo wa Brazil alinufaika na makosa ya golikipa wa Arsenal, Bernd Leno, akisawazisha bao la Pierre-Emerick Aubameyang la kipindi cha kwanza alilofunga kwa kichwa, baada ya yeye kufunga dakika ya 83 kabla ya Tammy Abraham kufunga la ushindi dakika tatu kabla ya mchezo kumalizika.

Jorginho, aliingia akitokea benchi dakika ya 34 wakati Lampard alipoamua kubadili mbinu baada ya Arsenal kutawala mchezo, alionyeshwa kadi ya njano kwa kumzuia Alexandre Lacazette dakika 55 wakati alipokuwa amechomoka kwenda kufanya shambulizi la kushtukiza, lakini aliepuka kadi ya pili kwa kumfanyia faulo Matteo Guendouzi dakika sita kabla ya kuisawazishia Chelsea.

"Alikuwa na bahati, pengine ingeweza kuwa kadi ya pili ya njano," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Katika 'dabi' ya London faulo nyingi zaidi zinatokea, nyingine zinatokea mapema kwenye mchezo na nyingine huwezi kupata kadi ya njano.

"Kwa uhakika kabisa tulikuwa na bahati, lakini kuna wakati mambo yanakuwa tofauti na tunatakiwa kukubali.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA KUMPAISHA LENO, AMZUIA XHAKA

## Ni wakati Arsenal ikirejea rekodi yake mbovu ya miaka 60, asema hataondoka Januari...

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameahidi kuinua moyo wa kujiamini kwa Bernd Leno baada ya makosa aliyofanya kipa huyo na kuigharimu Arsenal wakati ikilala 2-1 dhidi ya Chelsea, na kocha huyo mpya wa Gunners pia amesema anatumai kiungo Granit Xhaka atabaki katika klabu hiyo.

**Leno aliiruhusu krosi ya Mason Mount kumpita kabla ya Jorginho kuifungia Chelsea bao la kusawazisha katika Uwanja wa Emirates juzi, baada ya Pierre-Emerick Aubameyang kuifungia Arsenal bao la kuongoza lililowafanya kutawala kipindi cha kwanza.**

Arsenal ilivurunda dakika za mwisho, na Tammy Abraham kuifungia Chelsea bao la ushindi kwa mpira wa tobo uliompita Leno zikiwa ni dakika tatu kabla ya mechi kumalizika na kumhakikishia Arteta anakubali kipigo cha kwanza tangu atwae mikoba ya kuinoa timu hiyo.

Arteta alikiri kipigo kitaathiri kujiamini kwa Leno, lakini akawataka wachezaji wake kutazama mbele kuelekea mechi dhidi ya Manchester United siku ya Mwaka Mpya, kesho.

"Atakuwa chini, lakini tunapaswa kumuinua," Arteta alimzungumzia Leno. "Amekuwa kipaji kwa klabu hii ya soka.

"Nimesikitishwa sana na matokeo, jinsi tulivyoruhusu mabao na wakati. Nimefurahishwa na vitu vingi, lakini nimesikitishwa na kupoteza.

"Nadhani muundo ulikuwa mzuri. Tunahitaji kuthibiti hali hizo, lakini walikuwa wazuri katika kipindi cha mpito.

"Tunapashwa kuendelea."

Kuachwa kwa Xhaka kutoka kikosi cha kwanza cha Arteta kuliongezea uzito kwa tetesi za kiungo huyo raia wa Uswisi kujiunga na Hertha Berlin dirisha la usajili la Januari.

Arteta alisisitiza kuugua ndiko kulikochangia kufanya maamuzi hayo ya kutomchezesha, akiwaambia wanahabari: "Alianza kujisikia kuugua baada ya mechi dhidi ya Bournemouth.

"Natumai hataondoka Januari."

Kipigo hicho cha juzi, kinaifanya Arsenal kupata matokeo mabaya zaidi katika mechi za nyumbani kwa kipindi cha miaka 60 sasa.

Matokeo hayo, yanamaana 'Gunners' imepoteza mechi nne mfululizo nyumbani katika mashindano yote, na kwa mara ya mwisho kupoteza michezo minne mfululizo nyumbani ikiwa ni mwaka 1959.

Arteta atakuwa na matumaini ya kuhitimisha matokeo hayo na kupata ushindi wake wa kwanza atakapoikaribisha Manchester United kesho katika Uwanja wa Emirates.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YADUNDA EVERTON

ARSENAL, Newcastle United na Paris St-Germain zimeshindwa kuipata saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Brazil, Everton Soares, 23, kutoka Gremio. ***(Newcastle Chronicle)***

### HEE-CHAN KIMEELEWEKA

WOLVES inakaribia kuinasa saini ya mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Hwang Hee-chan, na ada ya pauni milioni 23 imekubalika kwa nyota huyo wa kimataifa wa Korea Kusini. ***(Hamburger Morgenpost, via Birmingham Mail)***

### HAALAND ATUA DORTMUND

MANCHESTER United ilitoa ofa kubwa kwa mshambuliaji wa Erling Braut Haaland, lakini Mnorway huyo mwenye umri wa miaka 19, amechagua kujiunga na Borussia Dortmund ili kujiendeleza. ***(Independent)***

### BONY KURUDI SWANS

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester City na Swansea, Wilfried Bony, 31, amesema anataka kurudi kujiunga na klabu hiyo ya Championship. ***(Telegraph)***

### CHELSEA, LAMPTEY WATETA

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema klabu hiyo ipo katika mazungumzo na beki wa kulia wa Tariq Lamptey, 19, kuhusu kusaini mkataba mpya, wakati huu wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu. ***(Goal)***

### LEMAR KUIGHARIMU ARSENAL

ARSENAL lazima watoe ofa ya kueleweka ili kuishawishi Atletico Madrid kumuuza Mfaransa Thomas Lemar, 24, katika dirisha la Januari. ***(AS, via Mirror)***

### MESSI KUMZUIA NEYMAR

BARCELONA itazingatia tu kumsajili kwa mara nyingine mshambuliaji wa Brazil, Neymar, 27, kama mbadala wa Lionel Messi, 32, wakati straika huyo Muargentina atakapoamua kuondoka klabuni hapo. ***(Sport)***

### UPAMECANO AWANIWA EPL

ARSENAL na Tottenham zinajiandaa kulipa pauni milioni 50 ili kumsajili beki wa kati wa RB Leipzig, Dayot Upamecano, 21, lakini itakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Manchester City. ***(Daily Star)***

### ATLETICO YAMSIKILIZIA CAVANI

ATLETICO Madrid inaweza kumfuata mshambuliaji wa Beijing Guoan, Cedric Bakambu, 28, katika dirisha la Januari kama haitaweza kumsajili chaguo lao la kwanza, Edinson Cavani, 32, kutoka Paris St-Germain. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### MADRID KUMZUIA RODRIGUEZ

REAL Madrid haitamruhusu kiungo Mcolombia, James Rodriguez, 28, kuondoka katika dirisha la Januari. ***(AS)***

### NEWCASTLE KUMFUNGA JONJO

NEWCASTLE inafanyia kazi mpango wa kuongeza mkataba wa kiungo Jonjo Shelvey, 27, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2021. ***(Chronicle)***

HABARI MICHEZO

## Azam wafunguka wakiifuata Singida

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema wamefanikiwa kuondoka na pointi tatu muhimu kutokana na wachezaji wake kupambana kwa kiwango kikubwa katika mchezo huo.

Cheche aliliambia gazeti hili jana kuwa kila mchezaji alionyesha kujituma katika mchezo huo, tofauti na ilivyokuwa katika mechi yao iliyopita.

Kocha huyo pia aliwapongeza wapinzani wao Polisi Tanzania kwa kucheza kwa kiwango bora na kusema kuwa hakuna mechi nyepesi katika Ligi Kuu Bara msimu huu.

"Tunawapongeza wachezaji wetu kwa hali ya mshikamano waliouonyesha, hii ndio ilisababisha kufanya vizuri, wamejitoa mwanzo hadi mwisho, tuliingia na ari ya kupambana, kiukweli ukomavu ndio umetusaidia," alisema Cheche.

Aliongeza kuwa kikosi chake kilitarajiwa kuondoka Moshi jana na kuelekea mkoani Singida kwa ajili ya kujiandaa kuwavaa wenyeji wao Singida United katika mchezo utakaofanyika kesho kwenye Uwanja wa Lenti zamani Namfua.

## Ligi ya U-21 Z'bar yasogezwa mbele

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesogeza mbele Ligi ya Vijana ya umri chini ya miaka 21, ili kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Januari 5, mwakani.

Hata hivyo, ZFF imeshindwa kutaja tarehe mpya ambayo ligi hiyo itaendelea.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada, alisema wameamua kuchukua uamuzi huo kutokana na kuwapo kwa changamoto ya viwanja kwa ajili ya kutumia kwenye ligi hiyo ya vijana.

"Kipindi hiki tuna uhaba wa viwanja, kuna michezo inayoshirikisha wafanyakazi wa wizara mbalimbali inayoendelea kwenye Uwanja wa Mao ikiwa ni kwa ajili ya kuelekea kwenye sherehe za Mapinduzi," alisema Ahmada.

Kiongozi huyo alisema wameshindwa pia kupeleka ligi hiyo kwenye Uwanja wa Amaan kwa sababu unafanyiwa matengenezo kwa ajili ya kuelekea sherehe za Mapinduzi hali inayosababisha Uwanja wa Mao kuwa na msongamano wa mechi mbalimbali.

Ligi hiyo ya vijana inashirikisha timu B za klabu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, ambayo huchezwa kila Jumamosi na Jumapili, kutokana na wachezaji wengi kuwa wanafunzi.

# NYOTA WA YANGA IKIIVAA SIMBA KUPEWA GODORO

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga itakayochezwa Jumamosi, Kampuni ya GSM Group, ambao ni moja ya wadhamini wa Yanga inatarajia kutoa zawadi ya godoro kwa mchezaji wa klabu hiyo atakayeibuka nyota wa mchezo huo unaosubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka nchini.

**Mechi hiyo itakayowakutanisha kwa mara ya kwanza katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, itachezwa kwenye Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na jijini jana, Meneja Masoko na Mawasiliano wa GSM Group, Matina Nkurlu, alisema wameamua kutoa zawadi hiyo ili kuwapa morali wachezaji wa Yanga.

Nkurlu alisema wao kama wadhamini wa Yanga ni wajibu wao kuhakikisha timu hiyo inawapa raha mashabiki wake kwa kushinda mchezo huo ambao pia unafuatiliwa na mashabiki na wapenzi wa soka Ukanda wa Afrika Mashariki.

"Kuelekea mechi ya kukata na shoka kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga, moja ya wadhamini wakuu wa timu ya Yanga, GSM Group kupitia godoro chapa GSM, tutatoa zawadi nono kwa Mchezaji Bora wa timu ya Yanga wakati wa mechi [hiyo ya watani wa jadi] kwa kumzawadia godoro la nchi 5x6x8.

"Tunaamini zawadi hii itawaongezea wachezaji morali ya kupambana kuiwezesha Yanga kupata ushindi na hivyo kuwapa raha mashabiki wao na kuendelea kupata matokeo chanya kwa mechi zingine zijazo," alisema Nkurlu.

Aliongeza: "Yanga ni klabu kubwa na bora hapa nchini kama ilivyo kwa magodoro yetu, hivyo mashabiki wao nao wanastahili matokeo yaliyo bora uwanjani ndio maana tumeamua kutoa zawadi ili kuwapandisha mzuka wachezaji wa Yanga kuelekea mchezo huo muhimu wa Jumamosi."

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema anaishukuru GSM Group kwa ahadi hiyo ambayo anaamini itawaongezea hamasa wachezaji wa timu yao.

Mwakalebela alisema timu yao imejiandaa vema na mchezo huo, na anaamini kikosi chao kitaonyesha ubora wake dhidi ya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara.

KOSA...




Kosa alilolifanya kipa wa Arsenal, Bernd Leno (Juu), baada ya kuokosa mpira na kumfanya Jorginho kuisawazishia Chelsea katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Emirates na Gunners kulala 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# *Riadha kuchaguana Desemba mwakani*

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa mchezo wa riadha nchini wametakiwa kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), ambalo linatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu ifikapo Desemba 20, mwakani.

Akizungumza jijini Mwanza juzi, Mwenyekiti wa RT, Anthony Mtaka, alisema ili kuendeleza mchezo huo, chama kinahitaji kuwa na viongozi ambao wana malengo ya kuuendeleza mchezo huo kuanzia ngazi ya chini.

Mtaka alisema anaamini viongozi wenye mapenzi na mchezo huo ndio wanaosaidia kuharakisha mafanikio na maendeleo ya mchezo huo.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha wadau wote kuwa uchaguzi ujao utafanyika Desemba 20, mwakani na ninawakumbusha kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi mbalimbali katika chama hiki, tunahitaji viongozi wenye uwezo wa kupambana na changamoto zinazotukabili," alisema Mtaka.

Aliongeza kuwa amefurahishwa na maandalizi ya mashindano ya taifa mwaka huu na anaamini kupitia michuano mbalimbali, Tanzania itapata wanariadha watakaofikia viwango vya kushiriki Michezo ya Olimpiki mwakani.

Alisema pia maandalizi yanaendelea kwa wawakilishi wa Tanzania watakaokwenda kushiriki katika mashindano ya riadha ya vijana ya umri chini ya miaka 20 yatakayofanyika mapema mwakani jijini Nairobi, Kenya.

Michezo
Jumanne Desemba 31, 2019
Nipashe



Guardiola ampiku Mourinho 100 EPL

HABARI UK.29

MNISAMEHE...



Tariq Seif (aliyenyoosha mikono juu) kama ishara ya kuomba msamaha kwa mashabiki wa timu yake ya zamani, Biashara United baada ya kuifungia timu yake mpya ya Yanga, wakati timu hizo zilipokutana kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga yapangua gia msimamo Ligi Kuu

●●● Tariq aanza kwa bao, nafasi tatu moja atupia, waishusha Kagera Sugar na kukaa nyuma ya Simba...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA mpya, Tariq Seif, aliyesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo akitokea nchini Misri alikokwenda kucheza soka la kulipwa, amepeleka furaha Yanga baada ya kufunga bao pekee dakika ya 84 lililoiwezesha timu hiyo kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Biashara United kutoka mkoani Mara kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana.

**Hata hivyo, mchezaji huyo ambaye ni mechi yake ya kwanza kucheza, akifanikiwa kufunga bao lake la kwanza, hakushangilia bao hilo, badala yake aliweka mikono juu kuomba radhi, kutokana na kuifunga timu yake ya zamani aliyoichezea kabla ya kutimkia Uarabuni.**

Ushindi huo, unaifanya Yanga kuanza kupangua gia za msimamo wa Ligi Kuu Bara, ambapo sasa imefikisha pointi 24 baada ya mechi 11, hivyo kuishusha Kagera Sugar hadi nafasi ya tatu licha ya kucheza mechi 14, lakini timu hizo zikiwa na pointi sawa ila Wanajangwani hao wakinufaika na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Lilikuwa ni bao lililowapa faraja mashabiki wa Yanga ambao tayari walishaanza kukata tamaa na kuona kuwa huenda wangelazimishwa sare ya bila kufungana. Tariq, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya David Molinga, kabla ya bao hilo alipata nafasi mbili, moja akishindwa kulenga lango na nyingine ikipanguliwa na kipa wa Biashara United, Daniel Mgore kabla ya baadaye kupokea krosi safi kutoka kwa mchezaji ambaye pia aliingia kipindi cha pili, Papy Tshishimbi na kuandika bao hilo pekee.

Awali ilikuwa ni kichwa chake kilishindwa kulenga lango, lakini katika dakika ya 60 alipiga kichwa cha kudundisha, na kipa wa Biashara, Mgore aliruka juu na kuupangua na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Mbali na Tariq, Yanga ilimchezesha mchezaji mwingine aliyesajiliwa kwenye dirisha dogo akitokea JKT Tanzania, Adeiyum Saleh.

Kipindi cha kwanza kilikuwa ni cha kupooza kwa timu zote mbili, huku Yanga ikipata nafasi mbili tu za wazi ambazo ilishindwa kuzitumia.

Lakini kipindi cha pili Biashara ilitumia muda mwingi kucheza nyuma ya mpira, huku ilikionekana kuzuia zaidi kuliko kushambulia na hilo ndilo lililowaponza.

Biashara ilifanya shambulio kali moja tu, dakika ya 48 wakati Bright Obina alipopiga shuti lililotoka pembeni kidogo ya lango.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inakaa nafasi ya pili nyuma ya Simba, wakati huu timu hizo zikijiandaa kukutana Jumamosi katika uwanja huo, hata hivyo Kagera Sugar yenye pointi 24, ingeweza kuendelea kung'ang'ania kukaa nafasi pili, lakini jana ilishindwa na kukubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Lipuli ikiwa nyumbani, Uwanja wa Samora mjini Iringa imeiangamiza Mbao FC mabao 3-0, Coastal Union ikiendeleza wimbi la ushindi Uwanja wa Mkwakwani kwa kuichapa Mbeya City mabao 2-0, Mtibwa Sugar ikiduwazwa bao 1-0 nyumbani Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro dhidi ya Alliance FC.

## Simba: Ndanda leo daraja la Yanga J'mosi

**Na Somoe Ng'itu**

MECHI muhimu! Hayo ni maneno ya Kocha Msaidizi wa Simba, Suleiman Matola, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ndanda FC kutoka mkoani Mtwara inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Baada ya mechi ya leo, Simba ambao watakuwa wenyeji, itaingia kambini kujiandaa na mchezo dhidi ya watani zao, Yanga utakaochezwa Jumamosi kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Matola, alisema wamejiandaa kupata ushindi katika mechi ya leo ambayo itakuwa ni sehemu pia ya maandalizi kuelekea mchezo wao dhidi ya Yanga.

Matola alisema kiufundi, mechi hizo ni tofauti, lakini wamejipanga kuingia uwanjani kwa tahadhari kwa sababu wanahitaji kuondoka na pointi tatu muhimu.

Alisema kila mchezaji yuko tayari na wanajua Ndanda wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili waondoke kwenye janga la kushuka daraja.

"Ni mechi muhimu sana kwetu, tunahitaji kushinda ili kuendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi, tunaiangalia Ndanda kwanza, halafu itafuata Yanga, ingawa tukipata matokeo ya ushindi, yataimarisha nguvu ya timu," alisema Matola.

Nahodha huyo wa zamani Simba aliongeza kuwa kila mechi kwao ni sawa na fainali, hivyo wamewaandaa wachezaji kupambana katika dakika zote.

Abdul Mingange, Kocha Mkuu wa Ndanda FC, alisema anaifahamu vema Simba na amewaandaa nyota wake 'kubana njia' ambazo wanazitumia katika kutengeneza mabao.

"Nimewaangalia Simba mechi zao zote, ninajua mahali ambapo wana upungufu, kama tutafanikiwa kuwabana kama tulivyowasoma, naamini tutapata matokeo mazuri, tunahitaji ushindi, ligi haina mwenyewe, hata nyumbani kwao tunaweza kuwasumbua," alisema Mingange.

Aliongeza kuwa amewataka wachezaji wake kutofikiria matokeo ya mechi zilizopita, kwa sababu kikosi cha msimu huu, si walichocheza nacho msimu uliopita.

Simba ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 31 baada ya kucheza mechi 12, wakati Ndanda FC yenye pointi nane imeshacheza michezo 13, iko katika nafasi ya pili kutoka mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo yenye timu 20.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >